NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Hamsini na Nane – Tarehe 26 Juni, 2018

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Moja, leo ni Kikao cha Hamsini na Nane. Katibu

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

### MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Swali la kwanza linaelekezwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na litaulizwa na Mheshimiwa Aisharose Matembe Ndogholi.

Na. 487

**Kuboresha Huduma za Hospitali ya Mtakatifu Gaspar – Itigi**

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE** aliuliza:-

Hospitali ya Mtakatifu Gaspar imekuwa Hospitali ya Rufaa tangu mwaka 2011 na inahudumia wananchi wa Mikoa ya Tabora, Singida na Mbeya. Wakati wa kampeni

mwaka 2015, Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli aliahidi kuipatia vifaa tiba, dawa na watumishi wa kutosha ili kupunguza changamoto wanazokutana nazo wagonjwa:-

Je, ni lini ahadi ya Mheshimiwa Rais itatekelezwa ili kusaidia hospitali hiyo kutoa huduma za afya kwa ufanisi na kuokoa maisha ya wananchi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aisharose Ndogholi Matembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi *(PPP)* katika utoaji wa huduma za afya, Serikali inatoa ruzuku ya fedha kwa ajili ya kulipia mishahara ya watumishi pamoja na ruzuku ya dawa na vifaa tiba. Jumla ya watumishi 50 wa Hospitali ya Mtakatifu Gaspar wanalipwa mishahara na Serikali ambapo ni Daktari Bingwa mmoja (Bingwa wa Upasuaji), Daktari mmoja, Daktari Wasaidizi *(AMO)* wawili, Tabibu wawili, Wauguzi 43 na Mteknolojia wa Maabara mmoja.

Mheshimiwa Spika, mgao wa dawa na vifaa tiba kutoka Bohari ya Dawa *(MSD)* unaendelea kutolewa na Serikali katika Hospitali ya Mtakatifu Gaspar ambapo katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali ilitoa dawa zenye thamani ya shilingi milioni 105.67 na mwaka wa fedha wa 2017/2018 dawa zenye thamani ya shilingi milioni 114.67 zimetolewa katika hospitali hiyo. Aidha, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inaandaa mwongozo wa gharama za matibabu katika hospitali ambazo siyo za Serikali ili kuzifanya hospitali hizo kutoa huduma zenye gharama nafuu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aisharose, nilikuona.

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa hospitali hii inahudumia wagonjwa wengi kutoka Mkoa wa Mbeya, Singida na Tabora lakini ina Madaktari Bingwa wachache; Madaktari Bingwa waliopo ni wanne tu. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha hospitali hii inakuwa na Madaktari Bingwa wa kutosha ili kutoa huduma bora kwa wakati wote?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa gharama za hospitali hii ya *Mission* pamoja na gharama nyingine za hospitali za binafsi ni kubwa sana ambapo wananchi wa kawaida hawawezi kumudu. Kwa mfano, mama anapoenda kujifungua anatakiwa kulipa Sh.150,000 kwa kawaida lakini anapojifungua kwa operesheni anatakiwa kulipa Sh.450,000. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Wilaya ya Itigi inapata Hospitali ya Wilaya?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Josephat Kandege, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala zima la kuwepo Madaktari Bingwa wa kutosha, ni nia ya Serikali kuhakikisha kwamba wanapatikana ili waweze kutoa huduma. Hivi karibuni Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeweza kutoa tangazo kwa ajili ya Madaktari. Naamini katika wale ambao watakuwa wameomba na Madaktari Bingwa watapatikana kwa ajili ya kuwapeleka maeneo kama hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira na swali hili limekuwa likiulizwa mara kwa mara na Wabunge wa Mkoa wa Singida, mnamo tarehe 7 mwezi

huu swali hili liliulizwa na leo linaulizwa kwa mara ya pili. Kwa hiyo, inaonyesha jinsi ambavyo wanajali wananchi wao katika suala zima la afya.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na gharama za matibabu ambazo zinatolewa na hospitali hii na hospitali zingine binafsi, kama ambavyo nimejibu katika jibu langu la msingi tunatarajia mwongozo kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa sababu Serikali inawekeza pesa zake, kuwe na bei ambazo wananchi wanaweza kumudu.

Mheshimiwa Spika, amechomekea na swali lingine kuhusiana na ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Itigi, naomba nimhakikishie ni azma ya Serikali baada ya kuwa tumemaliza hizi hospitali 67, katika maeneo yote ambayo hakuna Hospitali za Wilaya Serikali itaenda kujenga.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Mama Margaret Sitta, swali la nyongeza la wananchi wa Urambo.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubali kwamba Serikali inajitahidi sana kusaidia Hospitali ya Wilaya ya Urambo lakini bado tuna changamoto kubwa ambayo ni ukosefu wa *theater,* ni mradi wa *ADB* ambao ulijenga *theater* pale ikafikia lenta. Je, Serikali inawaliwaza vipi wapiga kura wangu wa Urambo kuhusu kumalizika kwa *theatre* ambayo ipo katika hatua ya lenta?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kama unakumbuka ujenzi wa hilo jengo la upasuaji Urambo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Spika, nilipata nafasi ya kutembelea Urambo na naomba nimpongeze kwa dhati kabisa Mheshimiwa Sitta amekuwa

ni mpiganaji kuhakikisha kwamba afya ya akinamama na watoto kwa ujumla inaboreshwa. Wakafanya kazi nzuri sana, wameanzisha na wodi maalum kwa wale watu ambao wangependa wawe kwenye *grade A,* ni jambo la kupongezwa na wengine ni vizuri tukaiga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona ile *theater* ambayo inajengwa ikafikia usawa wa lenta, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Sitta Serikali itahakikisha kwamba kazi nzuri ambayo imefanyika haiachwi ikapotea, kwa kadri pesa itakavyopatikana tuna wajibu wa kuhakikisha kwamba tunamalizia ile *theater* ambayo ilikuwa imekusudiwa kwa ajili ya kutoa huduma kwa akinamama na watoto. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwalimu Mulugo, swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na mimi kupata swali la nyongeza. Ni wiki mbili zimepita alikuja Katibu wa Hospitali ya Mwambani Bwana Kalindu na nikamwita Mheshimiwa Naibu Waziri tukakaa, tukaongelea habari ya Hospitali ya Mwambani pale Mkwajuni.

Mheshimiwa Spika, kama mnavyojua Songwe ni Wilaya mpya na hatuna Hospitali ya Wilaya lakini hii Hospitali ya Mwambani ndiyo inayotumika kama Hospitali ya Wilaya au Hospitali Teule, lakini watumishi mpaka sasa ni haba na hatupati dawa na hata mgao wa Serikali hauendi kama ambavyo inatakiwa ipewe Hospitali Teule. Ni nini Serikali inatamka juu ya jambo hili na Mheshimiwa Waziri anajua?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Josephat Kandege.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Mulugo alikuja na tukakaa pamoja na Daktari ambaye alikuwa ametoka Hospitali ya

Mwambani. Kimsingi Hospitali ya Mwambani kwa sababu ndiyo hospitali pekee iliyopo inatakiwa itumike kama *DDH.* Ni makosa tu ambayo yalifanyika na naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ndani ya muda mfupi tatizo litakuwa limeshatatuliwa na hospitali ile itatambuliwa kama *DDH* kwa sababu ndiyo hospitali ambayo ni tegemeo kwa wananchi wa Mwambani na Chunya kwa ujumla wake. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kaunje, Mbunge wa Lindi Mjini, uliza swali lako, tafadhali.

Na. 488

**Mkopo na Posho kwa Wenyeviti wa Serikali za Mitaa**

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH (K.n.y. MHE. HASSAN S. KAUNJE)** aliuliza:-

(a) Je, ni lini Serikali itadhamini Wenyeviti wa Serikali za Mitaa ili waweze kupata mikopo kama ilivyo kwa Madiwani na Wabunge?

(b) Je, ni lini Serikali itaanza kuwalipa posho/ mishahara Wenyeviti wa Serikali za Mitaa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Seleman Kaunje, Mbunge wa Lindi Mjini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, utaratibu wa Halmashauri na Bunge kudhamini mikopo kwa Waheshimiwa Madiwani na Waheshimiwa Wabunge umetokana na kuwepo kwa utayari wa benki zinazokopesha mikopo hiyo, hususan *NMB* na *CRDB* ambazo baada ya kuonesha utayari, makubaliano maalum husainiwa ambayo ndiyo hutoa mwongozo wa namna mikopo itakavyotolewa pamoja na viwango vyake.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa aina hiyo hadi sasa haujawezekana kwa Wenyeviti wa Serikali za Vijiji, Mitaa na Vitongoji kwa kuwa hadi sasa hakuna benki iliyoonesha utayari wa kutoa mikopo ya aina hiyo. Hata hivyo, ipo fursa kwa kiongozi mmoja mmoja kuwasiliana na benki moja kwa moja kwa ajili ya makubaliano binafsi ya mkopo kulingana na kiwango cha amana alichonacho, thamani ya ardhi, nyumba anayomiliki au biashara.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kazi kubwa inayofanywa na Wenyeviti wa Serikali za Vijiji, Vitongoji na Mitaa kupitia Mpango wa Maboresho ya Serikali za Mitaa, Serikali ilitoa mwongozo kuwa viongozi hao wawe wanalipwa posho inayotokana na asilimia 20 ya mapato ya ndani ambayo hurejeshwa na Halmashauri kwenye Kijiji/Mtaa husika.

Mheshimiwa Spika, changamoto zilizopo za ukusanyaji hafifu wa mapato ya ndani zimekuwa zikisababisha ugumu wa kutekeleza mwongozo huo katika baadhi ya maeneo. Kwa sababu hiyo, Halmashauri zote zimeagizwa zifanye mapitio ya vyanzo vyote vya mapato na ziimarishe makusanyo ya ndani ili ziwe na uwezo wa kulipa posho hizo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamida Abdallah, swali la nyongeza.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nishukuru kwa majibu hayo ambayo yamejibiwa sasa hivi lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, Madiwani wanafanya kazi sawa na Wabunge. Kwa nini Serikali isiwalipe mishahara kama ambavyo Wabunge wanapewa mishahara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni kwa nini Wenyeviti wa Serikali za Mitaa, sasa hivi Serikali haijaona umuhimu wa

kuwalipa posho ambayo wanastahili kupata maana wanalipwa posho ndogo sana. Serikali ingeona umuhimu kwa sababu wao wanasimamia kazi za miradi ya maendeleo katika mitaa. Kwa hiyo, ningeomba sasa Serikali ifanye maamuzi ya kuwaongezea posho ili waweze kukidhi mahitaji yao. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mnapouliza maswali haya msilinganishe sana na Wabunge kwa sababu na Wabunge nao wana malalamiko posho haitoshi. *(Kicheko/ Makofi)*

Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA) :** Mheshimiwa Spika, katika swali lake la kwanza, ni kweli kwamba Madiwani wamekuwa na mtazamo huo wa kuomba kwamba kuwe na malipo hayo ya mshahara, Serikali iliyapokea na hata wakati Rais alivyohudhuria kikao cha *ALAT* mwaka jana alipokea maombi yao. Mimi nasema tu kwamba majibu yaliyotolewa pale ndiyo sahihi na hadi hapo Serikali itakapotoa maelekezo mengine lakini kwa sasa hivi tutaendelea na utaratibu ambao tunao.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili kuhusu Wenyeviti wa Serikali za Vijiji, Vitongoji na Mitaa kwamba posho ni ndogo sana, msisitizo ambao tunautoa sisi kila Halmashauri ifanye mapitio *(review)* ya vyanzo vyake vya ndani pamoja na mbinu zao za makusanyo, wakusanye kiwango cha kutosha cha mapato ya ndani na wahakikishe kwanza, hata hiyo ndogo maana maeneo mengine mengi tuna malalamiko kwamba hawalipi, hata hiyo ndogo basi inalipwa baada ya hapo sasa ndiyo tutaona tunaendaje huko mbele. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hasna Mwilima, nilikuwa nimekuona, swali tafadhali.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Posho ya Wenyeviti wa Serikali za Vijiji kwenye Halmashauri zingine hawalipwi kabisa. Sasa nataka niulize tu swali kwa nini Wizara ya TAMISEMI isitoe Waraka Maalum kwenda chini kwa Wakurugenzi wote kuwaelekeza kwamba katika *own source* za Halmashauri wawe wanatoa kiasi fulani kwa ajili ya Wenyeviti wa Vijiji huku tukijua hao ndiyo wanaotusaidia kufanya kazi kubwa za maendeleo kwa niaba ya Serikali? *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa, kule Halmashauri kuna hela basi jamani? Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA) :** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika swali la msingi, huo Waraka ambao Mheshimiwa Mbunge anaupendekeza ulitolewa mwaka 2003, lakini kwa sababu umekuwa ni wa muda mrefu pengine labda baadhi ya wenzetu wanaanza kuusahau, basi tutachukua ushauri wake ili tutoe maelekezo tena.

Mheshimiwa Spika, msisitizo ni kwamba lazima Halmashauri zote zifanye mapitio ya vyanzo vyao vya mapato, waongeze mbinu za ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kusudi wawe na uwezo mzuri wa kuweza kulipa. Hii ni kwa sababu hata taarifa za *CAG* zinaonesha kwamba ile asilimia 20 katika baadhi ya Halmashauri imekuwa hairudi kule kwenye vijiji kwa sababu tu ya malalamiko kwamba wamekusanya kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waitara nilikuona, swali la mwisho la nyongeza kwenye eneo hili.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Mimi ni Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa Mstaafu, Mtaa wa Kivule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Serikali kutokutoa maelekezo mahsusi ya Wenyeviti wa Mitaa kulipwa posho inapelekea mzigo huu kupelekwa kwa wananchi ndiyo matokeo ya zile barua ambazo zinalipiwa, wananchi wanatwishwa mzigo huu. Kwa hiyo, ningeomba nijue, kwa kuwa Serikali imechukua vyanzo mbalimbali vya mapato kutoka Halmashauri na Halmashauri haipeleki fedha hizo kulipa Wenyeviti wa Mitaa na wanafanya kazi kubwa masaa 24.

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini isiwekwe sheria moja kwa moja ili wadai kama haki? Kwa sababu sasa hivi ni posho kwa hiyo hawana uhalali wowote ule, Halmashauri inaamua ilipe ama asilipe. Ni kwa nini Serikali isiwajali watu ambao ni wengi sana katika nchi hii, wanafanya kazi kubwa sana ya miradi, ulinzi na usalama, usafi na ku-*impose* sheria mbalimbali walipwe pesa ya kisheria badala ya hii ambayo ni hiari?

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la Mheshimiwa Waitara kutoka TAMISEMI, Mheshimiwa Joseph Kakunda, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA) :** Mheshimiwa Spika, kama anavyosema ni kweli Wenyeviti wa Serikali za Vijiji, Vitongoji na Mitaa wanafanya kazi kubwa na nyingi na kweli mzigo ni mkubwa sana kwa upande wao. Sisi kama Wabunge na Serikali tunawategemea sana katika kazi zetu za kila siku. Ili kazi zetu na za Serikali ziende lazima wale wafanye kazi.

Mheshimiwa Spika, sasa mapendekezo ambayo anayatoa na kuhusisha kwamba Serikali imechukua vyanzo vingi vya mapato kwenye Halmashauri, mimi nataka nimhakikishie kwanza kwamba vyanzo ambavyo vimechukuliwa siyo vingi…

**WABUNGE FULANI:** Aaaaa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA) :** Mheshimiwa Spika, vyanzo vingi bado vipo katika Halmashauri na ndiyo maana tumewaambia kwamba wafanye mapitio. Wakishafanya mapitio Halmashauri ambayo itakuwa na changamoto za ziada basi wataleta taarifa TAMISEMI na tutaweza kuifanyia kazi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata la Mheshimiwa Zuberi, Mbunge wa Liwale.

Na. 489

**Mgogoro wa Mpaka wa Wilaya ya Liwale na Wilaya ya Kilwa**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA** aliuliza:-

Kumekuwa na mgogoro wa muda mrefu wa mpaka kati ya Wilaya ya Liwale na Wilaya ya Kilwa:-

Je, ni lini Serikali itamaliza mgogoro huo ili kuleta amani katika Wilaya hizo kabla amani haijatoweka?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la wananchi wa Mirui, Mtawawa, Mkundi, Makonjiganga, tafadhali Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kilwa ilianzishwa kwa Tangazo la Serikali Na. 91 la tarehe 16 Mei, 1947 na Wilaya ya Liwale ilianzishwa kwa Tangazo la Serikali Na.185 la tarehe 5 Desemba, 1980. Hadi hapo hakukuwa na mgogoro wowote. Tangazo la Serikali Na. 134 la mwaka 1983 lilianzisha

Halmashauri za Wilaya ambapo Mirui iliorodheshwa kama kata na kijiji katika Halmashauri ya Wilaya ya Liwale na haikutajwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inautambua mgogoro huo unaohusu mkanganyiko ulioko kati ya Kitongoji cha Mirui katika Kijiji cha Nanjirinji A, Kata ya Nanjirinji, Wilayani Kilwa kwa upande mmoja na Kijiji cha Mirui katika Kata ya Mirui Wilayani Liwale kwa upande wa pili.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mgogoro huo ni sehemu ya migogoro mingi inayoshughulikiwa na Serikali chini ya uratibu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, nashauri Mbunge na wananchi wa maeneo husika wawe na subira wakati huu ambapo Serikali imetuma wataalam kwenye eneo hilo la mgogoro wanaofanya mapitio ya kina ya matangazo ya kuanzisha wilaya zote mbili na tangazo la kuanzisha halmashauri zote mbili kwa lengo la kuhakikisha mgogoro huo unapatiwa ufumbuzi wa kudumu ndani ya mwaka 2018/2019.

**SPIKA:** Swali la nyongeza, Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, Mbunge wa Liwale.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu yanayoridhisha ya Mheshimiwa Waziri, mgogoro huu, kama mwenyewe anavyokiri ni wa muda mrefu na mimi nimeshakwenda kwa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi akaniambia kwamba mgogoro huu bado uko kwenye ngazi ya mkoa, watakaposhindwa ngazi ya mkoa watauleta Wizarani. Nimekwenda kwa Mkuu wa Mkoa ameniambia kwamba yeye ameshauandikia Wizarani kwa maana ya kwamba wameshashindwa.

Mheshimiwa Spika, hata h ivyo, mimi mwenyewe binafsi nimemuandikia Mheshimiwa Waziri kumjulisha mgogoro huu mpaka sasa hivi sijapata majibu yoyote. Sasa kutokana na huu mkanganyiko wa kauli za Serikali, Mkuu wa Mkoa anasema hili na Waziri anasema lingine, nini kauli ya Serikali juu ya mgogoro huu yaani nani kati yao yuko sahihi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, anasema mgogoro huu utashughulikiwa mwaka huu wa 2018/2019. Je, Mheshimiwa Waziri, yuko tayari kuandamana na mimi baada ya Mkutano huu twende akaangalie hali halisi? Kwa sababu tayari watu walishaanza kuchomeana ufuta, juzi hapa ufuta wa Kijiji cha Mirui umekatwa na wananachi wa kutoka Kilwa.

**SPIKA:** Hivi upande wa Nanjirinji Mbunge wake ni Mheshimiwa Bwege au Mheshimiwa Ngombale?

**MBUNGE FULANI:** Ni Mheshimiwa Bwege.

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Kuchauka mnashindwa kukaa ninyi wawili mkalimaliza?

Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo. Naibu Waziri wa Ardhi amesimama, tafadhali Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Angeline Mabula. Pole sana kwa msiba Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya familia, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa namna ambavyo wameshiriki katika msiba huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni wiki mbili tu kabla ya msiba nilikuwa kule na nimefika mpaka kwenye jimbo lake. Taarifa nilizozipokea kutoka mkoani, walisema migogoro yote walikuwa wameorodhesha na wakasema kama mkoa wameunda timu za kiwilaya wanashughulikia migogoro yao, itakapowashinda wataileta Wizarani na taarifa ya maandishi wamenipa.

Mheshimiwa Spika, nataka tu nimhakikishie kwamba pamoja na kwamba timu ya Wizara iko kule katika kushughulikia ule mgogoro, lakini pia mkoa ulijiridhisha na ukaniridhisha pia mimi nilipokuwa kule kwamba migogoro

yao wanaisimamia wenyewe kwa sababu haijawashinda na wakikamilisha Wizara itakwenda kuweka mipaka, hasa katika yale maeneo ambayo yana utata wa mipaka.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, nimekuona, tafadhali.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Kama ilivyo Liwale, Wilaya ya Hanang kila upande imezungukwa na migogoro ya mipaka kati yake na Mbulu, Singida na Kondoa. Nataka kujua TAMISEMI itachukua hatua gani, kwa sababu imekuwa muda mrefu mno, hatimaye watu watauana kule ili haya matatizo ya mpaka yanayotukabili yaweze kutatuliwa na watu waishi kwa amani? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Migogoro ya mipaka iko mingi katika maeneo mengi lakini suluhisho la kwanza katika kutatua ile migogoro ni kwa pande zote mbili za maeneo husika kukaa. Kwa hiyo, pale wanapokuwa wamekaa wamekubaliana kwa pande zote mbili na hasa panapokuwa na utata, hapo ndipo Wizara inakuja kuingia kwa ajili ya kusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe tu, pamoja na swali la Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu na wengine ambao wana migogoro, pale inaposhindikana ndipo hapo tunatakiwa kuingilia kati kwa sababu huwezi kuingilia kati kabla pande zote mbili hazijakaa na kuridhia na kwa kuangalia zile *GN* zilizounda maeneo hayo ziko katika utaratibu upi.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Twende Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, swali la Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nami nikushukuru na nikupongeze kwa dhati kabisa kwa jinsi unavyoendesha vikao hivi hasa ukiwa makini kutetea *backbenchers*.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba Serikali itoe majibu ya swali na.490 na naomba Mawaziri wasikasirike. *(Kicheko)*

Na. 490

**Mawaziri Kutopatikana kwenye Simu**

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB** aliuliza:-

Mawaziri kama walivyo viongozi wengine wa Serikali, wapo kwa ajili ya kuwahudumia wananchi na kwamba wananchi wamewachagua Wabunge na Mawaziri (Serikali) ili kuwasiliana, kushirikiana na kushauriana katika kutatua kero zao; lakini kwa bahati mbaya sana wapo baadhi ya Mawaziri ambao kupatikana kwao hata kwenye simu ni jambo gumu kupita kiasi:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa ipo haja ya Mawaziri wenye tabia hiyo ya kujichimbia na kutopatikana kwenye simu kuacha tabia hiyo kwa maslahi ya wananchi?

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kuwa ipo haja ya kuweka utaratibu maalum wa kuifikia Serikali iwapo wananchi kupitia Mbunge wao wana shida ya kumuona Waziri anayehusika na akawa hapatikani hata kwa simu?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Kapteni Mstaafu Mkuchika na unaombwa usikasirike. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mbunge anayewakilisha pia

Baraza la Wawakilishi, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni B.3(1) ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 2009, simu ni moja ya njia za mawasiliano halali Serikalini. Waheshimiwa Mawaziri wanafanya kazi zao kwa lengo la kuwahudumia wananchi na wananchi nao wana nafasi ya kutoa maoni na shida zao na hatimaye kupata mrejesho. Mpaka sasa Serikali haina ushahidi wa kuwepo Mawaziri ambao kwa makusudi hujichimbia na kutopatikana kwa simu. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, zipo njia mbalimbali ambazo wananchi wanaweza kuzitumia kuwasilisha maoni na kero zao ofisini kwa Waziri licha ya simu peke yake. Wananchi wanaweza kuandika barua, kupiga simu, barua pepe kwa viongozi na watendaji wa Wizara kama Makatibu Wakuu au Makatibu wa Waheshimiwa Mawaziri na taarifa za wananchi zitamfikia Mheshimiwa Waziri na kufanyiwa kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jaku, swali la nyongeza.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri kutokuwa na afya kwa upande wangu, niwapongeze sana Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa *Engineer* Atashasta Nditiye na Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, kwa kupokea simu kwa wakati, niwapongeze sana kwa hili na wengine naomba wafuate mfano huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, hizo Kanuni nani anazisimamia ili hao Mawaziri ambao wamo humu ndani, hawapokei simu zikiwemo za Wabunge, mbali na za wananchi, ili hatua zichukuliwe? Ikiwa namba za ma-*RPC* ziko hadharani na ziko katika mtandao, sababu gani zinazosababisha Mawaziri hao namba zao zisiwe hadharani? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, Mheshimiwa Waziri kabla ya kupata Uwaziri hapa, Mheshimiwa Spika ni shahidi, alikuwa mkali kutetea wananchi wake na akawa ngangari kwelikweli. Ni lini Mawaziri namba zao zitatangazwa hadharani ili wananchi na Wabunge watakapowapigia simu wapokee?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Kapteni Mstaafu Mkuchika, tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, maswali yake kwa kweli ni moja lilelile limejirudia lakini pia nafikiri kuna mchanganyiko kidogo katika swali lake. Analalamika kwamba Mawaziri hawapatikani kwa simu lakini wakati huohuo analalamika kwamba namba zao haziko hadharani. Sasa hao ambao huwapati kwa simu ni wapi kama simu zao hunazo? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kujibu swali lake, nani anazisimamia hizo Kanuni nilizozitaja? Kanuni zinasimamiwa na Serikali, kila Wizara kuna viongozi wake na Wizara ya Utumishi inasimamia Kanuni zote za watumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, sasa ilimradi tumeshasema katika jibu la msingi kwamba hatuna ushahidi wa Waziri ambaye kwa makusudi hataki kupatikana, ndiyo maana hatujamchukulia hatua maana hatuna taarifa hizo. Kila Waziri hapa ana mkubwa juu yake, akizileta kama mimi siyo *size* yangu nitazipeleka juu, lakini atuletee na siyo kwako wewe tu, Mtanzania yeyote yule ambaye anaona kwamba hakutendewa haki, hampati Waziri kwa makusudi, hilo kwa makusudi naliweka kwenye, Wazungu wanasema *inverted commas,* maana yake mimi sina ushahidi nalo hilo.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana kila Wizara kuna sanduku la maoni. Sanduku lile una jambo la kuishauri Wizara,

una jambo umetendewa vizuri na Wizara unaandika unawapongeza, una jambo umefanyiwa vibaya na Wizara unaandika unawasema.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kapteni Mkuchika kwa majibu mazuri ya swali hilo kuhusu Waheshimiwa Mawaziri. Mheshimiwa Mkuchika lakini Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakiniandikia hapa, sina majibu, wananiuliza kuhusu Yanga, wanasema hivi Yanga bado ipo au? *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, swali la Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba nikutaarifu tu kwamba Yanga bado ipo. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 491

**Kuzuia Shughuli za Uvuvi Katika Ziwa Viktoria**

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA** aliuliza:-

(a) Je, ni utafiti gani umefanyika katika Ziwa Victoria mpaka kufikia hatua ya kuzuia uvuvi wa aina yoyote kwa kisingizio cha uvuvi haramu?

(b) Je, ni sheria gani inatumika kukamata nyavu na ndani ya dakika kumi zinachanwa bila ya kumpa mvuvi nafasi ya kujitetea?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mbunge wa Geita Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali haijazuia uvuvi wa aina zote kufanyika katika Ziwa Viktoria. Uvuvi unafanyika nchini kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2009 pamoja na sheria nyingine za nchi yetu. Aidha, kwa sasa Serikali inapambana na uvuvi haramu katika Ziwa Viktoria kama ilivyo katika maeneo mengine kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, upo utaratibu wa kisheria wa kukamata na kuharibu zana za uvuvi zinazotumika katika uvuvi haramu. Taratibu hizo zimeelezwa vizuri kwenye Kanuni Na. 50(1), (2) na (5) ya Kanuni za Uvuvi za mwaka 2009. Aidha, nyavu haramu huteketezwa kwa idhini ya Mahakama baada ya taratibu zote za kisheria kufuatwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Musukuma, swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Dhana ya uvuvi haramu imeenea sana kwenye kauli za Mawaziri, lakini kule ziwani kuna aina za samaki kama 30 na samaki pia wana makuzi tofauti, ni kama binadamu. Ukichukua umri wa Musukuma ukachukua na umri wa Mwalongo, tuko sawa, lakini ukituangalia kwa maumbile tulivyo tuko tofauti na unapotupa nyavu ziwani inakuja na samaki za aina tofauti wakiwepo wenye tabia kama yangu na Mwalongo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ukiwapima kwenye rula hawalingani lakini umri ni mmoja. Kwa kuwa sheria yenyewe ndiyo inajichanganya, ni lini Wizara itakuja na sheria ambayo itam-*favour* pia mvuvi anapokumbana na matatizo kama ya maumbile ya binadamu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Mheshimiwa Waziri wakati operesheni hii inapoendelea, kumekuwa na tabia ya kukamata nyavu saa nne na zinachomwa saa sita. Mfano mzuri ni kwenye Kisiwa cha Izumacheri kilichopo Jimbo la Geita Vijijini ambapo Maafisa Uvuvi walikamata nyavu

ambazo siyo haramu lakini wakanyimwa rushwa, wakachoma nyavu dakika 15 zilizofuata na nyavu hizi ni halali. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kufuatana na mimi kwenda kusikiliza *SACCOS* hiyo na kutoa adhabu kwa wale waliohusika na suala hili? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la lini Serikali itakuja na sheria mpya itakayowasaidia wavuvi waweze kufanya shughuli zao kwa uzuri zaidi, hasa ikizingatiwa hili analolisema la kwamba samaki wako wa aina tofauti na ile nyavu inapoingia inakwenda kuzoa hata wengine wasiohusika.

Mheshimiwa Spika, Serikali tupo katika hatua ya mwisho ya maboresho ya Sheria yetu ya Uvuvi na itakapokuwa tayari itaingia humu Bungeni ambapo Waheshimiwa Wabunge watashiriki kikamilifu katika kuhakikisha kwamba sheria ile tunaiboresha kwa pamoja kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ameeleza juu ya suala linalohusu nyavu, ya kwamba nyavu hizi zinapokamatwa ghafla tu zinachomwa moto na akanitaka kama niko tayari niweze kufuatana naye kwa ajili ya kuweza kwenda kuwachukulia hatua wale watumishi wa Serikali ambao wanatenda kinyume.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Musukuma na Waheshimiwa Wabunge wote na hata wananchi wote wanaoshughulika katika shughuli hizi za uvuvi, Wizara yangu tuko tayari kabisa sisi kama viongozi kwa *specific cases* kama hii anayoizungumzia Mheshimiwa Musukuma, tutakwenda popote pale na endapo tutabaini watumishi wetu wametenda kinyume sisi kama Mawaziri tuko tayari kuwachukulia hatua kwa ajili ya mustakabali mpana zaidi wa wananchi na wavuvi wetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hili swali tulibakize kulekule Kanda ya Ziwa, Mheshimiwa Constantine Kanyasu na Mheshimiwa Joseph Mkundi wa Ukerewe.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Kwa mujibu wa Kanuni za Uvuvi, ukienda kifungu cha 45(3)(b), naomba nisome, kinasema:-

*"No person shall:*

*(b) fish, land or possess, process or trade in Nile tilapia or fish locally known as "Sato" the total length of which is below 25 centimetres."*

Mheshimiwa Spika, ukisoma Kanuni hii, ni kama inafikiria *source* ya Sato ni moja tu, *Nile Tilapia* lakini sasa Tanzania tuna-*encourage* watu kufanya *aquaculture,* maana yake *sources* za sato ziko nyingi, lakini tuna maziwa na mito na Kanuni hii imetumika kusababisha usumbufu mkubwa sana kwa watumiaji wa sato nchi nzima. Ni lini Serikali au ni kwa nini Serikali isisitishe sasa kukamata watu kwa kutumia Kanuni hii ambayo yenyewe tu inajichanganya na ina makosa mpaka itakapofanyiwa marekebisho? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Luhaga Mpina, majibu tafadhali.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, nishukuru sana kwa swali hili la nyongeza la Mheshimiwa Kanyasu, lakini nimpongeze sana Naibu wangu kwa majibu mazuri sana aliyoyatoa hapo awali.

Mheshimiwa Spika, kama alivyoisoma Kanuni yetu na kama Naibu Waziri alivyoeleza, mwezi huu wa Saba, Wizara yangu itakuwa imemaliza zoezi la kufanya mapitio ya Kanuni ya Uvuvi pamoja na Sheria yenyewe ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003. Vilevile kwa nyongeza ni kwamba operesheni hizi zinazoendelea na wananchi wetu ambao wanajishirikisha

na ufugaji wa samaki, kila wanapofikia kuvuna samaki wao wanawasiliana na ofisi yangu ambayo inakuwa inazo taarifa za uhakika juu ya uvunaji wa samaki hao ili kusije kukatokea usumbufu wa aina yoyote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika kipindi ambacho Kanuni inarekebishwa, utaratibu umewekwa na Wizara kwa maana ya kwamba mawasiliano yako *proper* ya namna ya uvunaji kwa sasa wakati tunatengeneza Kanuni ambayo itakuwa ime-*favour* uvunaji wa samaki katika Ziwa Viktoria lakini wakati huohuo na wale wafugaji wetu wa samaki ambao wanafuga samaki kwenye maji.

**SPIKA:** Nilikuwa nimekutaja Mheshimiwa Joseph Mkundi, Mbunge wa Ukerewe na Mheshimiwa Dkt. Chegeni atakuwa wa mwisho kwenye eneo hili.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kuwa baada ya operesheni nyavu zinazotumika sasa ni mbovu sana, hazina kiwango na wala hazistahili kutumika kwa uvuvi, zinawatia hasara sana watumiaji. Je, Serikali ina mpango gani wa haraka kupata nyavu zinazostahili, zinazoweza kukabiliana na mazingira ya Maziwa Viktoria, Tanganyika na mengineyo ili wavuvi wetu mbali na kupata hasara za kuchomewa nyavu wasiendelee kupata hasara za kununua nyavu kila siku chache zinapokuwa zinapita? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, juu ya suala linalohusu ubora wa nyavu, ni kweli Wizara yangu imepokea malalamiko kutoka kwa wavuvi kutoka pande zote za nchi yetu hasa wavuvi wa Ziwa Viktoria na tumekwenda kujiridhisha. Tupo katika utaratibu wa kuendelea kufanya tathmini ya hali hii. Nataka nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge kwamba tunashirikiana vyema na

wenzetu wa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa ajili ya kuweza kupata viwango halisi vya ubora wa nyavu zetu zinazozalishwa nchini.

Mheshimiwa Spika, pale itakapobainika kwamba liko tatizo juu ya ubora huu, la kwanza tutawataka ama tunawataka wazalishaji wetu waongeze viwango vyao vya ubora, lakini ikibidi sisi kama Wizara tuko tayari kutafuta mpango mwingine wa kuweza kuwanusuru wananchi wetu ili waweze kuendelea na shughuli hii ya uvuvi bila ya tatizo lolote.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chegeni, swali kutoka Busega.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Zoezi la uvuvi haramu limetekelezwa sivyo ndivyo katika maeneo mengi sana na wavuvi wengi sana wamepata hasara kubwa sana kutokana na zoezi hili. Zoezi hili limefanywa na wafanyakazi ambao kwa kweli hawakuzingatia maadili na hata kanuni za kazi zao. Ilifikia mahali Mheshimiwa Waziri akasema kwamba yeye hana wapiga kura wavuvi hao wenye wapiga kura wavuvi mtajijua wenyewe. Nataka kujua kauli ya Serikali, wavuvi ambao wameingizwa hasara kubwa sana watalipwa fidia kiasi gani na lini fidia hiyo italipwa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Luhaga Mpina, tafadhali.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, suala la uvuvi haramu tumeeleza mara kwa mara hapa Bungeni na jinsi ambavyo linaendeshwa. Waheshimiwa Wabunge tumewaomba mara kwa mara kwamba kama kuna mtu ambaye ameonewa katika eneo lolote lile tuletewe ili sisi tuweze kuchukua hatua. Leo ni miezi sita Wizara yangu inasisitiza suala la watu walioonewa kuwasilisha malalamiko yao ili waliohusika waweze kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo Wizara yangu haiwezi kujua ni kitongoji, kijiji na kata gani, ni lini, Mkaguzi nani na alifanya makosa yapi kwa sababu hatua za ukamataji zipo. Sasa ikiendelea kuzungumzwa hivi kila siku kwamba watu wameonewa, halafu ushahidi hupewi, Waziri huwezi kuwa kwenye nafasi ya kuchukua hatua.

Mheshimiwa Spika, hili Bunge ndiyo linalotunga sheria, kwa nini Waziri alaumiwe na kuandamwa kwa kuchukua hatua za watu ambao wamevunja sheria? Nataka niseme kwamba wananchi na watu wote wataendelea kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria tulizonazo leo na kwa mujibu wa Katiba tuliyonayo sasa, watakaguliwa mahali popote na wakibainika watachukuliwa hatua. Watu wote wanaojihusisha na uvuvi haramu bila kujali vyeo vyao, wataendelea kuchukuliwa hatua mahali popote walipo kwa mujibu wa sheria tulizonazo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inasisitiza kama kuna mtu yeyote ambaye ana ushahidi dhidi ya manyanyaso au uonevu wa aina yoyote umefanywa na Afisa wangu siku hiyo hiyo hatua zitachukuliwa.

**SPIKA:** Nami niongeze, Waheshimiwa Wabunge wale mnaotoka Kanda ya Ziwa, kama kuna malalamiko mleteeni Spika. Leteni hapa na sisi tutaipa Serikali iweze kuangalia kwa sababu si nia ya Serikali wala mtu yeyote kuona kwamba mtu yeyote anaonewa popote pale katika nchi hii.

Waheshimiwa Wabunge, kwenye zile Kanuni ningeshauri sana pia, kwa sababu hili ni jukumu lenu peke yenu Serikali lakini Kamati yetu inayohusika na mambo ya uvuvi nao kidogo watazame ili waweze kutoa ushauri wa ujumla. *(Makofi)*

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo na swali la Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, Mbunge wa Itilima, Mheshimiwa Silanga, tafadhali.

Na. 492

## Kuporomoka kwa Zao la Pamba Nchini

**MHE. NJALU D. SILANGA** aliuliza:-

Tanzania ni nchi yenye mazao ya biashara kama pamba, korosho, tumbaku na kahawa. Zao la pamba linazidi kuporomoka kutoka wastani wa ekari moja kilo 400 hadi kilo 120 kwa ekari moja ikilinganishwa na nchi kama China ekari moja kilo 2,000, India kilo 1,500, Burkina Faso kilo 1,200 na wastani wa uzalishaji wa dunia ni kilo 1,200 kwa ekari moja:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kunusuru zao hilo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Silanga, kule Kongwa kuna ngoma inaitwa Silanga acha kabisa, siku moja nitakupeleka ukaione. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, Mbunge wa Jimbo la Itilima, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza Mkakati wa Kuendeleza Zao la Pamba unaoratibiwa na Bodi ya Pamba Tanzania kwa lengo la kuhakikisha kuwa tija na uzalishaji wa pamba nchini vinaongezeka. Kutokana na utekelezaji wa mkakati huo, uzalishaji wa pamba msimu 2017/2018 unatarajiwa kufikia zaidi ya tani 600,000. Aidha, mafanikio hayo yanatokana na upatikanaji wa mbegu bora, viuatilifu, huduma za ugani, uchambuaji na uongezaji thamani wa zao hilo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau imeanzisha Mkakati wa Kuzalisha Pamba hadi Mavazi kwa maana ya (*Cotton to Clothing Strategy 2016-2020)* ambao

unatarajia kuongeza uzalishaji wa pamba kutoka wastani wa kilo 600 hadi 700 kwa ekari kwa sasa na kufikia kilo 1,800 kwa ekari ifikapo mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, aidha, mkakati huo unalenga kuongeza utengenezaji wa nyuzi kutoka wastani wa tani 30,000 kwa mwaka hadi kufikia tani 90,000 ifikapo mwaka 2020 pamoja na kuongeza mauzo ya bidhaa za pamba nje ya nchi kutoka wastani wa Dola za Marekani milioni 30 hadi kufikia milioni 150 kwa mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha ongezeko la tija na ubora wa pamba, Serikali imechukua hatua ya kuimarisha mfumo wa uzalishaji wa mbegu za pamba ambapo kuanzia msimu 2018/2019, maeneo yote yanayolima pamba yatatumia mbegu aina ya *UKM08* na kuachana kabisa na mbegu aina ya *UK91* ambayo haina ubora. Aidha, aina mpya ya mbegu za pamba *UK171* na *UK173* zilizoidhinishwa mwezi Januari, 2018 zinaendelea kuzalishwa kwa wingi na zitaanza kuwafikia wakulima kuanzia msimu wa kilimo cha pamba wa 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Swali la nyongeza, Mheshimiwa Mbunge Itilima, tafadhali Mheshimiwa Silanga.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza ahsante sana kwa kunialika kwenda kuona ngoma, niko tayari kwenda huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza Naibu Waziri wa Kilimo kwa majibu yake mazuri aliyonijibu. Hivi sasa maeneo mengi yameonekana kuwa na ugonjwa wa mbegu hii *UKM08*. Je, Serikali inatoa tamko gani kwa wakulima wa zao la pamba kwa maeneo ambayo yanaathirika na ugonjwa huu *Fusarium* hasa ikizingatia kwamba viuatilifu vinavyokuja havifikii viwango na kusababisha mashamba mengi kuharibika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri ameelezea kwamba kuna mkakati mzuri kwa mwaka 2016/2017 ekari moja imeweza kuzalisha kilo 300 lakini kwa mwaka 2016/2017 wastani ambao tumeweza kukusanya kwa nchi nzima kwa maana kwa mikoa 17 na wilaya 56 ni takribani kilo milioni 120. Kwa hiyo, atakubaliana nami kwamba zao la pamba linazidi kuporomoka. Ukigawanya kwa wastani katika zao zima kwa nchi nzima ni Mkoa mmoja tu wa Simiyu wenye kuzalisha kilo 70,000 na mikoa 16 ndiyo unaigawanya. Kwa hiyo, kama Wizara iko shughuli ya kufanya kuhakikisha zao hili linaongezeka kwa uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la Mheshimiwa Silanga pamoja na ushauri alioutoa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, awali kabisa, naomba nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa sababu amekuwa akifuatilia sana juu ya zao zima la pamba na hasa ukizingatia na yeye pia ni mfanyabiashara wa zao hili la pamba.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye maswali yake mawili madogo ya nyongeza kwa ufupi kabisa na kwa pamoja ni kwamba zao la pamba kama zao la pamba na mbegu, sisi kwenye zao la pamba zile mbegu huwa inachukua muda mrefu sana na ukizingatia kwamba mbegu hizo tunazosema utafiti unafanyika muda mrefu muda wa karibu sana na kwa haraka ambao unaweza ukafanyika ni ile miaka mitano. Kwa maana hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote wajue kabisa kwamba suala zima la utafiti huwa linachukua muda mrefu na muda mfupi ambao unaweza ukafanyika ni kipindi cha miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake lile la pili la nyongeza kwamba kwa nini kilimo hiki cha zao la pamba kimeporomoka, ni kweli kwamba wakulima walikuwa hawafuati zile kanuni bora za kilimo cha pamba. Nichuke fursa hii kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri

Mkuu kwa sababu amekuwa ni *champion,* amekuwa akihamasisha na akiwaeleza hata Wakuu wa Mikoa juu ya ufuatiliaji wa zao zima la pamba.

Mheshimiwa Spika, vilevile amemuagiza hata Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kuboresha suala zima la ugani. Pia kama Serikali tumejipanga kuhakikisha kwamba katika msimu wa 2018/2019, tutaboresha zao la pamba kutoka hiyo tani 300,000 kwa ekari hadi tani 600,000 kwa kuzingatia hayo maelezo ambayo nimesema ili wakulima wote nchini waweze kuhakikisha kwamba wanafuata kanuni bora za kilimo cha pamba.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Tunaendelea na swali linalofuata la Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wa Buhigwe.

Na. 493

**Fidia kwa Wakulima wa Kahawa Buhigwe**

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawalipa wakulima 435 wa kahawa waliodhulumiwa katika Jimbo la Buhigwe?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Albert Obama Ntabalika, Mbunge wa Jimbo la Buhigwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2011/2012, Kikundi cha Wakulima wa Kahawa cha *Kalinzi Organic* kilipeleka jumla ya tani 15.8 za kahawa yenye thamani ya Dola za Kimarekani 74,397.24 kwa Kampuni ya Tanganyika *Coffee Curing Co*.Ltd kwa ajili ya kukobolewa na baadaye kuuzwa mnadani. Hata hivyo, baada ya kukoboa kampuni ya *TCCCo Limited* ilitambulisha kimakosa kahawa ya Kikundi

cha *Kalinzi Organic* kuwa ni kahawa ya Kikundi cha *Kalinzi Coffee Farmers* kwa maana ya *(KACOFA)* na hivyo Bodi ya Kahawa Tanzania kukilipa fedha za mauzo ya kahawa kikundi cha *KACOFA* badala ya Kikundi cha *Kalinzi Organic.*

Mheshimiwa Spika, baada ya kugundulika mkanganyiko huo, taratibu za usuluhishi zilifanyika na maamuzi yalitolewa ambapo kikundi cha *KACOFA* kilikubali kurejesha fedha hizo kwa Kikundi cha *Kalinzi Organic* kupitia mauzo ya kahawa yao ya msimu ule wa 2012/2013. Hata hivyo, katika msimu wa 2012/2013 na 2013/2014 Kikundi cha *KACOFA* hakikupeleka kahawa ya kuuza kwenye soko la mnada hivyo fedha hizo hazikuweza kurejeshwa kwa Kikundi cha *Kalinzi Organic* kama ilivyoamuliwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya mashauriano kati ya uongozi wa kiwanda, Bodi ya Kahawa, Wizara ya Kilimo na viongozi wa Mikoa ya Kilimanjaro na Kigoma iliamuliwa kuwa suala hilo liwasilishwe kwenye vyombo vya usalama kwa ajili ya uchunguzi.

Mheshimiwa Spika, upelelezi wa suala hilo umekamilika na jalada la shauri hilo lipo kwa Mwanasheria wa Serikali ili atoe uamuzi na mapendekezo ya hatua za kuchukua kwa kikundi cha *KACOFA*. Aidha, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba haki ya Kikundi cha *Kalinzi Organic* itapatikana.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Obama Ntabaliba, nilikuona.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza naomba nimpongeze Naibu Waziri wa Kilimo kwa majibu mazuri na kihakika kama Wizara wanaonesha wanalitambua suala hili vizuri. Kwa hilo, nawapongeza sana kwa majibu haya.

Mheshimiwa Spika, kuanzia 2011 - 2018 ni miaka saba sasa, hawa wakulima 435 wanaodai zaidi ya milioni 150 au

Dola 74,000 bado wanadai. Kwa kuwa Bodi ya Kahawa ilifanya makosa kumlipa mtu mwingine na Mheshimiwa Waziri amekiri kwenye majibu yako kwamba iko kwa Mwanasheria, wakulima hawa wanataabika na hii ni Serikali ya wakulima, ni lini fedha hizo zitapatikana na Mwanasheria ataweza kuliharakisha suala hili?

Mheshimiwa Spika, la pili kwa kuwa hii inatokana na matatizo ya soko hili la kahawa, ni mkakati gani uliopo wa bei na masoko ya kahawa kwa wakulima wetu? Wananchi wanataka kusikia. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nichukue fursa hii nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi ambavyo amekuwa akifuatilia sana suala zima la zao hili la kahawa katika jimbo lake. Kwenye maswali yake madogo mawili ya nyongeza, mimi nimejibu kwenye majibu yangu ya msingi kwamba hili suala liko Mahakamani na jambo linapokuwa Mahakamani, sisi kama Serikali tunaviachia vyombo vya sheria viweze kuchukua mkondo wake na ukizingatia pia Mwanasheria Mkuu ndiyo *in charge* katika suala zima hili.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili la nyongeza, ni kwamba, kama Serikali hata zao la kahawa tumejipanga na tumesema tunafufua, tunaimarisha Vyama vya Ushirika kuhakikisha kwamba wakulima wetu wa Kitanzania hawaonewi na wanakuwa na *strong bargaining power* kupitia Vyama vya Ushirika ili bei zao ziwe nzuri na mazao yaweze kuwa bora. Nashukuru.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Bulembo na Mheshimiwa Peter Serukamba.

**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kutokana na swali la msingi, naomba kuuliza Wizara ya Kilimo hapo. Kwa kuwa wakulima wa kahawa ni

sawasawa na wakulima wa pamba. Wakulima wa pamba wamewaruhusu waliofanya biashara ya mkataba waweze kuendelea na shughuli hiyo, lakini wakulima wa kahawa katika nchi wa mkataba hawazidi watano mpaka sita. Kwa nini Wizara inakuwa *double standard,* msimu umeanza sasa hivi wiki ya pili watu hawa hawataki kuwapa kibali cha kuweza kukusanya kahawa kwa sababu ni biashara yao. Naomba tujue hawa haki yao wanaipata wapi?

**SPIKA:** Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Dkt. Tizeba, majibu tafadhali.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, utaratibu tuliouweka sasa hivi lengo lake la kwanza ni kuhakikisha kwamba wakulima wanapata malipo stahiki kwa jasho lao. Mfumo tuliokuwa nao sasa hivi kwa kiwango kikubwa ulikuwa hautoi malipo stahiki kwa jasho la wakulima na moja ya njia zilizotumika kuwanyima haki wakulima ilikuwa ni mfumo wa kununua kahawa kwa kulipa *advance* kutoka kwa wafanyabiashara na hasa katika Mkoa ambako Mheshimiwa Bulembo anatoka maarufu kwa jina la Butura. Ili kukabiliana na Butura, lazima kuweka mfumo unaofafana maeneo yote.

Mheshimiwa Spika, jana nilisema hapa ndani wakati nachangia hoja ya Bajeti Kuu ya Serikali kwamba pale ambapo mikataba hiyo iliingiwa *officially* kwamba kuna mkataba na mamlaka za Serikali zinatambua mikataba hiyo kama ilivyo kwenye pamba, pamba mtu haingii mkataba mtu na mtu mmoja, mikataba hiyo inaingiwa kupitia mamlaka za Serikali, kama wako wakulima wa kahawa ambao wameingia mikataba kwa njia hiyo, nilielekeza kwamba wapeleke habari hiyo haraka Bodi ya Kahawa ili waweze kupata utaratibu wa kuuza kahawa kwa mtu waliyeingia naye mkataba.

Mheshimiwa Spika, ile mikataba ya kuingia kienyeji ndiyo utaratibu uliokuwa unasababisha watu kupoteza haki yao na jasho lao kwa kuuza kwa watu ambao wanawapa malipo kidogo kwa kahawa ya bei kubwa.

**SPIKA:** Nilikutaja Mheshimiwa Peter Serukamba atafuatia Mheshimiwa Innocent Bilakwate.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwanza *KACOFA* iko kwenye Kata yangu, *Organic* iko Kalinze ambako ni Kata yangu. Kwa masikitiko makubwa Waziri anasema kesi iko Mahakamani, si kweli hakuna kesi Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, kilichotokea, *KACOFA* walipeleka Kahawa na hawa *Organic-Kalinze* walipeleka Kahawa. Kile kiwanda kilipouza Kahawa ile kikawalipa *KACOFA*, hakikuwalipa *Kalinze Organic. Kalinze Organic* walipoanza kufuatilia pesa zao wamefanya usuluhishi Wizarani na Bodi ya Kahawa mwisho wake Kiwanda kikasema kitawalipa, naomba nitoe maelezo haya; kitawalipa *Organic* taratibu.

Mheshimiwa Spika, toka mwaka 2011 kiwanda kile ambacho kilikubali kuanza kuwalipa watu wa Kalinze *Organic,* kwamba tutawalipa taratibu mpaka leo hakijalipa. Waziri anakuja leo hapa anasema suala lipo kwa *Attorney General* wakati wameshakubaliana waanze kuwalipa taratibu.

Mheshimiwa Spika, swali langu; naomba Wizara isimamie watu wa *Kalinze Organic* waweze kulipwa fedha zao kwa sababu makosa haya yamefanywa na kiwanda kile cha Moshi.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo na ombi hili, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Dkt. Tizeba, tafadhali.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jinsi alivyojibu hili swali la msingi la Mheshimiwa Albert Obama. Jambo hili ni la siku nyingi na hatua za awali kama anavyozisema Mheshimiwa Serukamba ni kweli zilichukuliwa namna hiyo. Kosa lililofanyika ni ku-*identify* nani anatakiwa kulipwa baada ya yule kupeleka ile kahawa kule mnadani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Bodi ya Kahawa ilivyopokea yale malipo ikapeleka kwa mtu ambaye alitajwa na mtu aliyeleta kahawa kwamba ndiye *beneficiary* wa hiyo kahawa; kwa hivyo wakamlipa na wale watu wakapokea pesa isiyo yao na wakaitumia.

Mheshimiwa Spika, baadaye ilipoonekana kwamba wamepokea pesa isiyo yao na wametumia, kwanza wakatakiwa wasuluhishwe tu *amicably*, wakaitwa, wakakiri kwamba watalipa msimu utakaofuata, kwamba watakapouza kahawa msimu unaofuata watalipa hilo deni. Wale waliokuwa wanadai Mheshimiwa Serukamba wakakubaliana na hiyo *position,* kwamba watapewa pesa yao msimu utakaofuata.

Mheshimiwa Spika, msimu uliofuata wale mabwana wa *KACOFA* hawakupeleka kahawa, kwa hivyo sasa kukawa na *default* ya makubaliano hayo; na baada ya hapo ndipo taratibu zikaanza. Nikiri tu kwamba jambo hili lilienda polepole lakini sisi safari hii tulichokifanya tumelipeleka kwenye vyombo vya uchunguzi kwanza tujiridhishe kwa nini walitumia hela ambayo si yao *at a time* wakati ya kwao walishalipwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, humu ndani kuna jinai katikati ya hili jambo, kwamba mtu amekuta benki fedha ambayo si kwake lakini bila kuuliza benki hela hii imetoka wapi, ameitumia, Sheria za Fedha ziko wazi, umeona! Sasa katika hatua hiyo ndiyo Mwanasheria Mkuu wa Serikali atatushauri sasa hivi tuendelee na hatua gani.

Mheshimiwa Spika, kama atatushauri tuwapeleke Mahakamani ili wale viongozi wa ule Ushirika waweze kuchukuliwa hatua wachukuliwe hatua, kwa sababu *as we speak* hawa hela ya kuwalipa wale wenzao mara moja, kwamba tungewaambia leteni hizi pesa tuwalipe wale ambao wanastahiki ya kupata hizo pesa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent swali la mwisho kwenye eneo hili.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya swali la nyongeza. Sasa hivi ni kipindi cha msimu wa kahawa. Vyama vya Ushirika vimeshindwa kuwahudumia wananchi kupata maturubai ya kuvunia Kahawa na hii kahawa inaendelea kukaukia Mashambani, wananchi wamekosa msaada. Hata hivyo, hata wale ambao wamepata maturubai, maturubai haya hayana viwango yanachanika hovyo. Ni hatua zipi za dharura ambazo zitachukuliwa ili kunusuru zao hili na mkulima aweze kulifaidi? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, kwa kifupi tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tumekuwa na matatizo sana katika suala zima la Vyama vyetu vya Msingi na Vyama Vikuu vya Ushirika na ndiyo maana kama Serikali tunasema kwamba, tuko katika mikakati ya kuhakikisha tunafufua, tunaimarisha na kuboresha Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo kutokana na swali lake hili la msingi katika Jimbo lake la Kyerwa, kwamba mpaka sasa hivi kunasuasua, naomba nichukue fursa hii kuagiza Chama Kikuu cha Ushirika cha Kyerwa kuanzia leo wahakikishe kabisa kwamba, zoezi zima la mazao ya kahawa katika Jimbo la Kyerwa wanafanya kazi yao kwa ubunifu, wanafanya kazi yao kwa utii, wanafanyakazi yao kwa weledi, wanafanyakazi yao kwa uhakika.

Mheshimiwa Spika, lakini na mimi kama Naibu Waziri nikitoka hapa Bungeni ninaahidi kuwapigia Vyama Vikuu vya Ushirika vile *AMCOS* pale Kyerwa nikishirikiana na Mrajisi wangu kuhakikisha kwamba jambo hili halijirudii na linaweza kufanikiwa kwa uhakika.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nsanzugwanko nilikuona, swali la mwisho kabisa la nyongeza kwenye Wizara hii ya Kilimo.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru mimi nina swali dogo la nyongeza. Tarafa ya Herujuu huko Kasulu tunalima Kahawa nyingi na hasa Kata ya Herujuu, Kata ya Muhunga na Kata ya Muganza lakini eneo hilo halina Chama cha Ushirika na Chama cha Ushirika kiko Buhigwe kilometa 45. Ni kwa nini Mheshimiwa Waziri asitoe ruhusa sasa wakulima hawa wakauza kwa watu binafsi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, majibu tafadhali.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuwaruhusu kuuza kwa watu binafsi kwa sababu tutakuwa tume-*distort* mfumo tunaojaribu kuujenga. Tunajaribu kujenga mfumo hapa ambao tukiruhusu hicho anachokisema tutakuwa tumeuvuruga tena wenyewe wakati tunajaribu kutengeneza.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi Jimboni kwangu tunalima kahawa, lakini wale wakulima wa kwangu tumewaunganisha na vyama vingine ambavyo vina uwezo wa kufika sokoni na sisi tunaendelea tu kumshauri Mheshimiwa Nsanzugwanko kufanya namna hiyo. Jambo muhimu hapa ni kuangalia uwezekano wa wao wenyewe kuwa na *AMCOS* yao; na *AMCOS* zinaruhusiwa kufikisha Kahawa kwenye soko kule Moshi.

**SPIKA:** Ahsante sana, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Na. 494

### Mkanganyiko wa Watumishi wa Zimamoto Kwenye Viwanja vya Ndege

**MHE. LUCIA M. MLOWE (K.n.y. MARY D. MURO)** aliuliza:-

Kumekuwepo na mkanganyiko wa watumishi wa zimamoto kwenye viwanja vya ndege na viwanja hivyo kutokuwa huru katika kuwatumia kutokana na kuwa si sehemu ya waajiri wao:-

Je, nini kauli ya Serikali kuhakikisha viwanja vinajitegemea?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mary Deo Muro, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linasimamiwa na Sheria Namba 14, Sura ya 427 ya Mwaka 2007 iliyounganishwa Vikosi vya Zimamoto vilivyokuwa chini ya TAMISEMI na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuwa chini ya Kamandi moja ya Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji pamoja na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ni Taasisi za Serikali ambazo hufanya kazi kwa pamoja kwa lengo la kutoa huduma ya kulinda mipaka ya nchi, hivyo hakuna mkanganyiko wowote wa kiutendaji. Hata hivyo, naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa upo ushirikiano mzuri kati ya vyombo hivi vya ulinzi na usalama na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege katika kutekeleza majukumu yao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mlowe nimekuona.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali ya nyongeza. Pamoja na majibu ya Waziri naomba niulize kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; kwa kuwa watumishi wa Jeshi la Zimamoto wanafanya kazi katika mazingira magumu na mazingira hatarishi, lakini hawana vifaa vya kufanyia kazi. Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha watumishi hawa anapata vitendea kazi nchi nzima?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa Mkoa wa Njombe hadi sasa Jeshi la Zimamoto hawana Ofisi, je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha inajenga Ofisi pale Njombe? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mhandisi Masauni kutoka kwa Mheshimiwa Lucia Mlowe.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tuna changamoto ya vifaa ama vitende kazi kwenye Jeshi la Zimamoto na tunafanya jitihada mbalimbali kukabiliana na changamoto hiyo. Moja katika jitihada ambazo tunafanya ni kutenga fedha kwenye bajeti yetu kila mwaka ili kuweza kununua vifaa zaidi ikiwemo magari na vitendea kazi vingine mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, vile vile tunajaribu kuimarisha mahusiano kati ya Jeshi la Zimamoto kupitia halmashauri pamoja na majiji mengine. Wakati huo huo tumekuwa tukibuni mikakati mbalimbali ikiwemo mikakati ya kuweza kuchukua *program* za mikopo ambazo sasa hivi tuna mchakato ambao unaendelea. Nisingependelea kuzungumza sasa hivi kwa sababu haujafikia katika hatua ya mwisho, lakini ni moja katika jitihada ambazo tunafanya kuhakikisha kwamba Jeshi la Zimamoto linapata vifaa.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la Njombe, ni changamoto ya Ofisi katika mikoa hii mipya. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunalifahamu hilo na tunalichukulia kwa uzito na pale ambapo hali ya kifedha itaruhusu tutakabiliana na changamoto ya Ofisi katika Mkoa wa Njombe na mikoa mingine hususani mikoa mipya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Julius Kalanga, nilishakuona.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nashukuru kwa kunipa nafasi. Tumekuwa na tatizo la kuungua

kwa majengo mbalimbali ya Serikali ikiwemo vyuo na shule za sekondari hata katika Halmashauri ya Wilaya ya Monduli. Je, nini mkakati wa kuhakikisha kwamba angalau kila halmashauri inapata gari moja la Zimamoto?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Spika, swali lake linafanana sana na swali ambalo limeulizwa kwenye swali la msingi ambalo nimeshalijibu. Kwa hivyo jibu lake linakuwa vile vile, kwamba, mikakati ni ile ile ambayo nimeizungumza kuhakikisha kwamba tuna dhamira hiyo hiyo ya kuona kwamba magari yanafika katika maeneo takribani yote. Ndiyo maana tumeanza jitihada sasa hivi za kutanua wigo wa kuweza kupeleka huduma ya Zimamoto katika Wilaya nyingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kila mwaka tumefanya jitihada hizo kwa kufungua Ofisi, kupeleka Maaskari wetu kuanza kutoa huduma za kutoa elimu ili pale ambapo magari yatakapokuwa yamepatikana na vifaa vingine tuweze kuvifikisha huko viweze kusaidia jitihada hizi ambazo tumeanza nazo kwa mafanikio makubwa.

**SPIKA:** Swali la mwisho kwa siku ya leo linaelekezwa kwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na linaulizwa na Mheshimiwa Flatei Gregory Massay.

Na. 495

**Kukosekana kwa Mawasiliano ya Mtandao wa Simu-Mbulu Vijijini**

**MHE. FLATEI G. MASSAY** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga minara ya Simu katika Kata za Yayeda, Ampa Arr, Tumati, Gidilim Gorati, Endaagichan na Haydere katika Jimbo la Mbulu Vijijini ili wananchi waweze kuwasiliana?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ATASHASTA J. NDITIYE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* iliyaainisha maeneo mbalimbali ya Jimbo la Mbulu vijijini yakiwemo maeneo ya Yaeda, Tumati, Gidilim Gorati, Masieda, Endaagichan, na Hyadere na kuyaingiza katika zabuni ya awamu ya tatu iliyotangazwa tarehe 5 Juni, 2018. Zabuni hii inategemewa kufunguliwa tarehe 23 Julai, 2018. Endapo mzabuni atapatikana, mkataba kwa ajili ya kazi husika unatarajiwa kusainiwa tarehe 29 Agosti, 2018 na ujenzi wa minara unatarajiwa kuchukua miezi tisa tangu kusainiwa kwa mkataba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Massay, swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa katika majibu yake Mheshimiwa Naibu Waziri amesema mkataba ukisainiwa utachukua miezi sita mpaka mnara ujengwe. Nina minara mitatu ambayo kimsingi imejengwa miaka miwili mpaka sasa haijamalizika, kwa mfano; mnara wa *Airtel* ambao uko Maga, mnara wa *Halotel* ambao upo Gidilim na mnara wa *Halotel* mwingine ambao upo Tumati haujakamilika. Je, Mheshimiwa Waziri atasaidiaje minara hii ikamilike kwa sababu Serikali imeweka fedha nyingi ili wananchi wa Mbulu vijijini wapate mawasiliano?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa vijiji ni vingi ambavyo havina mawasiliano, Mheshimiwa Waziri yuko

tayari sasa kuja kuonja *taste* ya kukaa nje ya mawasiliano? Kwa mfano; Getereri, Mewadan, Migo, Harbaghe, Endadug, Eshkesh, Endamasaak, Gorad na Endamilai, yuko tayari sasa kuja ili uone hali ya mawasiliano ilivyo vibaya Mbulu Vijijini ili akatupangia vijiji hivi kupata minara?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Injinia Atashasta Nditiye, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ATASHASTA J. NDITIYE) :** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna minara mitatu ambayo imefungwa muda mrefu na mpaka sasa haifanyi kazi ipasavyo. Kuna mnara wa Maga ambao ulijengwa na *Airtel,* kuna matatizo yaliyotokea kati ya wakandarasi na jamii inayozunguka eneo hilo iliyosababisha mpaka sasa hivi mgogoro ambao unaendelea kutatuliwa kwa ngazi ya kata.

Mheshimiwa Spika, nahakikisha kwamba naendelea kuwafuatilia hawa watu wa *Airtel* kwa sababu wao waliingia mkataba na *UCSAF* kwa ajili ya kupeleka mawasiliano. Masuala ya mgogoro kati ya *Airtel* na Kata yanatakiwa yatatuliwe miongoni mwao lakini mawasiliano ya wananchi wa maeneo ya Maga yapatikane.

Mheshimiwa Spika, vilevile eneo la Gidilim ambako *Halotel* wamejenga mnara kuna kama miaka miwili haujaanza kufanya kazi kutoka na Mkandarasi kutopata vifaa vya kutosha kupeleka maeneo hayo. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunafuatilia yote hayo pamoja na Yaeda, Ampa ambako *Halotel* vile vile wamefunga ili kuhakikisha kwamba hiyo minara inaanza kufanyakazi kwa haraka sana.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, ni kuhusu kuambatana na yeye kuona maeneo hayo aliyoyataja. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Massay, kwa kweli anafanya kazi kwa bidii sana. Muda mwingi sana huwa tunawasiliana kuhusu masuala ya

mawasiliano; na mimi kama mwenye dhamana ya mawasiliano namhakikishia kwamba Serikali tunajua umuhimu wa kuwa na mawasiliano kwa wote kwa sababu mpaka sasa hivi tuna asilimia 94 ya Watanzania wanawasiliana. Hatutaki wabaki hata kidogo inapofika mwisho wa mwaka huu, tunataka Watanzania wote wawe wanawasiliana. Ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa mtaona muda hauko upande wetu, nawaombeni tuendelee na mambo mengine yaliyo katika meza na kama mnavyojua leo mambo ni mengi sana na leo ni siku maalum.

Nitaanza na matangazo ya wageni, na tunao wageni wengi; Waheshimiwa Wabunge naomba tusikilizane kidogo:-

Mgeni wangu wa kwanza ni mtu ambaye ningependa kumtambulisha kipekee kabisa Waheshimiwa Wabunge. Mtakumbukwa kwamba mwezi uliopita mwezi Mei, hebu naomba tusikilizane, tusikilizane wale wote mnaongea ongea. Please hasa huu upande wangu huu una shida huu, *Chief Whip* watu wako huku uwe unaangalia wanapiga sana kelele hawa.

Mwezi uliopita palikuwa na Harusi ambayo ilivuta hisia za Watanzania wengi, nafikiri wengi mliona kwenye vyombo vya habari ambapo bibi harusi alikuwa amembeba bwana harusi ambaye ni mlemavu. Sasa maharusi hawa ni wageni wangu leo na ninao hapa Bungeni lakini pia ni wageni wa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, Mbunge wa Liwale, na ninao katika jukwaa pale ni Ndugu yetu Jivunie Mbunda na mkewe. Naomba msimame hapo mlipo. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA**: Mheshimiwa Spika, ambebe tuone

**SPIKA**: ...na Jivunie, mama hebu mbebe mzee hapo, asante sana, asante sana, sana. *(Makofi/Kicheko/Vigelegele)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA**: *Baby! Baby!*

**SPIKA**: Ahsante sana, ahsante sana mnaweza kukaa sasa. Ni upendo ulioje, hebu tuwapigie makofi mengine maharusi hawa. *(Makofi/Vigelegele)*

Bwana Mbunda na mama kabla hamjaondoka baadaye kwenye saa saba nawaalika muonane na Mheshimiwa Spika kidogo, tunong'one kidogo; ahsante sana; huo ndio upendo halisi kabisa kabisa.

Waheshimiwa tuendelee kusikilizana; wageni wengine tulionao katika majukwaa yetu ni wageni wa Mheshimiwa Januari Makamba Waziri wa Nchi, ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Jimbo la Bumbuli Wilaya ya Lushoto Mkoani Tanga. *UDOM* wale wageni wa Mheshimiwa Makamba, wale pale karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Japhet Hasunga, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, ambaye ni mwimbaji wa nyimbo za injili kutoka Dar es Salaam, Ndugu Catherine Madi Lukindo, Catherine Lukindo, karibu sana Catherine. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa John Kadutu ambaye ni mwandishi wa Jembe FM kutoka Jijini Mwanza ndugu Juma Ayo, yule pale, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Allan Kiula ambao ni Madiwani wa CCM kutoka Mkalama Mkoani Singida, karibuni Waheshimiwa Madiwani. *(Makofi)*

Wageni 13 wa Mheshimiwa Philip Mulugo ambao ni Kamati ya Siasa ya CCM kutoka Wilaya ya Songwe, Kamati ya Siasa Songwe, wale pale, karibuni sana na mkihitaji kufanya kikao cha Kamati ya siasa ya Songwe leo niambieni niwape ukumbi. *(Makofi)*

Wageni 40 wa Mheshimiwa Fatuma Hassan Toufiq ambao ni viongozi wa UWT kutoka kata za Dodoma Mjini.

UWT mmependeza kweli kweli, karibuni sana, karibuni sana, sana, sana. Jamani mnaona UWT hiyo, sasa hii BAWACHA mbona hatuonagi huku? *(Makofi)*

Wageni 46 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni watumishi wa Mungu kutoka Kanisa la Sayuni *Gateway Ministries* kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana wageni wetu, karibuni sana, sana, sana. *(Makofi)*

Hivi Umoja wa Wanawake wa *CUF* wanaitwaje? Wana umoja wa Wanawake wa CUF kweli? Sijawahi kusikia. *(Kicheko)*

Wageni 36 wa Mheshimiwa Bagwanji Meisuria na Mheshimiwa Kanali Mstaafu Masoud Khamis ambao ni vijana wa Kanisa la Kilutheri, Dayosisi ya Morogoro wakiongozwa na Mwenyekiti wao Inspekta Mwashibanda. Karibuni sana, sana, sana, karibuni sana wageni wa Bagwanji, Baniani pekee humu ndani. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Balozi Adadi Rajabu ambao ni wapiga kura wake kutoka Muheza, karibuni sana wale pale. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Khatib Saidi Haji ambao ni ndugu yake kutoka Zanzibar Mjini, ndugu Omari Ally Hassan, karibu. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Joram Ismail Hongoli ambao ni wadau wa habari kutoka Mkoani Njombe. Karibuni popote pale mlipo, wale pale. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua ambaye ni mpiga kula wake kutoka Masasi, Ndugu Ahmad Said Masenga, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Josephine Chagula ambao ni watoto wake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Kwa mara nyingi huku kulia kwangu kelele zimezidi sana, *Chief Whip* watu wako bwana.

Mgeni wa Mheshimiwa Boniphance Mwita ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Hunyari kutoka Bunda, Ndugu Musa Iramba karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Martin Msuha ambao ni viongozi wa CCM Kata ya Msigani karibu. *(Makofi)*

Wageni 24 wa Mheshimiwa Mary Chatanda ambao ni wanafunzi wa chuo kikuu cha Dodoma, wanaotokea Korogwe Tanga. Wako wapi wageni wa Mheshimiwa Chatanda? Karibuni sana popote pale mlipo. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Justine Monko ambao ni marafiki zake wa maendeleo kutoka nchini Marekani wakiongozwa na Mkuu wa Chuo cha Ufundi kwa Watu Wenye Ulemavu, Ndugu Fatuma Hussein Malenga. Karibuni sana, karibuni sana, karibuni sana wageni wetu kutoka Marekani. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Jumaa Aweso Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji ndugu Shaban Sufiani Mussa Mwenyekiti wa Kijiji cha Boza kilichopo Wilayani Pangani Mkoani Tanga, karibuni sana Mwenyekiti. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Mariam Ditopile ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Utekelezaji wa Umoja wa Vijana wa Mkoa wa Dodoma, karibuni sana, karibuni, wale pale. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Venance Mwamoto ambao ni Madaktari kutoka hospitali ya *Aga Khan* Jijini Dar es Salaam. Karibuni Madaktari kutoka *Aga Khan* popote pale mlipo. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Joshua Nassari ambao ni viongozi mbalimbali kutoka Jimbo la Arumeru, wale pale karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ambao ni familia yake na wapiga kura wake kutoka Liwale, karibuni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Alex Gashaza ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya siasa Mkoa wa Kagera ndugu Christopher Kilaja, karibu sana Christopher. *(Makofi)*

Wanafunzi thelathini na sita kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara (*CBE*) kutoka Jijini Dodoma, majirani zetu wa *CBE* wale pale karibuni sana, sana, sana, karibuni *CBE* mjifunze kuhusu namna Bunge linavyofanya kazi. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaendelea, matangazo mengine, Kamati ya Bajeti saa saba mchana katika ukumbi wenu wa kawaida mkutane ili muweze kukutana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango na Naibu wake ili muweze kuzungumzia mambo yanayohusu Muswada wa Sheria ya Fedha ili muweze kukamilisha uandikaji wa maoni yenu mapema. Saa saba Kamati ya Bajeti mkutane katika uwanja wenu wa kawaida na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Naibu wake watakuja huko pamoja na watalaam wao.

Tangazo kwa Waheshimiwa wote wa Imani ya Kikristo, mnatangaziwa na Mheshimiwa Anna Lupembe Mwenyekiti wa ibada kwamba, leo kutakuwa na ibada na Mtumishi wa Mungu Bishop Oscar Ongere kutoka Sayuni *Gateway Ministries* atahudumu katika ibada hiyo. Pia leo kutakuwa na kwaya ya Mtakatifu Andrea kutoka Msalato. Kama mnakumbuka ile kwaya ya Mtakatifu Andrea ni moja ya kwaya *top* kabisa hapa katika Jiji la Dodoma.

Sasa Waheshimiwa Wabunge nina matangazo kadhaa, ambayo naomba tusikilizane vizuri, mengine ni marefu kidogo. Kabla sijayatangaza haya, Mheshimiwa Juma Nkamia jana alikuwa ameuliza swali ambalo baada ya kulipima nikaona kwamba, basi niruhusu Serikali iweze kutoa maelezo yake kwa ufupi kuhusiana na suala ambalo Mheshimiwa Nkamia aliliuliza, kwa sababu linahusiana na

mambo ambayo yanaweza yakatoa picha isiyo kuwa nzuri ya nchi yetu. Kwa hiyo nikaona ni vizuri basi tuwape nafasi Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kama wana maelezo kidogo kuhusiana na mwongozo alioomba Mheshimiwa Juma Nkamia.

Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, karibu tafadhali.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nasimama kutoa maelezo mafupi kwa jambo lililojitokeza kufuatia mwongozo wa Mheshimiwa Juma Nkamia ambalo lilikuwa linahusu kuamuliwa kwa Mashehe kuondoka waliokuwa wamepewa mwaliko kuendelea na shughuli hapa.

Mheshimiwa Spika, kwanza hakukuwepo na jambo baya la kusema kwamba kuna kushukiana ama vinginevyo, lilikuwa jambo tu la kiutaratibu ambapo kila nchi huwa ina taratibu za masuala ya kiuhamiaji. Kwenye masuala ya kiuhamiaji kuna nchi ambazo wageni wake wanapokuja Tanzania hupata *VISA* wanapofika uwanja wa ndege na kuna nchi ambazo huwa wanatakiwa wageni waombe *VISA* wangali bado wako katika nchi zao.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo ulitokea tu mkanganyiko unaohusiana na utaratibu ambazo zinahusu masuala ya kiuhamiaji, lakini pia na masuala mengine ya kimawasiliano ya ndani ya nchi ambayo yanahusiana na taasisi zinazosimamia mihimili ya kiimani katika dini husika pamoja na Idara yetu ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kabla ya jambo hili kuwa limeletwa kupitia mwongozo, Serikali tulishapata malalamiko hayo na kwa kuepusha migongano inayoweza kujitokeza tayari Wizara nilishaelekeza kwamba, warekebishe kasoro zilizojitokeza kwa taasisi hiyo iliyokuwa imepata wageni kuwasiliana na taasisi nyingine husika na kuleta kumbukumbu zilizo sahihi katika Idara yetu ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, kabla ya hapo tayari nilikuwa nimeelekeza kuwa Mashehe hao waendelee na shughuli zao ambazo waliitiwa na huku viongozi wa taasisi hiyo wakiendelea kuwasiliana na BAKWATA pamoja na Uhamiaji kuweza kuweka kumbukumbu sawa hizo za kiutaratibu ili hao watu waweze kufanya shughuli zao bila kubughudhiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naliarifu Bunge lako Tukufu pamoja na Waislam wote kwamba, jambo hilo tulilimaliza na tulielekeza Mashehe hao waendelee na kazi na tena hata wasibughudhiwe wafanye kazi kama ambavyo walikusudia.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba Serikali hii ya CCM inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli inaheshimu uhuru wa kuabudu wa wananchi wake na inaheshimu Katiba inayotoa uhuru huo wa kuabudu kwa wananchi wote na jambo hilo tutaendelea kuliheshimu.

Mheshimiwa Spika, napenda tu nizikumbushie taasisi zote zinazoalika wageni kuzingatia taratibu hizo za ualikaji wa wageni na taratibu na taratibu za kiuhamiaji ambazo ziko kikatiba na kisheria kwa nchi ambazo wanahitaji kupata *Visa* kabla hawajaja na vile ambazo wanahitaji kupata *Visa* wanapofika uwanja wa ndege ili kuepusha migongano ambayo inaweza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, labda tu kwa niaba ya Mheshimiwa Mkuchika, uliuliza Yanga wako wapi? Nikwambie tu hawako ligi za mchangani kwa sababu ni timu pekee iliyosalia kwenye timu nane bora zinazocheza mashindano ya kimataifa. Kwa jinsi Yanga wanavyojiandaa msimu ujao timu zingine zitapata tabu sana, tabu sana ikiwepo timu yako pendwa. (*Makofi*)

**SPIKA:** Wanapata taabu kujieleza wako wapi, huu mwaka hatari kubwa. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba nitoe uamuzi kuhusiana na mwongozo ulioombwa Bungeni juu ya Wimbo wa Taifa, Nembo ya Taifa na alama nyingine muhimu za Taifa.

Waheshimiwa Wabunge, mnamo tarehe 3 Aprili, 2018 Mheshimiwa Sixtus Mapunda aliomba mwongozo kuhusu dosari za maneno na melodia katika wimbo wa Taifa, unaopigwa na kuimbwa hapa Bungeni tunapoanza Bunge na tunapofunga Bunge. Halikadhalika tarehe 6 Aprili, 2018 Mheshimiwa Goodluck Mlinga aliomba mwongozo akiomba alama zinazotumika kwenye Nembo ya Taifa zirekebishwe kwani haziakisi mazingira ya Tanzania.

Waheshimiwa Wabunge niliipa kazi Sekretarieti yangu ya Bunge kufanya utafiti wa kina kuhusu hoja hizo na kubaini kuwepo kwa dosari ndogondogo za baadhi ya maneno na muziki *(lyrics* na *rhythms)* katika uimbaji wa wimbo wa Taifa unaoimbwa hapa Bungeni wakati wa kufungua na kufunga vikao kutokana na kukosekana kwa sheria mahususi ya kuongoza uimbaji na kusimamia wimbo huo kama ilivyo kwenye nchi nyingine. Mfano Kenya na Malaysia ambako zimewekwa maneno beti na *(melody) nota* za muziki kwenye sheria zao za Wimbo wa Taifa.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge alama muhimu za nchi yetu kufuatana na mwongozo wa Mheshimiwa Mlinga, alama muhimu za nchi yetu zinapaswa kulindwa kikamilifu. Naishauri Serikali iunde timu, ni ushauri tu, iunde timu maalum ya wadau mfano Wizara ya Habari, Wizara ya Elimu, Vyuo Vikuu, Sanaa, Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, *BASATA*, Majeshi, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka na kadhalika ili ikusanye taarifa kuhusu Wimbo wa Taifa na alama nyingine muhimu za Taifa kama vile ngao, bendera na muhuri wa Taifa ili kubaini dosari za kimatumizi na kutoa mapendekezo ya kurekebisha hali hiyo endapo kuna umuhimu wa kufanya hivyo.

Waheshimiwa Wabunge nawashukuru sana, Mheshimiwa Sixtus Mapunda na Mheshimiwa Goodluck

Mlinga kwa hoja zao ambazo ni uthibitisho wa uzalendo wa Bunge hili katika kulinda na kudumisha historia, utamaduni na utambulisho wa Taifa letu.

Vile vile naishukuru Sekretarieti ya Bunge kwa utafiti na uchambuzi iliyoufanya. Naishukuru pia Wizara, Taasisi, Idara na ofisi zote za Serikali kwa utafiti wao na maoni waliyotupatia hususan Profesa Boniventura Silivant Rutinwa Makamu wa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na wengine wote waliotuletea maoni na michango yao juu ya suala hili. *(Makofi)*

Kwa wale ambao hamkuwepo siku hiyo, Mheshimiwa Mlinga alikuwa na maoni kwamba, Nembo yetu ya Taifa kama mnavyoiona pale juu, wale Bibi na Bwana kama walikuwepo miaka ya 60 sasa leo watu wamebadilika kidogo. Alikuwa na maoni kwamba wangependeza zaidi kuliko walivyo, maana huyu bwana amepiga shuka tu huku juu kote hana hata fulana. Pia huyu mama naye, je, hawezi kuboreshwa kidogo?

Kutokana na jambo hili, kama nilivyosema nitawasilisha Serikalini taarifa nzima hiyo ya utafiti na uchambuzi wa Wimbo wa Taifa na alama nyingine muhimu za Taifa ili zifanyiwe kazi kwa kadri itakavyoonekana inafaa hasa Wizarani kwa Mheshimiwa Waziri Mwakyembe

Waheshimiwa Wabunge ili kuboresha upigaji na uimbaji wa wimbo wa Taifa hapa ndani ya Bunge kwa mujibu wa kanuni ya 27(2) ya Kanuni za Bunge nimeona ipo haja ya kumuwezesha kila Mbunge kushiriki kikamilifu kwa nia ya kuamsha ari na uzalendo wa nchi yetu wakati wa kuuimba wimbo huo.

Kwa muktadha huo Waheshimiwa Wabunge kwa yale ambayo yanatakiwa kufanywa na Bunge letu, naagiza kwamba kuanzia sasa Wimbo wa Taifa utakaopigwa na kuimbwa Bungeni utaongozwa na *brass band* itakayotoka miongoni mwa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Kwa hiyo ili kutofanya makosa makosa sasa tutaleta *brass band* wakati wa kufungua na kufunga Bunge, maana ule wimbo uliokuwa unaimbwa ulikuwa kidogo una kasoro kadhaa.

Waheshimiwa Wabunge ratiba yetu ya leo ni nzito na ngumu, lakini niwaambie tu kwamba kuanzia muda mfupi baada ya matangazo haya tutaendelea na Waheshimiwa Mawaziri kujibu baadhi ya hoja na tutaanza na Mheshimiwa Angela Kairuki na wengine watafuata, Mheshimiwa Mpina na wengine watafuata dakika 10.

Waheshimiwa Wabunge, kuanzia saa 11.00 jioni nitaomba kila mmoja wenu awepo hapa. Saa 11.00 juu ya alama kila mtu awe ndani kwa sababu ndipo tutaanza suala la kura ya uamuzi wa bajeti. Baada ya hapo tutakuwa na Muswada wa *Appropriation* kwa hatua zote na kura hii ni muhimu sana. *(Makofi)*

Sasa Waheshimiwa Wabunge kuna baadhi ya Wabunge ambao huwa wanasumbuliwa na tofauti kati ya utaratibu wa kupitisha bajeti wa kupitisha bajeti ya Serikali ambao leo tunashughulika nao na Muswada wa Sheria ya Fedha *(Finance Bill)* ambao utashughulika kwa siku mbili kati ya kesho na kesho kutwa.

Mjadala kuhusu Bajeti ya Serikali utahitimishwa na Waziri wa Fedha na baada ya hapo Bunge litapiga kura ya wazi leo jioni kwa kuita jina la Mbunge mmoja mmoja ili kutoa uamuzi wa kupitisha au kutokupitisha bajeti hiyo. Hii ni kanuni ya 107. Bunge likikataa kupitisha bajeti mara moja Rais atalivunja Bunge, ibara ya 90(2)(b) ya Katiba. *(Makofi)*

Narudia tena, endapo mlio wengi mtaikataa Bajeti ya Serikali, Bunge hili litavunjwa mara moja na baadhi ya wengine hapa mkirudishwa jimboni hamrudi humu. Kwa hiyo akili ya kuambiwa changanya na ya kwako.

Baada ya zoezi hilo la kupitisha bajeti kwisha Muswada wa *Appropriation* utasomwa kwa hatua zake zote

mfululizo, yaani Kusomwa Mara ya Kwanza, Mara ya Pili na Mara ya Tatu; hapo mchakato wa kupitisha bajeti za Serikali Bungeni unakuwa umekamilika, Kanuni ya 108.

Sasa Muswada wa Sheria ya Fedha *(Finance Bill)* unaainisha na kuzipa nguvu za kisheria taratibu zote za ukusanyaji wa kodi na maduhuli ya Serikali, usimamizi wa fedha za umma na kwa ujumla utekelezaji wa taratibu zote za kibajeti kama zilivyoainishwa kwenye Bajeti ya Serikali na kupitishwa na Bunge. Huwasilishwa na kujadiliwa kama Miswada mingine yoyote ya Sheria.

Muswada huu ulishasomwa mwaka wa kwanza tarehe 18 juni 2018, tayari umechambuliwa na Kamati ya Bajeti na wanaendelea kumalizia na utawasilishwa Bungeni na Kusomwa Mara ya Pili kesho na taratibu zake zote zitafuata. Mjadala huwa ni wa siku mbili kama nilivyosema, Mheshimiwa Waziri atahitimisha siku ya pili, Kamati ya Bunge Zima itakaa na Wabunge watahojiwa kwa ujumla na kuamua.

Tofauti na Muswada wa *Appropriation* ni kwamba kwenye *Finance Bill,* Kamati ya Wabunge wanaruhusiwa kuwasilisha mapendekezo ya marekebisho *Schedule of Amendment* kwa mujibu wa Kanuni ya 86(1). Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge na wapiga kura wanaotusikiliza kwa leo jioni wakati wa kupiga kura Mbunge hapigi kura kwa jambo moja au mawili anapiga kura kwa Mfuko mzima wa Bajeti, begi zima. Kwa hiyo ni vizuri wananchi wakaelewa kwa sababu ni muhimu sana tukaelewana katika jambo hili.

Basi baada ya hayo ningeomba sasa tuendelee *unless* kuna jambo la muhimu sana ambalo haliwezi kusubiri, ndiyo Mheshimiwa ni moja tu ngoja kidogo, nawaomba kwa kifupi sana tuanze na Mheshimiwa.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nasimama kwa msaada wa

Kununi ya 68(7) kuhusu jambo ambalo limetokea hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, leo umepokea mgeni Bwana Harusi na Bi harusi wetu ambao wametutembelea hapa Bungeni ni wana ndoa wa kihistoria. Kilichodhihirika ni kwamba mwanamke akiamua kuitengeneza nyumba yake kwa kweli hashindwi, kwa gharama yoyote ile ataweza kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wanaume wengine wote nimpongeze sana Bi harusi wetu kwa kufanikisha kuingia katika ndoa hii. Sasa umekuwa ni utaratibu wa Kitanzania pale ambapo watu wanataka kufunga ndoa kuwakaribisha wengine kwa ajili ya michango ili kufanikisha jambo hilo. Bi harusi na Bwana harusi hawakutupatia nafasi ya kufanya hivyo wakati wanakwenda katika maandalizi yao ya ndoa.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kuwa leo wameingia hapa Bungeni nilikuwa naomba mwongozo wako kwa nini katika posho zetu za leo Wabunge tusikatwe angalau Sh.20,000 ili iwe mchango katika kufanikisha ndoa hii ili na wao sasa waweze hata wakaanzie maisha kama pongezi yetu kwenye jambo hilo, naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**SPIKA**: Toa hoja tuone kama inaungwa mkono.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa hoja.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, naafiki

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono naomba kuwahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja ilitolewa na Kuafikiwa)*

**SPIKA***:* Kwa kauli moja, maharusi mtachangiwa Sh.20,000 na kila Mbunge wa Bunge hili la Jamhuri ya

Muungano hongereni sana na karibuni Bungeni. Hiyo ni zawadi ya Bunge kwenu kwa kutambua jambo hili muhimu sana la upendo wa ajabu ambao hatujawahi kuuona, karibuni sana. Pia nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa takrima hii ambayo mmeifanya Mungu atawalipa, ahsanteni sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Tunaendelea Mheshimiwa Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kwa kanuni ya 68(7) kuhusu swali namba 488 linalohusiana na Wenyeviti wa Vijiji, Wenyeviti wa Vitongoji na Madiwani.

Mheshimiwa Spika, Wenyeviti ndio kiungo wakubwa wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa na ndio wanaofanya kazi kubwa ya kusimamia maendeleo katika vijiji vyetu. Sasa nashauri, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri Serikali ingewafikiria kuwalipa posho hawa Wenyeviti kwa sababu kazi wanayoifanya ni ngumu sana, pamoja na Madiwani.

Mheshimiwa Spika, Madiwani wanafanya kazi kubwa ya kusimamia miradi ya maendeleo si kama Madiwani wa zamani kama sisi hapana. Kwa hiyo nashauri Madiwani waongezwe posho na hao Wenyeviti wa Vitongoji na Wenyeviti wa Vijiji uangaliwe uwezekano wa kuwalipa posho kwa kila mwezi.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako.

**SPIKA**: Ahsante sana Mheshimiwa Lubeleje, mwongozo wangu kama Serikali imesikia na kwa kweli itazingatia maoni hayo kadri watakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Mbarouk kwa kifupi.

**MHE. MUSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nasimama kwa kanuni ya 68(7), kuomba Mwongozo wangu, lakini kwanza nikumbushe kitu. Tarehe 14 niliomba

mwongozo hapa baada ya Wizara ya Afya kupiga marufuku kununua na kuuza damu kwa wagonjwa, nikaambiwa mwongozo ule ungejibiwa Jumatatu itakayofuata ilikuwa ni siku ya Alhamisi, lakini mpaka leo sijajibiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini mwongozo wangu wa leo, Bunge letu hili ni Bunge la wananchi na inapotokea kuna jambo linalowasumbua wananchi tukilijadili humu ndani wakati mwingine tunaambiwa halijatokea mapema humu ndani. Sasa jana kama ulibahatika kuangalia vyombo vyetu vya habari, kuna zoezi la ukaguzi wa bima wa vyombo vya moto. Sasa kuna mkanganyiko kati ya *Agents* wanaokata bima na hizi mashine za ukaguzi za sasa hivi; hata kama ulikata bima siku za nyuma...

**SPIKA**: Mheshimiwa Mbarouk hilo ni katika ambalo halijatokea naomba umuone tu Mheshimiwa Waziri, halafu mkishindwana utatuletea,

Mheshimiwa Mtolea. Mheshimiwa Mtolea hakusimama nafikiri ni wewe Mheshimiwa, samahani.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, naitwa Frank George Mwakajoka. Nami naomba mwongozo wako. Kumekuwa na tatizo kubwa sana kwenye maeneo yetu hasa mkoa wa Songwe na Mbeya kwa polisi kuzunguka kwenye polisi na watu wa halmashauri na jiji kuzunguka katika nyumba za wageni usiku na kuanza kukagua vitabu vya wageni na baadaye kumekuwa na usumbufu mkubwa sana...

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Mwakajoka hilo limetokea lini hapa?

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, tulikuwa tunajadili hapa na Mheshimiwa hapa kwa hiyo tulikuwa tunajadili ndani ya Bunge humu, tulikuwa tunajadili na Mheshimiwa Mbilinyi, kwa hiyo inatokea humu ndani ya Bunge. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Selasini, tafadhali.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi. Mwongozo wangu nami ni kanuni ya 68(7) kuhusu jambo lilitokea hapa Bungeni leo asubuhi.

Mheshimiwa Spika, ulipompa Mheshimiwa Chegeni nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kutokana na swali namba 491 alisema kwamba Mheshimiwa Waziri wa Uvuvi amekuwa na tabia ya kusema kwamba yeye hana wapiga kura wa samaki.

Mheshimiwa Spika, wakati anatoa majibu yake hakuzungumzia hili kwa kukanusha au vyovyote vile na mimi naona hii ni tuhuma nzito angeweza akasema hapana labda watu walini-*quote* vibaya na nini. Kwa sababu humu ndani kumezuka sasa tabia ya kutuhumiana, hata jana Mheshimiwa Musukuma katika mchango wake alisema katika Mfuko wa Kuendeleza Zao la Korosho ana hakika kwamba kuna Wabunge wezi na mimi niliomba mwongozo ili walau ifutwe au wawaseme lakini alisisitiza.

Mheshimiwa Spika, sasa mambo kama haya yasiposemewa yakafutwa kwenye *hansard*, *hansard* inakuja kusomwa na watoto wetu na wajukuu wetu, itaonekana kwamba Bungeni palipita Wabunge ambao walikaa si kwa maslahi ya nchi, walikaa kwa maslahi yao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ningeomba mwongozo wako ili Mheshimiwa Waziri aweze kulikanusha hili au aweze kutoa maelezo na lile la jana kama linaweza likatolewa ufafanuzi sababu Mheshimiwa Musukuma alisema ana hakika ana majina ya Wabunge wezi wa Mfuko huo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Sijui kama kuna haja ya Mheshimiwa Waziri kusimama na kujibu hilo maana alipata nafasi ya kujibu ukiona amenyamaza ujue amepuuzia. Sidhani; kwa sababu sisi wote tuko hapa ndani ingekuwa aliyetajwa ni mtu

ambaye hayuko miongoni mwetu, hata Musukuma alivyosema angesema watu ambao hawako miongoni mwetu ingekuwa ni *issue* kwamba tunawalindaje. Sasa ukitajwa Selasini halafu ukanyamaza maana yake ni kwamba umechagua, umeona ni bora hilo kuliacha lilivyo, *unless* kama Mheshimiwa Waziri unataka kujibu, Mheshimiwa Waziri tafadhali Mheshimiwa Luhaga Mpina Waziri wa Mifugo na Uvuvi, tafadhali.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, maneno mengine ni ya kama ulivyosema, lakini niseme tu kwa sababu limeongelewa hapa. Maneno mengine ni uchonganishaji tu kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Waziri chini ya kiapo siwezi kuwabagua wananchi wangu katika kuwasimami hata siku moja na siwezi kutoa kauli kama hizo hata siku moja. Majukumu yangu ni kwa mujibu wa Katiba, kwa mujibu wa sheria zilizowekwa. Kwa hiyo, ninachotaka kusema tu ni kwamba katika ulinzi huu wa rasilimali zetu watuvumilie kwa baadhi ya watu ambao wakati mwingine hata wao wenyewe wanahusika na biashara hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile kumekuwa na mambo ambayo yanazungumzwa, Wabunge wengine wanazungumza humu gari langu mimi lilikamatwa lakini hata hawaku-*declare interest,* halafu wanapata *airtime* ya kumtukana Waziri wanavyoweza, hawana *right* hiyo. Mimi kama Waziri, Bunge linanielekeza kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa. Hakuna Mbunge ambaye ana uwezo wa kumtukana Mbunge mwenzake kwa kadri awezavyo. Kwa hiyo mimi nilitaka tu niseme hayo.

**SPIKA:** Ahsante sana, hayo ndio majibu Mheshimiwa Selasini. Tunaendelea na Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. MUSUKUMA J. KASHEKU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana; na mimi nasimama kwa Kanuni hiyo ya 68(7). Wakati nimeuliza swali langu namba 491, Mheshimiwa

Waziri amekiri kwamba Sheria ile ya Uvuvi, Namba 22 imejichanganya na atakamilisha marekebisho yake mwezi wa Saba lakini zoezi hili linaendelea na Wabunge wengi...

**MWENYEKITI:** Unazungumzia kanuni au sheria yenyewe?

**MHE. MUSUKUMA J. KASHEKU:** Mheshimiwa Spika, nazungumzia kanuni na Wabunge wengi wamekuwa wakilalamika kuhusiana na watu wao kuonewa kwenye majimbo na maeneo yao. Majibu mepesi sana ya Waziri anasema anasingiziwa na sasa hivi umemsikia anavyolezwa kwamba watu wanazungumza hawaja-*declare interest yaani* majibu mepesi.

Mheshimiwa Spika, kauli yako umezungumza vizuri sana kwamba naomba mniletee malalamiko. Sasa ni kazi kubwa sana kwa Mbunge na muda tuliona kwanza kuanza kushughulika na mmoja mmoja pengine kuwabeba kuwaleta Dodoma. Kwa nini kiti chako kisiunde Tume ikaenda kuzunguka kutafuta hayo matatizo wakakuletea hicho kitabu cha malalamiko, tukaondoa hii kauli na dharau ya Waziri ya kusema tunamsema kwa kumsema sijui kwa kuvunja Katiba si sahihi. Ni kwamba kweli watu wetu wameonewa na wapo na anawajua, hata kwa majina amepelekewa hajachukua *action.*

Mheshimiwa Spika, niombe sana kama kuna uwezekano uunde tume ikafanye hii kazi ili hii fitna ya kuzungumza ijiondoe. Nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri unataka kusema chochote, karibu tafadhali.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, sijasema kwamba sheria iliyotungwa na Bunge hili imejichanganya sijasema hivyo. Nilichokisema ni kwamba ni kawaida, sheria yetu hii tumeitunga mwaka 2003, leo ni miaka 15 sasa na mambo mengi yamebadilika ya kiuchumi na

maendeleo kwa hiyo tunachofanya ni kuiboresha ili iende na wakati sawasawa.

Mheshimiwa Spika, la pili, hakuna mwananchi yeyote ambaye ananyanyaswa wala kuonewa katika hatua ya operesheni zinazoendelea. Leo niseme kwamba Serikali ipo katika ngazi ya kitongoji, katika ngazi ya kijiji, katika ngazi ya kata, katika ngazi ya wilaya, tunazo Kamati za Ulinzi na Usalama katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wananchi wanapopata matatizo hayo hayawezi kutoka katika *level* ya kijiji, *level* ya kitongoji, *level* ya kata, *level* ya wilaya yakaja moja kwa moja kwa Waziri. Kwa hiyo ndiyo maana mimi nikawa nasema muda wote, kwamba kama kuna shida yoyote tutaishughulikia, iwe imewasilishwa na Mbunge moja kwa moja kuja kwa Waziri au imewasilishwa na Wenyeviti wetu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Spika, niseme na kusisitiza kwamba hakuna mwananchi yoyote ambaye anaonewa na Serikali kwa mujibu wa nanii; sisi tunapambana na uvuvi haramu tu ambao tumeapa lazima tuutokomeze. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Musukuma kwa sasa hivi kuunda tume kwa maana ya Bunge sidhani, nadhani ni mapema kidogo *unless* tupate ushauri mzito zaidi kutoka kwenu huko mbele tunakoenda, lakini kwa sasa nadhani hebu tujaribu kwenda hivyo tunavyoenda tuone; na kama nilivyosema kama kuna shida yoyote kubwa tuambiane na sisi tutawaambia Wizara na Serikali kwa ujumla. Nina hakika si nia ya Wizara wala ya Serikali kuona kwamba mtu yeyote asiyekuwa na hatia anapata matatizo katika nchi yetu.

Sheria hii tuliitunga baadhi yetu tulikuwepo 2003, Mwenyekiti wa Kamati alikuwa Mama Makinda na sisi tulikuwa wajumbe. Tuliichambua sana sheria ile, sasa kinaweza kikatupita kitu fulani lakini katika madhumuni na sababu haikuwa kwamba tuunde sheria itakayosababisha usumbufu mkubwa kwa watu, hapana.

Pia mkumbuke Waheshimiwa Wabunge, wewe mwenyewe kama Mbunge una uwezo wa kuleta marekebisho wa sheria, Kamati yenu mnaweza kuleta mapendekezo ya marekebisho ya sheria kama kuna sheria ina matatizo, Serikali ina uwezo wa kufanya hivyo. Kwa hiyo badala ya kulalamika kila siku, basi hebu angalieni nafasi ambazo zipo katika kanuni na muweze kuzitumia vizuri.

Mheshimiwa Mulugo.

**MHE. PHILIPO A. MLUGO:** Mheshimiwa Spika, mwongozo wangu na mimi ulikuwa ni 68(7) ambao tayari Mheshimiwa Mtolea ameutoa, ilikuwa ni juu ya wanandoa wetu wa leo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mtolea.

**SPIKA:** Ahsante sana. Wa mwisho ni Mheshimiwa Mkuchika.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nimesimama kwa kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nikupongeze kwa maelekezo yako uliyoyatoa leo asubuhi kuhusu uimbaji wetu wa Wimbo wa Taifa. Naomba mwongozo wako kuhusu jambo moja. Kila nchi ina mapokeo yake katika utamaduni. Kwa mfano, nchi nyingi ukienda hata Marekani na wapi wanapoimba Wimbo wa Taifa wanaweka mkono kifuani, ndiyo mapokeo ya nchi yao.

Mheshimiwa Spika, sisi Watanzania mapokeo yetu tuna simama *attention,* awe mwanafunzi wa shule ya msingi, awe mgambo, awe askari, awe Spika tunasimama *attention*. Humu ndani tumeanza kuwachanganya watoto wa shule, ambao hawajui wafuate lipi? Wafuate mtindo wa Marekani wa kuweka mkono kifuani, wasimame *attention* au wa-*relax* au waendelee kuongea?

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako.

**SPIKA:** Huo ni mtihani mkubwa sana kwa Mheshimiwa Spika, lakini kama ulivyoeleza Mheshimiwa Waziri kwa kweli mapokeo yetu sisi na wengi wenu mmepita JKT na mahali pengine ni kusimama *attention*. Sasa hii si sehemu ya mapokeo yetu na wanapenda sana upande huu kufanya hivyo.

*(Hapa Mheshimiwa Spika alionesha kwa vitendo jinsi baadhi ya Wabunge wanavyofanya wakati wa uimbaji wa wimbo wa Taifa)*

**SPIKA:** Kwa hiyo, turudi kwenye msingi jamani alikuwa anatukumbusha tu Mheshimiwa Waziri tuzingatie hilo. Katika masuala Wimbo wa Taifa ni jambo rasmi inatakiwa tufuate misingi ile inayoendana na jambo hilo tangu waasisi na tunakoelekea.

Basi sasa muda ulipofikia sasa ni kuanza kwa uchangiaji, Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU-KATIBU MEZANI**

**HOJA ZA SERIKALI.**

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2017 na Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019; na

Mapendekezo ya Serikali Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Majadiliano yanaendelea, Waheshimiwa Mawaziri kuna mwenye dakika kumi na wenye dakika tano kadri mlivyojipangia wenyewe. Nitaanza na Mheshimiwa Profesa Ndalichako dakika kumi atafuatiwa na Mheshimiwa Mwakyembe dakika tano.

Mheshimiwa Profesa tafadhali.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza katika siku ya leo. Napenda kuanza kwa kutoa pongezi za dhati kwa Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Mpango, pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Kijaji pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu Dkt James Doto.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa nimpongeze kaka yangu Dkt. Philip Mpango, kwa uwasilishaji wa umahiri kabisa wa bajeti hii, alitumia saa moja na dakika arobaini na tano lakini hatukuchoka. Tunampongeza sana na naunga mkono hoja hii kwa sababu bajeti hii imeandaliwa kwa lengo la kutatua kero za Watanzania.

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu nitapenda kuzungumzia masuala machache kwa sababu ya muda na ningeanza na suala ambalo wachangiaji wengi walikuwa wakilizungumzia kwamba Serikali haipeleki fedha kwamba tunakuwa tunapitisha hapa bajeti lakini mwisho wa siku Serikali haipeleki fedha. Pia wengine walienda mbali na wakawa wanasema kwamba hii Serikali inaleta bajeti hewa.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Joseph Pombe Magufuli ambaye kwa kweli ni Raisi shupavu, ni Rais ambaye anafanya vitu kwa vitendo, akiahidi anatekeleza.

Mheshimiwa Spika, pongezi hizi nazitoa kwa sababu kwenye sekta ya elimu fedha zimekuwa zikija kama ambavyo zimepangwa. Wizara ya Elimu ilipangiwa jumla ya trilioni moja na bilioni mia tatu thelathini na sita na mpaka sasa Serikali imeshatoa trilioni moja na bilioni mia moja ishirini na tisa.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imekuwa ikitekeleza ahadi yake ya elimu bila malipo kila mwezi bila kukosa, fedha kwa ajili ya elimu bila malipo zimekuwa zikienda bilioni ishirini kwa wakati. Pia Serikali ilikuwa imetenga bilioni 427.54 kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu na mpaka sasa ninapozungumza tayari Serikali imekwisha pokea shilingi bilioni 427.44 sawa na asilimia mia moja ya fedha zote ambazo zilitengwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na upatikanaji huu wa fedha katika sekta ya elimu Serikali imeweza kufanya mambo mengi. Tumeweza kujenga madarasa kwa ajili ya kuongeza upatikanaji wa nafasi za elimu pamoja na kuboresha mazingira ya elimu ambapo jumla ya madarasa 1907 yamejengwa lakini na matundu ya vyoo elfu nne mia tano na moja.

Mheshimiwa Spika, na nichukue nafsi hii kuwapongeza kwa dhati, umoja wa Wanawake Wabunge kwa uchangishaji wa vyoo bora kwa mtoto wa kike ambao kwa kweli inaungana na juhudi za Serikali katika utoaji wa elimu bora tunashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, pia tumeweza kujenga mabweni 338, tumefanya ukarabati wa shule kongwe 45 na vilevile ukarabati wa vyoo vya walimu 17. Vile vile kutokana na upatikanaji wa fedha hizi Serikali imeweza kuendelea kuimarisha tafiti katika nchi hii. Serikali ilitoa shilingi bilioni 3.2 kwa ajili ya miradi nane ya tafiti na hii miradi imelenga katika kuimarisha viwanda pamoja na kilimo.

Mheshimiwa Spika, jana tulikuwa tunazungumzia masuala ya kilimo, tunajua kwamba kilimo ndio kinabeba Watanzania na kwa hiyo Serikali imetoa bilioni 3.2 ambazo ni kwa ajili ya miradi minane ya utafiti. Kwa mfano na taasisi inayoshughulika na magonjwa ya binadam, *(NIMR)* imepata fedha kwa ajili ya kutengeneza maabara kwa ajili ya dawa, pia Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi *(MUHAS)* kimepata fedha pia kwa ajili ya masuala ya dawa.

Mheshimiwa Spika, hatujasahau na hapa Mkoa wa Dodoma Makao Makuu tumetoa fedha kwa ajili ya kuimarisha utafiti wa zao la zabibu. Kwa hiyo tumetoa fedha kwenye hii Taasisi ya Utafiti wa Mifugo ya *TALIRI* kwa ajili ya kuzalisha mifugo.

Mheshimiwa Spika, vile vile tumetoa fedha kwa ajlili ya utafiti wa kuboresha mitambo ya kuzalisha mvinyo katika Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya Makutupora. Haya yote nayazungumza kwa uchache tu kuonesha kwamba Serikali ya Awamu ya Tano ni Serikali ambayo inatenda kwa vitendo na hii yote imetokana na bajeti ambayo imetengwa.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kwenye Taasisi za Elimu ya Juu, Serikali hii imefanya mambo makubwa sana kwenye hizi Taasisi za Elimu ya Juu. Ukienda Chuo Kikuu cha Dar es Salaam sasa hivi inajengwa maktaba ya kisasa na ya kipekee katika Bara la Afrika, ambayo itakuwa na uwezo wa kuweka wanafunzi 2,500 kwa wakati.

Mheshimiwa Spika,ile vile Tume ya Mionzi ya Taifa inajenga Maabara kwa ajili ya kupima mionzi na maabara hiyo ikikamilika kwa kweli itakuwa ni maabara ya kipekee katika Ukanda wa Afrika. Tayari vifaa kwa ajili ya maabara hizo vimekamilika. Nashukuru kwamba Serikali imeshatoa fedha ambazo zilikuwa zimetengwa kwa ajili ya hii Tume na zinaendelea kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, katika suala la kusema kwamba Serikali inatenga fedha haizitoi; kwa sababu ya muda siwezi kumaliza taasisi, lakini niseme kwamba ukienda Mzumbe, ukienda Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine, ukienda Mbeya Chuo cha Utafiti, ukienda Arusha *Technical* utakuta mambo mengi yanafanyika.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo lilikuwa linazungumziwa katika michango ni namna gani Serikali inaimarisha elimu ya ufundi. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kama ambavyo imeainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na ambao umekuwa

ukitekelezwa mwaka hadi mwaka, Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kuhakikisha kwamba inaongeza ujuzi kwa wananchi katika nyanja mbalimbali, maana kuna ujuzi wa chini, kuna ujuzi wa kati na ujuzi wa juu.

Mheshimiwa Spika, hivi tunavyoongea katika Chuo cha Ufundi Arusha Karakana zote zinabadilishiwa vifaa ili ziweze kutoa mafunzo ya kisasa. Kuna kontena kumi na sita ambazo zimefungwa, tayari vifaa vile vipo kwa ajili ya kufungwa, kwa hiyo Serikali inaendelea kuimarisha.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la Walimu, kwa sababu elimu si majengo tu, ni pamoja na Walimu. Serikali imekuwa ikiendelea kuimarisha utoaji wa mafunzo ya ualimu. Sasa hivi tunafanya upanuzi wa vyuo vyetu vya ualimu; ukienda kule Kitangali utakuta Chuo cha Ualimu cha kisasa kimejengwa, nenda Mkuguso, nenda Ndala, nenda Shinyanga utaona kazi nzuri ambayo inafanywa na Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Spika, Serikali hii ambayo Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli ni Rais ambaye anaangalia wanyonge hajasahau wanafunzi wenye mahitaji wenye mahitaji maalum. Kwa hiyo katika mambo ambayo tunafanya tumeendelea pia kuimarisha utoaji wa elimu kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maaalum.

Mheshimiwa Spika, hivi ninavyozungumza ujenzi wa shule maalum kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum inaendelea katika Chuo cha Ualimu Patandi. Sambamba na ujenzi huo lakini Serikali pia imepanga kununua vifaa kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum; na tayari tumeshatoa maelekezo kwamba katika shule zote katika miundombinu yote ya kielimu inayojengwa lazima tuzingatie mahitaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niseme tu kwamba niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuiunge mkono bajeti ya Serikali kwa sababu ni bajeti ambayo italeta maendeleo, ni bajeti ambayo inakwenda kutatua kero za wananchi na ni bajeti ambayo inatusaidia hata sisi

Waheshimiwa Wabunge kutekeleza ahadi ambazo tumezitoa kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nategemea kwamba jioni kama ulivyoelekeza Wabunge wote watajitokeza wapige Kura ya Ndiyo katika bajeti hii ili wanafunzi wa elimu ya juu waendelee kupata mikopo ambapo tunategemea kutoa mikopo kwa wanafunzi 123,000.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naunga mkono hoja, lakini kwa heshima kubwa nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote tupige Kura ya ndio. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Profesa Ndalichako. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe dakika tano na Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, dakika kumi.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Nianze kwa kuunga mkono hoja na vile vile kumpongeza Waziri wa Fedha na Naibu wake kwa kazi nzuri na yenye viwango. Katika dakika tano pengine nigusie suala moja tu, muda ukibaki nitaongelea suala la pili na pengine la tatu.

Mheshimiwa Spika, jana lilijitokeza suala la ukabila hapa, ambalo haliwezi likabaki kwenye *Hansard* bila ya ufafanuzi. Kwa bahati mbaya sana liliibuliwa na Mbunge ambaye namheshimu sana na ambaye mimi mwenyewe najivunia kwa kumwita mdogo wangu Mheshimiwa James Mbatia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Wabunge wenzangu hapa, pamoja na maudhi yote ambayo tunaweza kuyapata, maana sisi wote ni binaadam, tuna upungufu mwingi sana; sisi viongozi tusikubali kwa njia yoyote ile kuwa abiria kwenye basi la ukabila na basi la udini. Tukifanya hivyo, tutafuta kabisa mafanikio makubwa ambayo Taifa hili limepata

kupita Taifa lolote lile katika Bara la Afrika hasa katika kujenga umoja wa kitaifa na sisi kujisikia ni Watanzania na si ni wakabila.

Mheshimiwa Spika, ndugu yetu Mheshimiwa Selasini ni Mheshimiwa mmoja Mbunge na ambaye vile vile namheshimiwa sana; jana aliweza kutoa sababu kwa nini imekuwa hivyo, akagusia magazeti mawili, kwamba kuna magazeti mawili hapa, Tanzanite na *Jamvi* kwamba ndiyo sababu hasa nafikiri kwamba kuna ubaguzi wa Wachaga.

Mheshimiwa Spika, lakini haya magazeti yanaweza kushtakiwa tu na Sheria ya Huduma ya Habari kifungu cha 41, mtu akileta upuuzi upuuzi mpeleke Mahakamani. Sisi kama Wizara ya Habari tutakuwa mashahidi wenu tutafungiaje, kesho tutafungia mtasema tunaminya uhuru wa habari.

Mheshimiwa Spika, Wizara hatuwezi kufungia kitu ambacho hakiko *direct* katika kuvunja usalama wa nchi hii. Kama umetukanwa wewe nenda Mahakamani, kifungu cha 41 kinakuruhusu, lakini ukileta hapa kwa sababu umesema wewe ukaleta Wachaga wote wanabaguliwa ni maneno ambayo kwa kweli yanaturudisha nyuma sana Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme neno moja, hivi leo Mchaga ni nani katika Taifa leo la Watanzania? Yupi hapa anaweza akashika jiwe akamtupia, akatupa jiwe kwenye kabila lingine asimguse mkwewe au mjomba wake kule? Hili Taifa limebadilika sana; mimi niko kwenye hali ngumu hapa, mimi natoka Mbeya huko lakini siwezi kutupa jiwe kwa Mchaga, watoto wangu wenyewe ni Wachaga wana damu hiyo na ndiyo Tanzania nzima iko hivi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1961pengine tukumbushane kwa vijana wadogo wadogo hapa; tulipopata Uhuru, ulikuwa ni uhuru wa makabila haya zaidi ya 120 ambayo hawakuwahi kukaa na

kukubaliana kwamba sisi ni Taifa. Kwa hiyo kazi kubwa aliyokuwa nayo Baba wa Taifa ni kuunda *a Nation State*; ataiundaje?

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana Baba wa Taifa ilibidi afanye kazi kubwa ambayo viongozi wengine wote Afrika walidharau na ndiyo maana kwao bado ukabila ni mkubwa. Sisi hatuna ukabila hapa, yeyote yule anayepanda basi la ukabila hana safari ndefu huyo, atapotea, ndiyo maana kitu cha kwanza Mwalimu ikabidi tusitishe mamlaka ya Machifu katika Serikali, ilikuwa nzuri tu, ili tuunde *national state*.

Mheshimiwa Spika, pili lugha ya Kiswahili kuwa ndiyo lugha yetu ya Taifa; lakini tatu *education system* yetu. Unakumbuka na viongozi wengine hapa, unamaliza darasa la saba wewe unatoka Kyela sekondari utakwenda Bukoba, wa Bukoba atakwenda Nachingwea, wa Nachingwea ataenda Tanga, wa Tanga ataenda Kigoma.

Mheshimiwa Spika, tumejichanganya na tuna tafiti za kisosholojia hapa, watu wote waliopitia mfumo huo, asilimia zaidi ya 85 hawajaoa maeneo yao, wameoa maneo mengine; na ndilo Taifa alilokuwa anataka kuliunda Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana, nimeanza ndani ya Bunge hili tumeanza kupanda mabasi ya ukabila, mabasi ya udini. Kuna sentensi za udini na za ukabila, tuache kabisa sisi ni viongozi, hawa watoto, bahati mbaya nimepewa dakika tano, lakini ujumbe wangu ulikuwa ni kwamba jana nilishtushwa, nikasema haya yasiongelewe hapa, tusiongee kabisa, tumefika mbali, tumefanikiwa sana kama Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nakuhakikishia hili ni Taifa jipya, hapawezi kabisa kuwa na mtu akisema watu fulani tunabaguliwa, haiwezekani utambagua nani? Maana wote ni wale wale. Ahsante sana.

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mheshimiwa Mwakyembe, kwa kweli ujumbe ulioutoa ni muhimu kweli kweli na mimi nipigie mstari kama kiongozi katika Bunge hili.

Waheshimiwa Wabunge, hili jambo la ukabila si la kuliendekeza, kulisema hapa. Tunaweza tukasema tukidhania tunajenga lakini kumbe tunafanya makosa makubwa sana. Unaweza kujikuta wewe unayelalamika kuhusu jambo fulani ndiyo ipo huko Serikalini na kila mahali kuliko hata jamii nyingine ambazo hazisemi.

Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge, nawaomba tujiepushe sana na kama kuna shida kama hizo hebu tujaribu kunong’ona miongoni mwa viongozi ili tuone kama jambo hilo lipo, basi tulirekebishe taratibu bila kulimwaga kwenye jamii bila utaratibu. Kwa kweli wa kujifunza na kurudi nyuma katika mambo haya ni sisi wote kama jamii ya Watanzania, katika makundi yetu yote; yawe makundi ya kisiasa, yawe makundi ya kidini, yawe makundi ya kijamii, iwe ni timu za mipira, michezo na kadhalika tuendelee kuwa Watanzania wamoja namna hiyo.

Dalili za ukabila ni dalili mbaya sana na hatuwezi kufika popote kama tunachochea ukabila. Kwa sababu Mheshimiwa Selasini ndiye *Chief Whip* hapa nimwambie rafiki yangu katika watu ambao dada zao wameolewa kila mahali ni dada zako. Mna wajomba nchi nzima, wengi sana, dada zako ni *liberal* kweli kweli.

Kwa hiyo yaani nchi hii ni moja bwana huwezi kumpata huyo Mchaga utampa wapi? Ikija siasa hizo wajomba ni wengi mno kila mahali. Kwa hiyo tumechanganyika upendo ule tuliouona ndio upendo wa Watanzania yaani hivyo kabisa. Kwa hiyo sisi wanasiasa tusiwe ni chanzo cha kuparaganyisha nchi yetu katika mambo ya kikabila.

Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, atafuatiwa na Mheshimiwa Mkuchika, dakika tano

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Labda nianze kwanza kwa kumkumbusha Mheshimiwa Selasini, wale anaowasema wale ndiyo shemeji zake wakubwa maana dada zake wana rangi ambayo inavutia sana makabila ya wale anaowasema. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Selasini, hata Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla ni shemeji yako pia. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa hivyo hata nyumbani kwangu leo nimeondoka asubuhi nimewaaga wajomba zake. Kwa hivyo, haya mambo hayawezekani katika nchi yetu. Sisi ni wamoja na hata Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe ana wajomba zako wa kutosha, Mheshimiwa Mwigulu, Mheshimiwa Makamba *and the list goes on and on!* Huwezi kuzungumza ukabila Tanzania. Tuachane na haya mambo ya hovyo hovyo, hayatusaidii kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nianze kuchangia kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshiimwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa jinsi ambavyo anaendelea kutoa dira na mwelekeo wa Taifa letu katika kuboresha maisha ya Watanzania na kuleta ustawi wa Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nichangie hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Richard Phillip Mbogo kuhusiana na uvunaji wa mazao ya maliasili kutoonekana kuchangia kikamilifu katika pato la Taifa letu. Alipenda kujua sababu hasa ni nini?

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Misitu inachangia pato la Taifa kwa kiwnago cha asilimia 3.5 tu! Kinaonekana ni kiwango kidogo sana na hata sisi tunaosimamia sekta hii tunaona kwamba kiwango hiki ni kidogo, lakini kiukweli kiwango hiki hakipaswi kuonekana kidogo ila kinachosababisha kikubwa ni *formula* ya mfumo wa fedha kwa namna ambavyo mchango wa Sekta ya Misitu

unakokotolewa, lakini mchango wa Sekta ya Misitu na mazingira kwa ujumla ni mkubwa sana kwenye uchumi wa Taifa letu kuliko ambavyo inasemwa kwamba ni asilimia 3.5 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ku-*mention* mambo machache tu, Sekta ya Misitu inachangia kwenye upatikanaji wa maji, umeme na kwenye kilimo. Ukitaka kuitazama kwa upana wake utaona kwamba kama Watanzania zaidi ya asilimia 70 wanategemea kilimo kama shughuli yao ya msingi ya kiuchumi na kama kilimo kinategemea maji ya mvua na kama mvua zinatokana na uwepo wa misitu iliyohifadhiwa, maana yake kwa kiasi kikubwa sana uchumi wa Tanzania wa watu wetu walio wengi unategemea kwa kiasi kikubwa misitu ambayo inahifadhiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia, wanyama kuanzia ng'ombe au zaidi ya milioni 36 ambao Mheshimiwa Mpina kila siku hapa anajivunia nao wanategemea maji yanayotokana na uhifadhi wa vyanzo vya maji ambavyo ndiyo hiyo misitu inayohifadhiwa. Uzalishaji wa umeme, miradi ya umeme ambayo kila siku Mheshimiwa Dkt. Kalemani hapa anajivunia na Waheshimiwa Wabunge kila siku mnaomba umeme kwa ajili ya wannachi wetu. Ule umeme unaozalishwa kutokana na maji ukirudi kinyumenyume utakuja kugundua unatokana pia na uhifadhi wa misitu ambao tunaufanya katika Wizara yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, ukitaka kukokotoa vizuri ukaangalia hizo *factor* zote utaona wazi kabisa kwamba Sekta ya Misitu inachangia kwa kiasi kikubwa sana kwenye uchumi wa nchi yetu kuanzia kwenye kuzalisha umeme, kilimo, mifugo, samaki, uhifadhi wa wanyamapori kwa sababu kwenye hii misitu pia tunahifadhi wanyamapori. Sasa ni nani ambaye ana *formula* ya kiuchumi ya kuangalia umuhimu wa misitu katika uhifadhi wake wa bioanuai ambao unafanyika. Kwa kweli utaona ni kwa kiasi kidogo sana *formula* inayotumika na wenzetu wa Wizara ya Fedha kukokotoa umuhimu wa misitu inavyotumika.

Mheshimiwa Spika, pia misitu inatusaidia sana kuondoa madhara ambayo yangejitokeza kutokana na uwepo wa hewa ya ukaa. Kama tungekuwa hatuna misitu maana yake hewa ya ukaa ingeongezeka duniani na mazingira yangeharibika maradufu na maradufu. Kwa hivyo, kwa kuhifadhi misitu tunaweza kupunguza ongezeko la hewa ya ukaa angani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile kwenye misitu tunapata asali, uyoga, dawa na tunapata hewa ya *oxygen* ambayo sisi sote tunaivuta. Sidhani kama *formula* za kiuchumi zinaangalia hadi *oxygen* ambayo tunavuta kila siku ambayo inatokana na uwepo wa misitu ambayo inatusaidia ku-*control* hewa ya ukaa hapa duniani.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, kwa kweli mchango wa misitu katika uchumi na katika pato la Taifa hauwezi kuwa ni hiyo asilimia 3.5 tu ambayo inazungumzwa na wanatakwimu za kiuchumi. Sisi tunaamini ingepaswa kuwa kubwa zaidi ya hiyo lakini kwa sababu ya *formula* inayotumika mchango wake unaonekana kuwa ni huo wa asilimia 3.5 ya pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili nilipenda kuzungumzia ilitolewa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya ambaye alisema kwamba utumiaji wa mazao ya misitu nchini kwa kutengeneza samani badala ya kuagiza kutoka nje ya nchi ambapo tunapoteza chanzo cha mapato.

Mheshimiwa Spika, tunakubaliana na yeye, lakini bado sana teknolojia ya wazalishaji wetu hapa ndani imekuwa duni kwa kiasi kikubwa na mazao mengi yanayotokana na uvunaji wa misitu bado hayajatumika kikamilifu kwa matumizi mengine mbalimbali ikiwemo hiyo ya kutengeneza samani za maofisini na majumbani, lakini pia kutengeneza *briquette* kwa ajili ya mikaa na matumizi mengine mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali imekuwa ikitoa maagizo mbalimbali mara kadhaa kuhusu taasisi mbalimbali

za Serikali kuanza kutumia samani za hapa ndani na mfano mzuri ni kwenye Bunge lako ambapo tunatumia samani zinazotokana na mazao ya misitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia mwaka huu kadri ambavyo Ilani ya Uchaguzi inatuelekeza tutenge asilimia 10 ya mazao ya misitu kwa ajili ya viwanda vya ndani, tunafanya hivyo. Huu ni mwaka wa pili sasa tumekuwa tukifanya hivyo, tunatenga uzalishaji kwenye misitu kwa asilimia 10 kwa ajili ya viwanda hususan katiak mashamba yetu ya Longuza na mashamba ya Mtibwa.

Mheshimiwa Spika, hoja ya mwisho ambayo napenda kuchangia inatokana na mchango alioutoa Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe hapa Bungeni kuhusiana na kwamba *VAT* imepunguza kasi ya ukuaji wa Sekta ya Utalii hapa nchini. *Introduction* ya *VAT* inaweza ikasemwa kwamba imepunguza kasi ya ukuaji wa Sekta ya Utalii lakini sisi tunapenda kuona kwamba bado ni mapema mno kufanya tathmini ya aina yoyote ile kama *introduction* ya *VAT* imeathiri ukuaji wa sekta ama la!

Mheshimiwa Spika, hatupingi wala hatukubali, lakini tunaona tu kwamba muda wa kufanya tathmini bado hautoshi na sisi tunaona sababu za ku-*introduce VAT* kwenye Sekta ya Huduma za Utalii ilikuwa ni ya maana sana, kwamba sekta hii kwa muda mrefu imekuwa ikionekana kama vile ni sekta ipo na haizalishi sana kwa ajili ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, sasa, ili Watanzania wa kawaida waweze kufaidika na Sekta ya Utalii ni lazima Sekta ya Utalii itozwe kodi ili hizo kodi ziende kutumika kutekeleza miradi ya kijamii ambayo itawagusa wananchi wengi, hilo ni jambo la kwanza. Pia, ni lazima wananchi wawezeshwe kushiriki katika Sekta ya Utalii ili nao wapate kipato kutokana na sekta yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa bahati mbaya sana, sekta hii kwa miaka mingi imekuwa ikiwa *controlled* na wawekezaji kutoka nje ambapo mawakala wapo nje ya nchi

na baadhi ya mawakala wapo ndani. Malipo kwa kiasi kikubwa yamekuwa yakifanyika nje ya nchi na kwa hivyo hapa Tanzania tunakuwa hatupati chochote. Pia wafanyabiashara wa Tanzania walikuwa wachache kwa miaka mingi.

Mheshimiwa Spika, sasa tulichokifanya katika miaka hii ni kutanua wigo wa kuwavutia wawekezaji wa ndani nao washiriki kwenye biashara ya utalii ili pia tuweze kupata kodi. Pia tunapo-*introduce VAT* maana yake walau tunapunguza *economic leakage* ambayo ilikuwa inasababishwa kwa mapato ya utalii kubaki nje na kutokuingia hapa ndani kwa sababu tunachaji kwenye huduma ambazo ziko hapa ndani. Kwa kufanya hivyo, tunakuwa tuna uhakika sasa ule mchango mkubwa ambao unaonekana kwa sekta pana ya utalii wa asilimia 17.6 kuwa na faida kwa wananchi wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja na ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA**: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla. Mheshimiwa *Captain* Mstaafu Mkuchika dakika tano atafuatiwa na Mheshimiwa Januari Makamba, dakika kumi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nataka nianze kwa kuunga mkono hoja. Vile vile napenda kumpongeza Waziri wa Fedha kwamba baada ya kutoka Chuoni kufundisha akaja kwenye siasa. Hotuba aliyoitoa mwaka huu ya utangulizi wa Serikali hii imefanya nini, ameshahitimu siasa. Alimaliza kila kitu katika yale mambo kumi aliyoyasema yaliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano, basi hotuba ya Waziri wa Fedha hakuna hotuba yako imenoga kama ya mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, upande wangu Utumishi na Utawala Bora kulikuwa na hoja kama tatu nitazieleza kwa kifupi. Kwanza ni suala la ajira, Wabunge wengi wamesimama wametaka kufahamu suala la ajira

likoje. Nataka nieleze tu kwamba Serikali kwa makusudi ilisimamisha ajira kwa muda katika kipindi cha kuhakiki watumishi. Maana unaweza ukampa mtu *promotion* kumbe mfanyakazi yule *fake*, unaweza kumpa mtu *promotion* kumbe vyeti vyake sio halali. Ndio maana ikasimamishwa kwanza, ili zoezi la uhakiki likashakamilika zoezi lianze. Zoezi limekamilika, tumewabaini wafanyakazi hewa 19,708, tumewabaini vyeti fake 14,409, tazama pesa kiasi gani tumeokoa. Malengo ya uhakiki makubwa ni mawili:-

Mheshimiwa Spika, kwanza tuwapate watu wafanye kazi ambayo wanataaluma nayo. Mtu anaingia *theatre* anapasua watu awe ni mtu ambaye cheti chake kinamruhusu kupasua watu. Tumewabaini watu wanavaa majoho meupe wanaingia walikuwa wanafanya *operation* sasa hatuwezi kucheza na maisha ya watu. Ndio maana Serikali ikasema kwanza, tuwe na uhakika kila mmoja anafanya kazi ambayo ana taaluma nayo.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine nalo Utawala Bora ni kusimamia rasilimali za umma zitumike vizuri. Unapowalipa wafanyakazi hewa, unapowalipa watu ambao vyeti vyake si sahihi, hayo ni matumizi mabaya ya fedha za umma. Kwa hiyo, nataka niseme baada ya hili zoezi kukamilika tumeshaanza ajira, mpaka Juni, tutakuwa tumeajiri watumishi 22,150 mpaka tarehe 30 ya mwezi huu.

Mheshimiwa Spika, katika hao Walimu ni 7000 tayari *process* ya ajira inaendelea na Afya 8000. Kwa hiyo, nataka niwaombe Wabunge wenzangu wale ambao tunasimamia ujenzi wa zahanati tusiwe na mashaka, tumalize zahanati hakuna zahanati itakayokamilika ikaacha kufanya kazi eti kwa sababu haina watumishi, tutawaajiri. Hilo ni la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, ilikuwa upande wa mishahara na hili limeongelewa na Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim wa Mtambile, Mheshimiwa Susan Kiwanga wa Mlimba na Ndugu yangu Mheshimiwa Mwita Waitara. Kifupi walisema kwamba, watumishi wa umma

hawajaongezewa mishahara kwa muda mrefu sasa na pia hata nyongeza yao ya mwaka *(increment)* hawapewi. Hali hii inasababisha wanapostaafu kupata mafao kidogo. Maelezo ya Serikali ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, si sahihi kwamba watumishi wa umma hawajaongezewa mishahara kwa muda mrefu kwani nyongeza hiyo haikutolewa kuanzia mwaka 2016/2017. Kama nilivyoeleza kutokana na uamuzi wa Serikali kupitia Muundo wake na kufanya zoezi la uhakiki watumishi. Aidha, hivi sasa Serikali inaboresha utoaji wa huduma ya elimu na afya na kutekeleza miradi maendeleo ambayo itakuwa chachu ya ukuaji wa uchumi na maendeleo kwa ujumla katika siku za baadaye.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uwezo wa kibajeti imekuwa vigumu kugharamia utoaji wa huduma ya elimu na afya, kutekeleza miradi hiyo mikubwa pamoja na kuongeza mishahara kwa wakati mmoja. Uwezo wa bajeti utakapokuwa mzuri Serikali itatoa nyongeza na mishahara kwa watumishi wake.

Mheshimiwa Spika, tulipokuwa Iringa kwenye Sikukuu ya Wafanyakazi, Mheshimiwa Rais alisema hali ya hewa, akiona kwamba hali ya hewa inaruhusu hatangoja kupandisha siku ya sikukuu, hata ngoja kupandisha siku ya mwaka mpya, muda wowote hali itakaporuhusu mishahara itapanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali ilitoa nyongeza ya mwaka *Annual Salary Increment* kwa watumishi wa umma na itaendelea kutoa nyongeza hiyo katika mwaka wa fedha 2018/2019 na miaka mingine kadri ya uwezo wa bajeti utakavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho lilihusu upandishaji vyeo. Hili lilitolewa na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda na Mheshimiwa Dkt. Prudenciana Kikwembe. Hoja ilikuwa kwamba Serikali ya Awamu ya Tano ilizuia stahiki mbalimbali

watumishi ikiwemo upandishwaji madaraja kupisha zoezi la uhakiki. Kwa kuwa zoezi limekamilika watumishi wamepandishwa madaraja, kwa tarehe za sasa na sio kwa tarehe walizostahili kupanda madaraja. Hali hiyo inasababisha watumishi kustaafu na kupata mafao kidogo. Serikali iwalipe stahiki zao watumishi kwa vile zoezi la uhakiki limekamilika.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya Serikali ni kweli Serikali ya Awamu ya Tano ilizuia stahiki mbalimbali za watumishi ikiwemo upandishaji madaraja ili kupisha zoezi la uhakiki ambalo lilifanyika kwa manufaa makubwa na kuokoa kiasi kikubwa cha fedha za Serikali kwa kuondoka watumishi hewa. kama nilivyosema 19,708, watumishi wenye vyeti *fake* 14,405. Hata hivyo kwa watumishi...

**SPIKA**: Mheshimiwa Waziri malizia.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, *paragraph* moja tu naisoma.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kwa watumishi ambao walikuwa na barua ya kupandishwa vyeo, mishahara yao iendelee kubadilishwa katika mifumo shirikishi na taarifa za kumbukumbu za watumishi kila mwezi kwa kuzingatia tarehe walizostahili kadri ya tarehe yao ya kustaafu kazi kwa umri ilivyokaribia.

Mheshimiwa Spika, iwapo kwa bahati mbaya yupo mstaafu ambaye alikuwa na bahati ya kupandishwa cheo lakini mshahara haujabadilika hadi alipostaafu; mstaafu wa namna hii anashauriwa aende kwa aliyekuwa mwajiri wake amjazie fomu maalum ya madai ya malimbikizo ya mishahara inaitwa Mheshimiwa Spika, *Salary Arrears Claims Form* ili aweze kulipwa madai yake kwa njia za hundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, kama nilivyosema naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mkuchika. Mheshimiwa Januari Makamba atafuatiwa na Mheshimiwa Angella Kairuki, dakika kumi kila mmoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia bajeti hii na nianze kwa kukupongeza kwa jinsi unavyoongoza Bunge letu vizuri kwa busara na hekima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Mpango, Waziri wa Fedha, Naibu Waziri wa Fedha, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote. Nimefuatilia mijadala ya bajeti hata kabla ya hapo, mijadala mbalimbali iliyohusu Wizara ya Fedha. Bahati mbaya sana katika baadhi ya mambo niliyobaini ni mashambulizi binafsi kwa Mheshimiwa Dkt. Mpango *(personal attack)*, kwamba kuna wakati tabia yake, kwamba ana kiburi, ilikuwa inazungumzwa kuna wakati hata elimu yake inatiliwa mashaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati mwingi kilichopo mezani huwa ni hoja, lakini bahati mbaya, mimi bahati nzuri nimepata kumfahamu Mheshimiwa Dkt. Mpango miaka kumi tumekuwa wote, alikuwa msaidizi wa Rais, Uchumi mimi nilikuwa Msaidizi wa Rais, Hotuba, nimefanya nae kazi kwa karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukitaka kujua *humility* au *humbleness* ni Dkt. Mpango, hii habari ya kiburi, binafsi na wote ambao tuna-*interact* naye binafsi hiyo haipo. Kwa hiyo nadhani wakati mwingine humu ndani ya Bunge tupingane tu na ni haki na ni sahihi, kuwa na mawazo tofauti ya alicholeta mezani lakini tunapomwendea binafsi tunakuwa tunakosea. Wakati mwingine sio yeye tu hata humu ndani baina ya Wabunge na Wabunge, umebaini Mbunge anapotoa hoja kinachojibiwa sio alichosema bali ni yeye yukoje na anaishi wapi na anafanya shughuli gani na yote ambayo yamezungumzwa yanakuwa sio tena hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Bunge la namna hiyo nadhani sio Bunge unalolitaka na sio Bunge linalostahili hadhi na uzito wako kama wewe Spika. Kwa hiyo, nataka ni-*vouch*, nimtetee Dkt. Mpango kwamba namfahamu na pia ukiondoa tu tabia yake ya kusikiliza na kuheshimu kila mtu, pia ni msomi mzuri bila shaka yoyote. Amefanya kazi Benki ya Dunia, ameaminiwa na Marais wawili, amepitia kwenye mikono ya Profesa Ndulu ambaye tunamsifu ni gwiji wa uchumi hapa nchini, ameaminiwa nje ya nchi na ndani ya nchi na pia ni mcha Mungu, kaka yake ni Askofu anatoka huko katika familia ya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Dkt. Ashatu wote ambao tunapishana naye kwenye *corridor* hatuwezi kusema kwamba, ana kiburi, tunamjua kwamba mtu ana heshima. Vilevile watalaam wa Wizara ya Fedha wakiongozwa na Bwana Dotto na wao pia ukimfuata bwana Dotto anakusikiliza na anafanya maamuzi akielewa jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niliona wakati tunaongelea bajeti hawa viongozi wetu wakuu ambao tumewapa kazi kubwa sana ya kuandaa bajeti na kuiwasilisha na kujibu siyo kazi ndogo wanaifanya kwa niaba yetu sisi Watanzania. Hivyo, tusiwapeleke kule ambapo tutazidi kuwatia msongo wa mawazo kwamba kazi wanayofanya hatuithamini. Kwa hiyo, nawapongeza kwa weledi wao lakini pia kwa hulka zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kuna hoja mbili, tatu zimetolewa hapa...

**SPIKA:** Kabla hujaenda kwenye hoja Mheshimiwa January, wala usikae, nataka kumwambia Mheshimiwa Dkt. Mpango na Mheshimiwa Dkt. Ashatu, katika siasa alichokifanya January ndiyo kinachopaswa kufanywa. Yaani katika siasa lazima upate watu wakusemee, lakini ukisema mwenyewe jamani mimi mtu mzuri, watu watasema unaona. Kwa hiyo, ni jambo zuri sana amelifanya, namshukuru sana kwa niaba yetu, endelea Mheshimiwa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, naomba nikuthibitishie kwamba sikukaa chemba na Mheshimiwa Dkt. Mpango kabla ya kuzungumza hapa siku ya leo. Kwa hiyo hizi ni hisia kabisa binafsi na zinawasilisha mawazo mengi hapa katika Baraza la Mawaziri na Wabunge wengi ambao tunafanya kazi na Mheshimiwa Dkt. Mpango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mambo kadhaa yamezungumzwa kuhusu muungano hasa kubwa ni hoja ya Mheshimiwa Dkt. Ally Yussuf Suleiman ambaye ametaja mambo matatu, ambayo napenda kuchukua nafasi hii kuyajibu harakaharaka.

Mheshimiwa Spika, la kwanza ni akaunti ya pamoja, amesema muda mrefu akaunti hii haijaanzishwa. Ni kweli na akaunti hii ya pamoja imewekwa ni hitaji la kikatiba kifungu cha 133 cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kinaelekeza kwamba kuwe na Mfuko wa Akaunti ya Pamoja ya Fedha ambayo itakuwa sehemu ya Mfuko Mkuu wa Hazina ambapo kutawekwa fedha yote itakayochangwa na Serikali mbili kwa kiasi kitakachoaamuliwa na Tume ya Pamoja ya Fedha. Hilo ndiyo neno la msingi, kwa kiasi kitakachoamuliwa na Tume ya Pamoja ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Akaunti hii ya Pamoja haijakuwepo kwa sababu mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha kuhusu kiwango cha mgawanyo ndiyo yanafanyiwa kazi na Serikali sasa hivi. Hili ni jambo kubwa linahitaji uamuzi wa Mabaraza yote mawili ya Mawaziri ya pande zote mbili na linahitaji *input* kubwa ya wataalam.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kinachoendelea sasa hivi ni kusubiri maamuzi baada ya wataalam kuwa wanamalizia kazi yao. Kwa hiyo, sisi kama Serikali azma ya kutimiza matakwa ya kikatiba bado ipo palepale, lakini kwa kuwa ni jambo kubwa lazima tuliendee kwa umakini na utaratibu ili liweze kufanikiwa kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, suala la pili lililozungumzwa kuhusu Muungano ni suala la mchakato wa sasa hivi unaoendelea wa usajili wa meli. Kama unavyofahamu Tanzania ina aina mbili ya usajili wa meli; kuna usajili wa meli za ndani na usajili wa meli za nje zinazopeperusha Bendera ya Tanzania. Kwamba mtu yuko nje ya Tanzania ana meli yake, lakini anataka atumie Bendera ya Tanzania. Usajili huo unafanywa na Mamlaka Zanzibar ndiyo tulivyokubaliana, usajili wa meli za ndani unafanywa na *SUMATRA*. Sasa kulitokea changamoto ya kutokuwepo na uangalifu na umakini katika usajili wa meli za nje zinazopeperusha Bendera ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kilichojitokeza ni kwamba meli zinazopeperusha Bendera za Tanzania zilikutwa nje ya nchi zinafanya makosa makubwa, kubeba silaha, magendo, madawa ya kulevya na kupaki kwenye Bandari zisizoruhusiwa. Kwa hiyo, Serikali ambacho tumeamua kufanya siyo kuinyang'anya Zanzibar mamlaka ya usajili hapana, kwamba hili jambo la usajili tushiriki wote. Kwamba asiwe mtu Dubai ana muhuri tu yeye anagonga tu na kukabidhi bendera, lazima vyombo vya Usalama vya nchi vishiriki, kwa sababu tunapotoa bendera yetu, ni alama ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tulikubaliana kwamba wenzetu watafanya lakini wasifanye peke yao kuwe na *input* ya Vyombo vya Ulinzi na Usalama na *due diligence* wa meli zote zinazoomba kutumia Bendera ya Tanzania. Kwa hiyo, hicho ndicho kinachofanyika na wala wenzetu Wazanzibari wasione tunawapora na kwa kweli ni muhimu haya mambo kuyajua kabla ya kuyasema, kwa sababu yanaamsha hisia ambazo si sahihi.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni Kisiwa cha Fungu Mbaraka au Latham; kwamba Mheshimiwa Dkt. Ally Yussuf Suleiman alisema kwamba Tanzania Bara inataka kupora Kisiwa hiki kwa sababu kuna rasilimali. Labda niseme kwamba nchi yetu ni moja hatujafikia mahali pa kugombea eneo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**SPIKA:** Kinaitwaje Kisiwa hicho?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Naam.

**SPIKA:** Kisiwa hicho kinaitwaje?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, kinaitwa Fungu Mbaraka au Latham kipo katikati hapa Bahari ya Hindi. Kwa hiyo, kuna dhana inajengeka kwamba kuna mgogoro kati ya Bara na Zanzibar kuhusu umiliki wa Kisiwa hicho.

Mheshimiwa Spika, chanzo cha mgogoro ni kwamba inawezekana eneo lile lina mafuta. Sasa hii dhana inaenea na inaamsha hisia. Sasa niseme tu kwamba huko nyuma wakati suala la mafuta ni la Muungano na *TPDC* ndiyo ilikuwa inatoa leseni ni kweli pale mahali palitolewa *blocks* za kuchimba, kutafuta mafuta.

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya wale waliyotafuta mafuta hawakuyapata, kwa hiyo wakarudisha zile *block*, kwa hiyo, mpaka leo lile eneo halina mtu anayetafuta mafuta. Kwa hiyo dhana kwamba tunagombea eneo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania siyo sahihi, Katiba zetu ziko wazi kuhusu maeneo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nchi yetu hii ni moja, Zanzibar ikinufaika Tanzania imenufaika, Bara ikinufaika Tanzania imenufaika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kwa wenzetu Wanzazibari na Watanzania kwa ujumla kusijengeke dhana kwamba tunagombana kuhusu eneo lolote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, umezungumza kuhusu lugha humu ndani za ukabila na ukanda na mengineyo. Hata hivyo, kuna moja ambalo ni muhimu kulizungumza lugha zinazohusu Muungano wetu. Namna ambavyo tunauchangia na kuuelezea Muungano wetu ni kana kwamba bado hatujakubaliana kuhusu umuhimu wake na kwamba

tumeamua kuungana. Kuna lugha kali sana ambazo zinafadhaisha watu wa upande mmoja na kudhalilisha upande mmoja au mwingine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningependa utumie rungu lako na kiti chako na joho lako na busara zako kukemea hizi lugha ambazo zina-*condemn* kwa ujumla watu wa upande mmoja au mwingine kuhusu Muungano. Muungano wetu sisi tumeamua kuwa nchi moja, tumeamua kuwa jeuri na kutengeneza mipaka yetu ya Tanzania. Kwa hiyo, naomba urithi huo tuulinde na Bunge lako lichukue uongozi katika kuulinda urithi huo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa January Makamba. Mheshimiwa Angellah Kairuki atafuatiwa na Mheshimiwa Luhaga Mpina ambaye atakuwa wa mwisho kwenye michango.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nipende tu kusema kwamba naunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri kwa asilimia mia moja. Kipekee tu napenda kumpongeza sana yeye Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa Hotuba nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la kwanza, kama msimamizi wa Sekta ya Madini nipende tu kutoa shukrani sana kwa Serikali kupitia kwake Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa kukubali kuweza kufuta tozo zilizokuwa zikitozwa katika chumvi, tozo takribani 10 kati ya 16 ambazo kimsingi zilikuwa zimesababisha sana gharama za uzalishaji wa chumvi kuwa kubwa na pia kumsababishia mchimbaji wetu mdogo wa chumvi kutokuweza kupata faida.

Mheshimiwa Spika, ilikuwa kwa takribani gunia la kilo 50 walikuwa wanapata faida ya Sh.150 tu ilikuwa ni faida ndogo. Pia walikuwa wanashindwa kushindana kisoko na

matokeo yake ilikuwa chumvi ya kutoka nchi za jirani ilikuwa inaingia kwa wingi zaidi na hatimaye sisi ambao tuna chumvi nyingi humu kutoweza kufanya biashara au kuwa na ushindani. Kwa hiyo nipende tu kusema kwa niaba ya Sekta ya Madini na Wizara tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja ya Mheshimiwa Musukuma kuhusiana na tozo au kiwango kikubwa cha kodi kinachotozwa katika madini ya dhahabu au kwa wachimbaji wetu wadogo wa dhahabu na alikuwa ameeleza kwamba kuna tozo ya asilimia takribani kumi na nne (14%).

Mheshimiwa Spika, nipende tu kumweleza Mheshimiwa Musukuma kwamba kwa mujibu wa Sheria yetu ya Madini Sura namba 123, wachimbaji wadogo wanatozwa takribani asilimia 12.3 ya kodi ambayo inajumuisha mrabaha wa asilimia sita, inajumuisha kodi ya zuio ya asilimia tano, ada ya ukaguzi wa uzalishaji wa madini asilimia moja, pamoja na ushuru wa huduma au *service levy* kwa halmashauri kwa asilimia 0.3 ambayo jumla yake ni asilimia 12.3 na kwa upande wa wachimbaji wakubwa na wa kati wao wanatozwa mkokotoo wa asilimia 37.3.

Mheshimiwa Spika, alipendekeza kodi kwa wachimbaji wadogo ziondolewe; nipende tu kumweleza Mheshimiwa Mbunge kwamba tumekuwa tukiliona na kwa kuwa Serikali yetu ni sikivu kama ambavyo tumefanya katika chumvi. Niendelee tu kuwaomba shirikisho la Vyama vya Wachimbaji Wadogo *(FEMATA)* tukae, tuweze kulizungumza suala hili na kuliona ni kodi zipi au ni tozo zipi ambazo zinaweza zikafikiriwa kuzingatiwa katika punguzo hilo au kuweza kuondolewa.

Mheshimiwa Spika, lengo letu kubwa kama Serikali nikuhakikisha kwamba tunakuwa na uchimbaji mdogo, uchimbaji mdogo ambao utakuwa na faida kwa wachimbaji wetu. Lakini pia sisi kama Serikali bado tunaendelea kuona ni namna gani tunawasaidia kwa upande wa teknolojia,

masuala mazima ya mtaji, mafunzo, kupata masoko lakini zaidi kuwapa teknolojia mpya na waweze pia kujifunza teknolojia ya kisasa katika uchimbaji.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia kupitia Serikali kupitia bajeti yetu ya Wizara ya Madini katika mwaka ujao wa fedha tutajenga vituo vya mifano vitano katika maeneo ya Chunya, Bukombe, Rwamgasa, Tanga pamoja na Kilwa. Pia tutajenga vituo saba vya umahiri Mpanda, Handeni, Musoma, Songea, Bariadi, Bukoba na kwingineko.

Mheshimiwa Spika, lengo letu kubwa ni kuhakikisha kwamba tunawafundisha kwa mfano ili waweze kuchimba kwa teknolojia ya kisasa kupitia vituo hivyo ambavyo tumeviweka kwa gharama nafuu sana, lakini hatimaye lengo letu ni kuhakikisha kwamba tunawarasimisha ili waweze kuingia katika mfumo rasmi wa kibiashara pamoja na kikodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho nipende tu kuoa rai kwa Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa, kuhakikisha kwamba wanazingatia viwango vya tozo za kodi vilivyoanishwa katika Sheria. Wako wengine unakuta wameenda katika maduara ya uchimbaji wa Madini, unakuta wanaambiwa wakivuna mifuko 10, mifuko labda mitano inaenda kwenye Halmashauri. Niombe sana tuzingatie viwango ambavyo vimeainishwa kisheria ili kuhakikisha kwamba wachimbaji wetu hawa wadogo hatimaye wanaweza kukua.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Sera yetu ya Wizara ya Madini na Serikali kwa ujumla wachimbaji hawa hadhi yao hii si ya kudumu wanatakiwa tu watumie hadhi ya uchimbaji mdogo kama daraja hatimaye waweze kuwa wachimbaji wa kati na hatimaye pia kuwa wachimbaji wakubwa kama ambavyo wengine kama wakina *Busolwa Mining* pamoja na akina Mzee wangu Marwa wameweza kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja pia ya zuio la usafirishaji wa *carbon*, hoja hii nadhani leo nitakuwa

nasimama kwa mara ya tatu kuweza kuielezea. Kaka yangu Mheshimiwa Musukuma ameweza kuieleza lakini nipende tu kurudia maelezo ya Serikali kwamba zuio letu la usafirishaji wa *carbon* liko palepale kama nilivyotoa maelezo yangu tarehe Mosi Juni, kama nilivyotoa maelezo yangu pia tarehe 14 Juni.

Mheshimiwa Spika, nipende tu kwa kweli kuwapongeza sana wamiliki wa *Illusion Plants* takribani watano kwa Kahama tayari wameshaanza kujenga *Illusion Plants* hizo. Nipende pia kuwapongeza wawekezaji takribani watatu ambao wameshaanza kuonesha nia ya kuwekeza Shinyanga, vile vile pia niwapongeze sana wawekezaji wengine watatu ambao wameonesha nia ya kuwekeza katika maeneo ya Tabora.

Mheshimiwa Spika, zaidi niwapongeze sana Kampuni ya *GEMAAfrica* ambao tayari wameshakamilisha kujenga mtambo wa *Illusion Plants* Wilaya ya Geita. Nipende kuwapongeza Kampuni ya *Transco Gold* pamoja na Nyamigogo, *Nang'ana Group* pamoja na *Busamu Company* ambao nao wameshakamilisha ujenzi wa *Illusion Plants* katika Wilaya ya Kahama.

Mheshimiwa Spika, kipekee pia niwapongeze *Framal Investment* ambao tayari nao wameshakamilisha ujenzi wa mitambo yao katika Wilaya ya Musoma pamoja na *Deep Mine Service* ambayo kwa sasa na wenyewe wanatafuta eneo la kujenga mitambo husika ya *Illusion Plants* katika Wilaya ya Kahama.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Geita na Tarime bado watu wengi wamekuwa wakionesha nia. Nipende tu kuwakaribisha sana wawekezaji na Watanzania wengine kuona ni namna gani wanatumia fursa hii kuwekeza katika ujenzi wa *Illusion Plants* katika sehemu ambazo bado wawekezaji hawajenda lakini pia huduma zao zinahitajika. Hata hivyo, nipende kusema kwamba agizo la Serikali bado linasimama palepale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kuhusiana na Mheshimiwa Ole Millya alieleza kwa kina sana kwamba mapendekezo ya Kamati Maalum ya Mheshimiwa Spika iliyochunguza mnyororo mzima wa biashara ya uchimbaji wa *Tanzanite* kwamba hayajatekelezwa. Nipende tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu hata siku moja hatuwezi kudharau mapendekezo au maazimio ya Kamati Maalum ya Spika ambayo tunaamini ni mapendekezo ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, vilevile nipende tu kueleza tu kwamba kama ambavyo tulieleza tarehe Mosi, Juni, 2018 katika hotuba yangu ukurasa wa 46, tulieleza namna kabisa masuala mazima ya majadiliano kupitia ubia wa Kampuni ya *Tanzanite One* pamoja na *STAMICO* yanavyoendelea na tulieleza katika hotuba yangu ukurasa wa 46 kwa wale ambao watakuwa nayo wanaweza kufuatilia.

Mheshimiwa Spika, tumeotoa maelekezo kwa Kampuni ya *Tanzanite One* pamoja na *STAMICO* kurudisha leseni ya uchimbaji ili iweze kuandaliwa utaratibu mpya ambao utaiwezesha Serikali na Taifa kwa ujumla kuweza kunufaika zaidi katika uchimbaji na biashara nzima ya *Tanzanite* kwa kuzingatia Sheria ya Madini, Sura namba 123.

Mheshimiwa Spika, hayo mengine ya kusema yamegawia, sijui imekuwaje mara imehuishwa, nipende tu kusema kwamba niwaombe Waheshimiwa Wabunge wajikite zaidi katika maelezo ya Mheshimiwa Kabudi aliyoyatoa tarehe Mosi, Juni lakini pia wajikite katika kufanya *reference* katika hotuba yangu niliyoitoa ya bajeti katika ukurasa ule wa 46. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nipende tu kusema kwamba katika makubaliano yale ambayo Kamati ya Majadiliano ya Taifa kupitia kwa Kiongozi Mheshimiwa Kabudi, makubaliano yaliyoingiwa tarehe 15 Aprili na Kampuni ya *Tanzanite One* tayari wameshaanza kulipa mkupuo wa kwanza wa fidia

ambayo walikuwa wameelekezwa na *obviously* fidia hii inaingia kwa Taifa na kuna taratibu zake kwa mujibu wa Wizara ya Fedha kwa malipo kama hayo yanalipwa kwa taratibu gani.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru na napenda kusema tu kwamba, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Angellah Kairuki, Waziri wa Madini, tunakushukuru sana. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Mpina, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, tafadhali dakika 10.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi uliyonipa ili niweze kuchangia katika hotuba hii iliyo mbele yetu ya Bajeti Kuu ya Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Mpango pamoja na Naibu wake.

Mheshimiwa Spika, kwanza niungane kwa dhati kabisa kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya katika Taifa hili katika kupigania maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nifunguke tu kwamba Bunge lako hili kabla ya mimi sijawa Waziri hapa nimepitia maeneo mengi sana na Bunge hili limenipeleka kwenye Taasisi mbalimbali kwenye Mabunge ya Afrika, nimeenda kwenye Mikutano mingi ya kikanda na ya Kimataifa sijawahi kuona Kiongozi ambaye *committed* kama Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Nampongeza sana kwa kazi kubwa anayoifanya katika nchi yetu hii ya Tanzania katika kupigania maendeleo ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nikupongeze wewe sana, moja ya sifa ya Kiongozi ni kutengeneza viongozi. Toka ulivyokuwa Mwenyekiti wa Bunge hili, baadaye ukawa Naibu Spika, baadaye ukawa Spika umetengeneza viongozi wengi sana kwenye Bunge hili. Kwa hiyo, uwezo wako siyo wa kutiliwa mashaka yoyote na mtu yeyote anayejua historia na mimi

pia tu nikuombe kwamba kwa baadhi ya wale Wabunge wageni ambao hawaijui historia wasiwe wanakurupuka kushambulia watu wasiowajua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na nirudie pia kumpongeza sana Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango na Naibu wake Ashatu Kijaji kwa kazi kubwa sana ambayo wanayoifanya katika kulinda uchumi wa nchi yetu. Katika kipindi hiki kifupi cha Utawala huu wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na Serikali hii ya Awamu Tano mambo mengi yamefanyika sana, mageuzi makubwa yamefanyika ya kiuchumi ambapo Mheshimiwa Dkt. Mpango tunampongeza sana kwa kazi hiyo kubwa kwa kuendesha hilo gudurumu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mtakumbuka na Wabunge watakumbuka hapa na wengine wameni-*refer* kwenye michango yao niliwahi kulia mbele ya Bunge hili na kukataa Bajeti ya Serikali, kipindi ambacho kilikuwa kigumu sana kwangu pia kwa chama changu, lakini yalikuwa ni baadhi ya mambo ambayo leo hii yamefanyiwa marekebisho makubwa na mageuzi makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo mambo makubwa nsihukuru, nimpongeze hapa Mheshimiwa Stanslaus Mabula ambaye alipata nafasi hapa ya kuchangia kuna mambo makubwa katika Taifa hili ambayo tulikuwa tukiingia hasara kubwa na tulirekodiwa kati ya nchi ambayo ina-*facilitate* zoezi la *Illicit Financial Flow* kwa kiwango kikubwa. Hata hivyo, mapambano yaliyowekwa, *mechanism* zilizowekwa, kupiga vita suala la *Illicit Financial Flow* katika nchi yetu, huwezi kuamini leo akina nanii ambao wanafanya tathmini ya *Illicit Financial Flow,* tunawakaribisha Tanzania waje watu-*access*.

Mheshimiwa Spika, watakuja kuona jinsi udhibiti mkubwa uliyofanyika na sasa zoezi hili linafanyika kwa kiwango cha chini sana hapa nchini kwetu. Pia mambo ya

*transfer pricing* vilevile, mambo ya *dollarization* vilevile na suala gumu hili lilishindikana siku zingine suala la *credit rating* na lenyewe katika kipindi hiki limeweza kufanyika. Kwa hiyo, viongozi wetu ambao wanaongoza jukumu hili, Waziri wa Fedha na msaidizi wake, pamoja na Katibu Mkuu wake na wengine wote wanaohusika katika usimamizi wa uchumi wetu tunawapa heko na tunawapongeza sana kwa bidii hizo za kazi.

Mheshimiwa Spika, basi baada ya kusema hayo, niweze kuzungumza kidogo kuhusu baadhi ya mambo ambayo yamezungumzwa ambayo yanatekelezwa katika Wizara yangu:-

Mheshimiwa Spika, moja ni jambo la chanjo na uogeshaji wa mifugo kwamba, tunayo shida kubwa. Ni kweli kabisa nakubali kwamba, suala la chanjo na uogeshaji wa mifugo ambapo mifugo mingi inakufa kila mwaka kwa kukosa chanjo na mifugo mingi inakufa kila mwaka kutokana na kupe na kwa kutokana na kutokuogeshwa. Sasa tunafanya kila aina kuhakikisha kwamba, jambo hili tunalifanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, Chuo chetu cha Utafiti cha Uzalishaji wa Chanjo cha Kibaha kinaendelea vizuri kuzalisha chanjo hapa nchini. Vilevile tumepata bahati ya kupata mwekezaji mpya kutoka India ambaye naye anakuja kujenga kiwanda hapa kwa ajili ya kuzalisha chanjo kwa wingi. Kwa kufanya hivyo, tutaweza kuwahakikishia wananchi wetu na kuwa-*guarantee* kupatikana kwa chanjo kwa muda na kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kama hiyo haitoshi pia, kwamba, Wizara yangu inatengeneza sasa mpango ambao utawezesha chanjo kupatikana kiurahisi, lakini vilevile uogeshaji wa mifugo kuwezekana kwa urahisi na vilevile kwa bei ambazo wafugaji wetu watazimudu. Kwa hiyo, jukumu hilo linafanyika na mpango huo tutahakikisha kwamba, wafugaji wote, halmashauri zote zinashirikishwa katika kuutekeleza.

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine la pili liliwahi kuzungumzwa hapa Bungeni kuwa ni suala la uzalishaji wa maziwa hapa nchini na hasa ikilinganishwa nchi yetu na nchi ya Kenya kwamba, sisi tunazalisha mpaka sasa hivi lita za maziwa bilioni 2.4 wakati Kenya wanazalisha bilioni 5.2.

Mheshimiwa Spika, katika ulinganifu huo ni kweli kabisa, lakini nataka kuwa-*assure* Waheshimiwa Wabunge kwamba, kutangulia si kufika, tumejipanga vizuri katika kuhakikisha kwamba, tunakuja na uzalishaji mkubwa wa maziwa hapa nchini. Sisi hatuwezi kushindana na Kenya, hatuwezi kushindana na nchi yeyote ile ya Afrika kwa sababu, sisi kama ninavyosema, ni nchi ya pili tu kuwa na mifugo mingi hapa Afrika ikiwa nchi ya kwanza inayoongoza mpaka sasa hivi ni Ethiopia.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, sisi tuna malisho mazuri kuliko mtu yeyote, tuna maji bora kuliko mtu yeyote pamoja na kwamba, ng'ombe wa maziwa sasa hivi ni 789,000 tu, lakini mpango tulioanzisha sasa hivi wa kuhimilisha mifugo yetu ambao tunaita *this is a massive artificial insemination* ambapo tutahimilisha kila mwaka kutafuta mitamba milioni moja kwa mwaka, kwa miaka mitatu tutakuwa na mitamba milioni tatu na tutaweza ku-*compete* na yeyote na tutaweza kuzalisha maziwa mengi kuliko mtu yeyote. Tuna mifugo, tuna maeneo mazuri na swali hili limenifurahisha na liliulizwa na Mheshimiwa Jesca. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini niseme kwamba, Kituo chetu cha Taifa cha Uhimilishaji *(NAIC)* tumekifanyia ukarabati mkubwa sana ambao utawezeasha kuzalisha mbegu nyingi za kutosha. Tumenunua madume bora 11, kuna mtu mmoja aliwahi kuchangia hapa Bungeni akasema kwamba, madume hayo 11 hayawezi kutosheleza na kwamba, ni kidogo mno na kwamba, Serikali haiko *serious.*

Mheshimiwa Spika, niwaambieni kwamba, haya madume 11 yanaweza kuhimilisha ng'ombe zote wa Afrika Mashariki. Mbegu zinazozalishwa na madume 11 zinaweza kuhimilisha mahitaji yote ya uhimilishaji katika nchi za Afrika

Mashariki. Kwa hiyo, tumejipanga vizuri na tutakuwa na maziwa mengi ya kutosha katika nchi yetu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, duuh! Haya madume 11 haya, naona madume ya Kisukuma haya, yanaweza kushughulikia ng'ombe wote nchi hii hatari kubwa, lakini ndio taarifa za kisayansi hizo. *(Makofi/ Kicheko)*

Sasa tunakuja kwa Mtoa Hoja na Msaidizi wake. Kama mnavyojua tumeongea kwa siku saba mfululizo, mambo ni mengi. Kwa kweli, sio rahisi kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuyagusa yote, tunawashukuru Waheshimiwa Mawaziri ambao wametangulia kupunguza baadhi ya mambo ambayo yalikuwa yanagusa *Sectoral Ministries,* basi sasa moja kwa moja nimwite Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha na Mipango, Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, ili aanze kwa dakika 20 halafu tutamwita mtoa hoja ahitimishe hoja yake.

Mheshimiwa Naibu Waziri karibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii. Kabla sijaanza kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujalia sote fursa hii ya kuwepo katika jengo lako hili Tukufu kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, pia baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, kama ilivyo kawaida, napenda niwashukuru wazazi wangu wawili, Mzee Kijaji na Mke wake Mama Aziza Abdallah, nawashukuru sana kwa malezi yao kwangu yaliyonifikisha hapa nilipo siku hii ya leo.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa kazi kubwa

anayoifanya katika Taifa hili kwa kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo alizunguka Taifa hili kuinadi ilani hiyo. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, hakika yuko makini anatekeleza kile ambacho aliwaahidi Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza pia, Mheshimiwa Mama yetu Mama Samia Suluhu Hassan, mama wa mfano kwa Taifa la Tanzania. Amekuwa ni mama yetu wa mfano, sisi wanawake tunajivuna kuwa na mama kama yeye, aendelee kupambana sisi wanawake wenzake tuko naye sambamba kuhakikisha tunayatenda kwa ajili ya watoto wa kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru na nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo yake kwetu sisi tulio chini yake. Kwa kweli, ni kiongozi imara, ni kiongozi makini, busara zake zinatuwezesha kufika hapa tulipo siku hii ya leo.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru wewe pia, kaka yangu, Mheshimiwa Spika Job Yustino Ndugai, kwa uongozi wako imara kwa Bunge letu Tukufu na Waheshimiwa Wenyeviti na watendaji wote wa Bunge letu Tukufu. Naomba niseme kwamba, najivunia na najisikia faraja kuwa ni Mbunge kutoka moja ya Majimbo ya Dodoma ambako wewe ni mlezi wetu, najivunia sana Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nimshukuru Mheshimiwa Waziri wangu wa Fedha. Kwa mara ya kwanza niliposimama ndani ya Bunge hili, miaka miwili iliyopita, tukiwa tunawasilisha bajeti ya Serikali kama hivi, nilimwambia Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba, najivunia kufanya kazi chini yake. Miongozo yake, ushauri wake kwangu kwa kweli, ameweza kunifanya nisimame na kuwa ni mmoja wa Manaibu Waziri imara kabisa.

Mheshimiwa Spika, ulisema huwezi kujisifu mwenyewe, lakini naomba nijisifu mwenyewe na sijafika hapa ni kwa

sababu, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango ananipa nafasi ya kutenda haya ninayoyatenda. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri na nakuombea kwa Mwenyezi Mungu azidi kukuimarisha, busara yako inatungoza sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia, niwapongeze sana watendaji wote ndani ya Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu Mheshimiwa Dotto James. Niliwaeleza tulipoanza mchakato huu mwezi Machi nikawaambia, kama ni siku basi ilikuwa alfajiri ule mwezi wa Machi na leo hii tarehe 26 mwezi Juni basi ni saa 12.00 jioni. Naomba niwaambie siku yetu tumeikamilisha kwa ufanisi mkubwa, Watendaji wote wa Wizara ya Fedha najisikia faraja sana kufanya nanyi kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kusema na kama ilivyo kawaida yangu naomba ni-*site* Aya mbili ndani ya Kitabu Kitukufu cha Mwenyezi Mungu, *Quran* na hii naomba iende kwa Mheshimiwa Rais wetu. Mheshimiwa Rais namwambia maneno haya ya Mwenyezi Mungu kutoka *Surat Al-qalam,* Aya ya 7 - 8; Mwenyezi Mungu anasema katika Aya ya 7 kwamba:

*"Falaatutwiil-mukadhdhibina, waddu lautudihinu fayudihinuun"* Mwenyezi Mungu anasema hivi, wala usiwatii wale wanaokadhibisha yale unayoyatenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwambia Mheshimiwa Rais, asiwatii hata kidogo wale wanaokadhibisha jitihada zake anazozifanya kwa ajili ya wananchi wanyonge wa Tanzania. Dunia inaona, jamii inaona, Watanzania wanaona, Watanzania wanasema. Pia nimwambie Mheshimiwa Rais wangu kwamba, hii yote Aya ya pili niliyosema, Mwenyezi Mungu anasema, hao wanaokadhibisha wanatamani ulegeze japo kwa sekunde moja, ili waweze kutulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namwambia Mheshimiwa Rais aendelee kupambana. Sisi tunaona,

Watanzania wanaona na Mwenyezi Mungu akipenda 2019 haya ninayoyasema yatadhihirika ndani ya Taifa la Tanzania. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais endelea kuchapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niseme machache katika hoja ambazo zimewekwa mezani na Waheshimiwa Wabunge wamesema. Hoja ya kwanza nayo imekuwa ni kuhusu Serikali ya Awamu ya Tano kuelekea kuziua halmashauri zetu. Jambo hili limesemwa kwa uchungu na msisitizo mkubwa na Waheshimiwa Wabunge ndani ya Bunge lako Tukufu. Naomba niseme yafuatayo:-

Mhesimiwa Spika, limesemwa jambo hili kwa kisingizio cha kwamba, Serikali ya Awamu ya Tano imechukua makusanyo ya *property tax,* lakini pia makusanyo ya ushuru wa mabango. Tulipitisha sheria ndani ya Bunge lako Tukufu na ndipo tulipoanza kutekeleza hili ambalo linalalamikiwa leo.

Mheshimiwa Spika, na sheria tuliyoipitisha, Sheria ya Fedha ya Mwaka 2017 ilituruhusu kukusanya mapato haya kwenye halmashauri zetu zote ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Serikali siku zote ni sikivu na hasa Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi, ni Serikali sikivu; ilisikiliza maoni yaliyotolewa katika ripoti ya Kamati yako Maalum, maarufu kama *Chenge One. Chenge One* katika taarifa ile walisisitiza kwamba, Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato ya Tanzania ikusanye kodi ya majengo, ikusanye na kodi ya mabango na Serikali iko sikivu tukaanza kuyatenda haya.

Mheshimiwa Spika, kwa nini tumefanya hivyo? Tumefanya hivyo, ili kama ilivyoshauriwa ndani ya *Chenge One* ni kuimarisha makusanyo ya mapato hayo, ili tuweze kuyapeleka kwa Watanzania kwa Taifa zima. Nimshukuru sana na niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri waliosema kabla yangu, wale waliokema ile kuligawa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nilisema mwaka jana wakati nachangia Bajeti ya Wizara ya Fedha kwamba, tuko kwenye hatari kubwa ya kuligawa Taifa hili vipandevipande, ule umimi tuuache ndugu zangu. Tunachokifanya Serikali ya Awamu ya Tano ni kuyakusanya mapato haya na kuhakikisha tunayarejesha kwenye halmashauri zetu kulingana na bajeti za halmashauri husika na ndicho ambacho tumekuwa tukikifanya Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Spika, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge waelewe hiyo dhamira njema ya Serikali yetu, tumekuwa tukifanya hivyo, hakuna halmashauri ambayo imekosa bajeti ya maendeleo, wala bajeti ya matumizi ya kawaida katika utendaji wetu ndani ya miaka mitatu iliyopita. Katika kudhihirisha haya Serikali yetu imekuja na mpango wa kuziwezesha halmashauri zetu kuweza kuja na mipango imara, mipango mikakati kwa ajili ya kuongeza mapato ya halmashauri.

Mheshimiwa Spika, hili napenda kulisema, tuelewane jambo moja, Wakurugenzi wa Halmashauri ni watendaji wakuu wa halmashauri zetu. Hawa wanaitwa ni *CEO* wa halmashauri zetu zote na misingi ya mafanikio ya mtendaji yoyote wa taasisi haijawahi kubadilika kati ya sekta binafsi na sekta ya umma. Ndio maana sasa Serikali imekuja na mpango huu kwamba, tunataka kupima ubunifu wa watendaji wetu, ili tuweze kuwawezesha kuwapa pesa, ili waweze kutekeleza mipango ya maendeleo, lakini yenye tija kwa wananchi wanaowaongoza. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge sisi ni madiwani katika halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kaka yangu Jafo tulifanya kikao tarehe 14 Mei, pale Wizarani tukisaini mikataba ya shilingi bilioni 131.5 kwa ajili ya halmashauri zile zilizoonesha ubunifu wa kubuni miradi ya maendeleo itakayoleta tija kwa wananchi wao, itakayoleta tija kwa halmashauri zao kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Spika, naomba niwasifu sana Wakuu wa Mikoa wafuatao: Mkuu wa Mkoa wa Dar-es-Salaam, Mkuu

wa Mkoa wa Pwani, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Mkuu wa Mkoa wa Geita, Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Mkuu wa Mkoa wa Simiyu na Mkuu wa Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawasifu Wakuu hawa wa Mikoa kwa sababu, wana-*vision,* wana ndoto ndani ya mikoa yao. Wamekaa na watendaji wao baada ya sisi kutoa mwongozo wa kuja na mikakati hii kwa ajili ya kuongeza mapato ya halmashauri, Wakurugenzi wao wakaja na maandiko mazuri ambayo yamepata fedha hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi Jumamosi nilikuwa Mkoani Simiyu. Wengi wakanishangaa, unakwenda kuhitimisha bajeti kesho kutwa, umefikaje Simiyu leo? Nikawaambia niko Simiyu kwa sababu, ni utekelezaji wa bajeti tunayoipitisha. Nilikwenda Simiyu kuangalia viwanda vilivyoanzishwa ndani ya Mkoa wa Simiyu na Halmashauri za Wilaya ndani ya Mkoa wa Simiyu. Nikawa namuuliza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Maswa, nikamwambia baada ya kuanzisha kiwanda hiki cha chaki kwa mwaka mmoja unakusanya mapato kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, akaniambia ndio wameanza, wanakusanya zaidi ya milioni 600 kwa mwaka kwa kiwanda hicho kimoja. Nikamwambia una sababu sasa wewe na Baraza lako la Madiwani la kwenda kusimama kusubiri mapato ya kusubiri mtu anayetoka kujisaidia chooni kwamba, unakusanya mapato? Akaniambia hana sababu kwa sababu, ana miradi ambayo inamuongezea mapato na hana sababu ya kulalamika hajapata mapato kutoka Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, hili napenda lieleweke na liende kwa Wakurugenzi wote wa Halmashauri zote 185 kwamba, Serikali iko tayari. Mkoa wa Simiyu peke yake mikataba tuliyosaini juzi wamepata shilingi bilioni 8.2 kwa ajili ya viwanda vidogo vidogo na ndio maana nimekuwa

nikisema tatizo la Serikali ya Awamu ya Tano sio pesa, tatizo unataka pesa ukafanye nini. Hilo ni jambo la msingi sana, lazima tukae pamoja tuelewane kama viongozi, ili tujue ni nini tunakwenda kufanya na Watanzania tunaenda kuwapa nini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hili niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge hili la kulalamikia mapato haya yaliyokusanywa yamekusanywa yanakwenda wapi?Yamekusanywa halafu yanarejeshwa kwenye halmashauri kulingana na bajeti.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ukiacha hiyo ya kurejeshewa hiyo tumekuja na mkakati wa kuongeza mapato ya halmashauri. Kwa nini tusikae na Wakurugenzi wetu tukaelekezana, wakaandaa maandiko, tukatekeleza, Serikali haijazuia kuanzisha viwanda vidogovidogo.

Mheshimiwa Spika, naomba sisi tuwe wa kwanza kutenda maono ya Mheshimiwa Rais, tuwe sisi ni wa kwanza kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, iliyosema 2025 Tanzania itakuwa ni Tanzania ya viwanda. Mwaka 2025 Tanzania itakuwa ni Tanzania ya watu wenye kipato cha kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hayawezekani haya kama tusipokuwa wabunifu sisi viongozi na tukawaelekeza wananchi wetu, tukaainisha fursa zilizomo ndani ya maeneo yetu katika kutenda ili kuja kuiona Tanzania ya viwanda na Tanzania ya uchumi wa pato la kati. Haya yanawezekana, mikoa niliyoitaja wameonesha dhamira hii kwa kuanza kutenda, wengine tuige ili tuweze kufanya kazi kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ambayo ningependa kuitolea ufafanuzi, naomba niziseme hizi mbili tu, najua muda sio rafiki, ilikuwa ni Serikali ya Awamu ya Tano kuvunja Katiba na Sheria kwa kukusanya pesa za Mifuko Maalum na kuziingiza kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali bila kuzipeleka kwenye matumizi yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie hili, hakuna Serikali inayoheshimu Katiba, Serikali inayoheshimu sheria zilizotungwa na Bunge lako kama Serikali ya Awamu ya Tano. Nasema haya kwa sababu tunaielewa Katiba, Ibara ya 135 (1) na (2), Ibara ya 136(2), Ibara ya 143(2)(a) na (b) tunaifahamu kama Wizara ya Fedha na tunaifahamu Sheria ya Bajeti iliyotungwa na Bunge lako Tukufu. Hatuko tayari kuvunja Katiba yetu wala kukiuka sheria zilizotungwa.

Mheshimiwa Spika, nasema haya kwa sababu kwanza mapato ya Serikali yako ya aina mbili, hayo yanayokusanywa kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali ambayo yametajwa katika Katiba 135(1) na (2), ambayo hayo yakikusanywa kutoka kwenye *Revenue Collection Account* ya *TRA* moja kwa moja huenda katika Mfuko Mkuu wa Hazina yakisubiri kupangiwa matumizi ili yapelekwe yanakotakiwa. Aina ya pili ni haya yaliyotajwa 135(2) na 136(2) ambayo ni mapato yenye Mifuko Maalum, matumizi yake ni maalum.

Mheshimiwa Spika, naomba kuliambia Bunge lako Tukufu, tunailinda Katiba, tunatekeleza Sheria. Hakuna mapato yoyote kutoka kwenye vyanzo maalum yanayoingia katika Mfuko Mkuu wa Hazina. Mapato haya yakishakusanywa kutoka kwenye *Petroleum Levy Deposit Collection A*ccount yanakwenda moja kwa moja kwenye mifuko husika. Naomba kusema yafuatayo kwa *data* zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, Mfuko wetu wa Nishati Vijijini, mpaka kufikia tarehe 30 Mei, tulishakusanya shilingi bilioni 309.209. Nini tumepeleka kwenye Mfuko wa *REA?* Tumepeleka zaidi ya shilingi milioni 333.528 zaidi ya asilimia 108 ya tulichokikusanya kwenye kipindi hiki cha miezi 11. Kwa nini zimezidi hizi asilimia nane? Zimezidi kwa sababu huwa kuna *lag period.* Zinazokusanywa Juni, huwa zinakwenda kwenye *REA Accoun*t mwezi Julai.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ndiyo maana mnaona hii *8%* inayozidi. Ndiyo maana napenda kuliambia Bunge lako

Tukufu kwamba tuko tayari, tuliapa kuilinda Katiba na kuisimamia Sheria. Hatuko tayari kuvunja Katiba wala Sheria.

Mheshimiwa Spika, huo ulikuwa ni Mfuko wa *REA*. Tukienda kwenye Mfuko wa Barabara, mpaka tarehe 30 Mei, 2018 tumekushanya zaidi ya shilingi milioni 740,655. Nini tumepeleka kwenye Mfuko wa *Road Fund?* Tulichokipeleka ni shilingi milioni 783,141 zaidi ya asilimia 100 imezidi 6%. Kwa hiyo, hakuna sehemu ambako fedha hizi za Mifuko Maalum zinakwenda kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina, hapana. Tutalinda sheria na pia tutaisimamia.

Mheshimiwa Spika, tukienda kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Reli, mpaka tarehe 30 Mei, 2018 tumekusanya shilingi milioni 203,974 na tumepeleka shilingi milioni 221,971 zaidi ya asilimia 109.

*(Hapa kengelei lilia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, najua ni kengele ya pili, yako mengi ya kusema, lakini nataka kusema haya yanayoonesha *image* ya Wizara ya Fedha kwamba tunavunja Katiba na Serikali yetu, nasema hapana, hatuvunji Katiba. Tuko tayari kufanya kazi kwa ubunifu wa hali ya juu, kuhakikisha Taifa hili linasimama kiuchumi, tunafikisha maendeleo kule kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, kile nilichomwambia Mheshimiwa Rais wangu nilipoanza kusema hapa, naomba nimwambie Mheshimiwa Waziri wangu wa Fedha kwamba *Falatutwii-l-mukadhdhibina, waddu Lautudihinu, fayudihinuun.* Wala usigeuke nyuma, utageuka jiwe Mheshimiwa Waziri. Chapa kazi, tuko tayari kukusaidia kufanya kazi yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji kwa maneno yako mazuri na muhimu ya kutia moyo. Tunakushukuru sana kwa jinsi unavyomsaidia Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Sasa ni wakati wa mtoa hoja, Mheshimiwa Dkt. Phillip Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango. Karibu sana sasa uhitimishe hoja yako. Karibu sana, una dakika 40. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa Rehema zake na kuniwezesha kusimama tena mbele ya Bunge lako Tukufu kuhitimisha mjadala wa Hotuba ya Bajeti Kuu ya Mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, siku ya Alhamisi tarehe 14 Juni, 2018 niliwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2017 na Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2018/2019 na pia Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hizo nilieleza mambo mbalimbali yaliyotekelezwa na Serikali kwa kipindi cha mwaka 2017/2018. Matokeo ya utekelezaji, changamoto zilizojitokeza, mambo ya msingi ambayo Serikali inakusudia kutekeleza katika mwaka 2018/2019 na mapendekezo ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, baada ya mawasilisho hayo, Waheshimiwa Wabunge walipata nafasi kwa siku saba; tarehe 18 – 22 na tarehe 25 na leo tarehe 26 Juni, 2018 ya kujadili Hotuba ya Bajeti ya Serikali kwa mujibu wa Kanuni ya 106(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Hivyo napenda kutumia fursa hii kukushukuru kwa dhati kabisa wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuendesha mjadala huu vizuri ambao unatarajiwa kuhitimishwa leo jioni kwa kura.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea zaidi, napenda kutambua michango mizuri iliyotolewa na Kamati ya Kudumu

ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini. Pia Makamu Mwenyekiti, Jitu Soni, Mbunge wa Babati Vijijini.

Mheshimiwa Spika, nakiri kuwa Kamati hii ilihoji mambo mengi na pia kutoa ushauri kuhusu hatua mbadala au maboresho. Mimi na wenzangu katika Wizara ya Fedha na Mipango, tunaahidi kutoa ushirikiano wa hali ya juu kwa Kamati maana tunaamini kwamba Wajumbe wote wa Kamati ya Bajeti wataendelea kuongozwa na maslahi ya Watanzania walio wengi, hasa wanyonge katika kuishauri Serikali. Ahsanteni sana Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuzungumza na kwa maandishi. Jumla ya Wabunge 208 wamechangia hoja niliyowasilisha. Kati ya hao, 180 wamechangia kwa kuzungumza na 28 kwa maandishi. Naomba niseme kwa niaba ya Serikali, ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu mliyoitoa kwenye bajeti hii kwa niaba ya wananchi mnaowawakilisha.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia wananchi wote waliotoa maoni na ushauri juu ya Hotuba ya Bajeti ya Serikali kupitia majukwaa mbalimbali na vyombo vya habari. Napenda kuwahakikishia kuwa Serikali inathamini sana michango hiyo, nami na wataalam wa Wizara ya Fedha na Mipango na taasisi zilizo chini yake tumeyapokea na tumejipanga kuyafanyika kazi mambo yote waliyotushauri kwa maslahi ya Tanzania. Baadhi tutayazingatia katika bajeti hii na mengine katika bajeti zijazo.

Mheshimiwa Spika, naomba niweke wazi kabisa, tumeyapokea pia mawazo ya Wabunge kutoka Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Hata hivyo, napenda nisisitize kuwa tumepokea yale tu yanayoendana na Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025 *(The Tanzania Development Version 2025),* Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano uliopitishwa na Bunge lako Tukufu na Ilani ya CCM kwa ajili ya uchaguzi

Mkuu wa Mwaka 2015 ambayo imebeba ahadi za Chama Tawala kilichochaguliwa na wananchi na kukipa ridhaa ya kuongoza nchi.

Mheshimiwa Spika, nyaraka nilizozitaja ndiyo chimbuko la ajenda za Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wetu wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania. Kamwe hatutasita kumsifia Rais wetu kwa kazi nzuri iliyotukuka anayowafanyia Watanzania wote. Hatuko tayari kuyumbishwa na agenda za kuandikwa. Sisi tunaandika wenyewe na tunatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Tanzania wanayo macho na hawalazimiki kuambiwa tazama. Wale wa Bukoba Mjini wanaona Shule ya Sekondari ya Ihungo iliyojengwa upya baada ya kuharibiwa na tetemeko la ardhi. Wananchi wa Mwanza wanafurahia daraja la waenda kwa miguu la Furahisha na kivuko kipya katika Ziwa Victoria. Wakazi wa Jiji la Arusha wanaona barabara mpya kutoka Arusha mpaka Tengeru ilivyopendezesha Jiji lao. Wananchi wenzangu wa Kigoma wanaona barabara ya Kidahwe hadi Kasulu imeanza kuwekwa lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Dar es Salaam wanaona barabara za juu katika makutano ya *TAZARA* ikielekea kukamilika na bandari ikipanuliwa na kuongezewa kina. Wanaifakara sasa wanavuka mto Kilombero kupitia Daraja la Magufuli kwa usalama. Wananchi wa Mtwara wanaona uwekezaji mkubwa wa upanuzi wa Bandari ya Mtwara.

Mheshimiwa Spika, vilevile, wananchi wa Masasi sasa wataondokana na adha ya ukosefu wa maji, kufuatia ukarabati wa miundombinu ya kusambaza maji na ujenzi wa matenki ya kuhifadhia maji Chiwambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakazi wa Jiji la Dodoma wameikaribisha Serikali na sasa tuko hapa. Wananchi wa

Tanga wanashuhudia kuanza kazi ya ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Hoima, Uganda hadi Chongoleani, Tanga. Upatikanaji wa dawa na vifaa tiba umeongezeka nchi nzima. Watoto wetu kote nchini wanafaidi elimu bila ada na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa yote hayo na mengine mengi, kwa nini tusiisifie Serikali ya CCM na Jemedari wetu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nirejee kwa muhtasari mapendekezo yaliyoungwa Mkondo na wachangiaji wengi. Kwanza, kufuta kodi ongezeko la dhamani kwa taulo za kike; pili, kupunguza kiwango cha kodi ya Mapato ya makampuni kutoka asilimia 30 hadi asilimia 20 kwa wawekezaji wapya wa viwanda vya madawa ya binadamu na viwanda vinavyotengeneza bidhaa za ngozi; na kulinda wawekezaji wa ndani kwa kuongeza ushuru kwenye bidhaa zinazotoka nje ya nchi ambazo zinaweza kuzalishwa na viwanda vya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nne, ni kusamehe *VAT* kwenye vifungasho vya madawa ya binadamu vinavyotengenezwa mahususi kwa ajili ya viwanda vinavyozalisha dawa hapa nchini; na tano, kusamehe *VAT* kwenye virutubisho vinavyotumika kutengeneza vyakula vya mifugo kwa lengo la kupunguza gharama kwa wafugaji na kuhamasisha ufugaji bora.

Mheshimiwa Spika, sita, ni kuanzisha utaratibu maalum wa kusamehe kodi ambao unalenga kusamehe malimbikizo ya nyuma ya riba na adhabu kwa kiwango cha asilimia 100 na pia kuweka msisitizo katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati ikiwemo ujenzi wa reli kwa kiwango *cha standard gauge*, mradi wa kufua umeme Rufiji, mradi wa makaa ya mawe na chuma, Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Spika, pia mradi wa kusindika gesi asilia kuwa kimiminika kule Lindi. Pia kuna shamba la miwa na

shamba la sukari Mkulazi na uendelezaji wa maeneo maalum ya uwekezaji. Hatua zote hizi zililenga kuhamasisha ujenzi wa viwanda hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia niseme kwa kifupi hoja na ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza tulishauriwa kuongeza tozo ya Sh.50/= kwa lita ya dizeli na petrol lakini pia zilitolewa hoja kuhusu pendekezo la Serikali la kuanzisha mfumo wa *stamp* za kodi za kielektroniki kwamba itekelezwe kwa uangalifu. Pia tulishauriwa kwamba Serikali itoe mara moja bakaa ya fedha za ushuru wa korosho zinazosafirishwa nje ya nchi kwa Bodi ya Korosho; nne, kwamba kwenye kuanzishwa kwa akaunti jumuishi ya Hazina tuelezwa kwamba hatua hii ni kinyume cha Katiba ya nchi na vilitajwa vifungu; tano, kuongeza bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa kuzingatia umuhimu wa sekta hii.

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa na hoja kuhusu uhalisia wa bajeti ya Serikali, umuhimu wa kuboresha mazingira ya uwekezaji na kufanya biashara nchini. Vile vile ilitolewa hoja kwamba kasi kubwa ya ukuaji wa uchumi siyo halisia.

Mheshimiwa Spika, ilielezwa kwamba ni muhimu kuboresha mifumo ya ulipaji kodi na kuheshimu sheria zinazosimamia masuala ya ukusanyaji wa kodi, lakini pia ilielezwa kwamba mwenendo wa Sekta ya Fedha hauridhishi; lakini pia kwamba vyanzo vikuu vya mapato ya Halmashauri vinachukuliwa na Serikali Kuu bila kuvirejesha. Lingine ni kwamba Serikali sasa ichukue hatua za madhubuti zaidi kulipa madai mbalimbali na kwamba deni pia la Taifa linakua kwa kasi mno na hivyo lidhibitiwe.

Mheshimiwa Spika, mawazo mengine ni pendekezo la kufuta sheria iliyoanzisha Tume ya Mipango kwamba siyo jambo jema kwa maendeleo ya nchi. Pia kulikuwa na masuala mbalimbali yanayohusu mahusiano ya kiuchumi na

kibiashara kati ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali na Muungano wa Tanzania; na vile vile tulishauria kwamba Serikali iangalie tena baadhi ya hatua mpya za mapato kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, kama ulivyosema mwenyewe, ni wazi kabisa kuwa hoja na michango mbalimbali iliyotolewa kwa siku saba na Waheshimiwa Wabunge haiwezi kufafanuliwa kwa muda wa hizi dakika 40. Hivyo kama ilivyo ada, napenda kuliahidi Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu itatoa ufafanuzi wa kina wa hoja zote na kuziwasilisha kwa maandishi kupitia kwa Katibu wa Bunge kwa ajili ya rejea ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kufafanua vizuri baadhi ya hoja zinazohusu sekta wanazozisimamia.

Mheshimiwa Spika, wakati wote wa mjadala humu Bungeni kuhusu mapendekezo ya Serikali ya Makadirio na Mapato ya Matumizi kwa mwaka ujao wa fedha, Serikali ilisikiliza kwa makini maoni na ushauri kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali sikivu ya CCM ilipokea na kufanyia kazi ushauri wa kizalendo kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na wadau mbalimbali na sasa napenda kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu mapendekezo ya kufanya marekebisho ya baadhi ya kodi na tozo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni Sheria ya Michezo ya Kubahatisha Sura ya 41. Napendekeza kuwianisha viwango na msingi wa ukokotoaji wa kodi ya Michezo ya Kubahatisha hasa inayoshabihiana. Kwanza, kubashiri matokeo (*Sport Betting for land based and on line)*. Pili, ni sehemu ya mashine 40 *(forty machine sites*); ya tatu ni Bahati Nasibu ya *SMS Lottery* na *Casino* za mtandao *(internet casino).*

Mheshimiwa Spika, kiwango cha kodi kinachopendekezwa katika michezo hii inayoshabihiana ni asilimia 25 ya mauzo halisi (*Gross Gaming Revenue - GGRA)* badala ya viwango na wigo uliopo sasa. Pili, kwa michezo ya Bahati Nasibu ya Taifa *(National Lottery)* napendekeza kutoza kodi kwa kiwango cha asilimia 20 kwa mauzo halisi *(GGR)* badala ya asilimia 10 ya mauzo ghafi *(Gross Sales)* inatozwa sasa.

Tatu, ni kuongeza kiwango cha kodi kwenye zawadi ya ushindi (*Gaming Tax on Wining)* kutoka asilimia 18 hadi asilimia 20 kwenye Bahati Nasibu ya *SMS Lottery*. Michezo ya kubashiri matokeo *Sports Betting, Slot Machine Operations,* Bahati Nasibu ya Taifa, sehemu ya mashine 40 na *casino* ya mtandaoni (*internet/online casino)*. Nne, kupunguza kiwango cha kodi, kwenye zawadi ya ushindi yaani *Tax on Winnings* kwa michezo ya *Casino* ya ardhini (*Land Based Casino)* kutoka asilimi 18 hadi asilimia 12 au chini.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo hayo ya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Michezo ya Kubahatisha, yanatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 29.7.

Mheshimiwa Spika, napendekeza pia kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148 ili kwanza kutoa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye mashudu yanayotumika kutengeneza chakula cha mifugo kama ifuatavyo:-

(a) Mashudu ya Soya *HS Code 2304.00.00;*

(b) Mashudu ya Pamba *HS Code 2306.10.00;* na

(c) Mashudu ya Alizeti *HS Code 2306.30.00.*

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kwa kuwawezesha wafugaji kupata chakula cha mifugo kwa bei nafuu zaidi na hivyo kuhamasisha ufugaji bora na kuongeza mchango wa Sekta ya Ufugaji katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, lakini pili, ni vifaa vya kukusanyia kodi *taxi instruments* ambazo ni *stamp* za kodi za kielektroniki *HS Code* 4907.00.90 na pili, ni mashine za kielektroniki za kutolea risiti *(Electronic Fiscal Devices) HS Code* 8470.50.00.

Mheshimiwa Spika, lengo la mapendekezo haya ni kutoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani, kwenye *stamp* za kodi za kieletroniki na mashine za kielektroniki za kutolea risiti ili kuwapatia unafuu wazalishaji wa bidhaa zinazobandikwa *stamp* za kodi za kielektroniki pamoja na kutoa hamasa juu ya matumizi ya mashine za kielektroniki za kutolea risiti. Hatua hizi pia zinatarajiwa pia kuimarisha usimamizi na udhibiti wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo haya ya Sheria za Kodi za Ongezeko la Thamani yatapunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 1.6.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Sheria ya Michezo ya Kubahatisha pamoja na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa ujumla wake yataongeza mapato ya Serikali kwa shilingi bilioni 639.0 hadi shilingi bilioni 646 sawa na ongezeko la shilingi bilioni saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi walichangia hoja kuhusu marekebisho katika Sheria ya Tozo ya Huduma ya Bandari, Sura 264 kwa kurekebisha kifungu cha (3) kinachohusu kuongeza tozo za huduma za bandari kutoka Sh.500/= hadi Sh1,000/= kwa wasafiri ambao ni wakazi nchini na kutoka Dola za Marekani tano (5) hadi 10 kwa wasafiri ambao ni wageni nchini na kuomba kuwa msamaha uendelee kutolewa. Serikali imewasikia na msamaha huo utaendelea kutolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge walizungumzia pia marekebisho katika Sheria ya *VAT* aya ya 22, sehemu ya kwanza ya jedwali, kwa kufuta msahama wa kodi ya ongezeko la thamani kwa ndege ndogo za kukodisha na kuiomba Serikali iendelee kutoa msamaha huo. Nichukue fursa hii kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba Serikali

ya CCM imefanyia kazi hili na sasa msamaha huo utaendelea kutolewa kama kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 75 wa hotuba yangu nilipendekeza kufuta leseni ya kukidhi matakwa ya Sheria ya Afya na Usalama. Napenda kufanya marekebisho eneo hilo lisomeke, "kufuta ada ya leseni ya kukidhi matakwa ya Sheria ya Afya na Usalama."

Mheshimiwa Spika, nirudie tena kusema, Chama cha Mapinduzi kimeielekeza Serikali yake kuwa sikivu na maboresho niliyoyaeleza yanathibitisha hilo. Aidha, tutaendelea kufanyia kazi mapendekezo yote na ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge na wananchi wengine kwa maslahi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwenye baadhi ya hoja na ushauri uliotolewa na Wabunge wengi. Kwanza kulikuwa na hoja kwamba Serikali iongeze tozo ya Sh.50 kwa lita ya mafuta ya *petrol* na *desel* kwa ajili ya Mfuko wa Maji ili kuwe na chanzo kinachotabirika (*ring fence)*.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uwepo wa changamoto ya upatikanaji wa maji katika sehemu mbalimbali nchini, mijini na vijijini. Katika kutatua changamoto hii Serikali imekuwa ikitenga fedha kwenye bajeti kwa ajili ya miradi ya maji. Aidha, baadhi ya miradi iligharamiwa moja kwa moja na wadau wa maendeleo wa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi hizi za Serikali na wadau wa maendeleo, bado maeneo mengi mijini na vijijini yanakabiliwa na uhaba wa maji. Kutokana na hali hii, Waheshimiwa Wabunge walipendekeza kuongeza tozo ya Sh.50/= kwa kila lita moja ya mafuta ya *petrol* na *diesel* kwenye bajeti ya mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Serikali imechambua kwa kina pendekezo hili. Pendekezo hili ni zuri lakini wakati huu sio muafaka kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, tumetazama mwenendo wa matarajio bei ya mafuta kwenye Soko la Dunia na tunaona wazi kabisa kwamba kwa takwimu tulizonazo mwenendo wa bei ya mafuta ulimwenguni inakwenda juu, kwa hiyo, huu siyo wakati muafaka. Tutatoa takwimu kupitia kwenye Ofisi ya Katibu wa Bunge, kuonesha uchambuzi ambao tumefanya.

Mheshimiwa Spika, kutokana na Ripoti ya Hali ya Uchumi wa Dunia (*World Economic Outlook* ya *IMF)* iliyotolewa mwezi Aprili, bei ya mafuta ghafi inatarajiwa kuongezeka hadi kufikia kati ya wastani wa Dola 60 hadi 70 kwa pipa, ikilinganishwa na matarajio ya awali ya Dola za Marekani 50 mpaka 60 kwa pipa kwa mwaka 2018.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2019, bei ya mafuta ghafi inatarajiwa kufikia wastani wa Dola 65.5 kwa pipa na ongezeko hilo linachangiwa na makubaliano ya kupunguza uzalishaji wa mafuta kwa wanachama wa *OPEC* na baadhi ya wazalishaji wasio wanachama wa *OPEC* na hali hii inaweza kusababisha ongezeko la kasi ya mfumuko wa bei, nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kodi na tozo zilizopo kwenye mafuta kwa sasa ni nyingi sana; na bidhaa za mafuta ya *petrol* na *diesel* zina kodi nyingi. Pendekezo lililotolewa na Waheshimiwa Wabunge kama lingekubaliwa, ingekuwa ni mzigo mkubwa sana. Kwanza kuna tozo na kodi kwa ajili ya mamlaka mbalimbali za umma, hizo ziko 11; ziko kodi za Serikali Kuu tatu, ziko kodi na tozo za mauzo ya jumla ya mafuta, ziko mbili; kuna tozo na kodi kwa mauzo ya rejareja ya mafuta, ziko tatu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kodi na tozo hizi, ni wazi kabisa kwamba bidhaa za mafuta ya *petrol* na *diesel* zimebebeshwa mzigo mkubwa sana katika kuchangia maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, baada ya kufanya tathmini, tumeona kwamba tozo hii ingeongeza bei ya

mafuta nchini na kusababisha kupanda kwa *pump prices* ya mafuta ya *diesel* na *petrol*. Tunayo mifano ambayo tumechambua kwa Dar es Salaam, kiasi gani ambacho bei ya mafuta ingeongezeka. Vile vile ingeleta athari kwenye utulivu wa uchumi kwa ujumla *(macroeconomic stability)* na kusababisha bei za bidhaa na huduma ambazo zinazalishwa hapa nchini kuongezeka *(second round effect)*.

Mheshimiwa Spika, wakati wa Hotuba ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji, zilielezwa njia mbadala za Serikali katika kugharamia Miradi ya Maji Nchini. Kwa hiyo, nisingependa kuzirejea, itoshe tu kusema kwamba tumetenga shilingi bilioni 673.2 kwa bajeti ya mwaka ujao wa fedha kugharamia miradi ya maji mijini ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, ahadi ya Serikali ni kwamba tuna dhamira ya dhati ya kupeleka fedha kwenye utekelezaji wa miradi ya maji kama ilivyopitishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya mwaka ujao wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile tumepokea fedha katika mwaka uliokwisha. Tumeshasaini mkataba na Benki ya *Exim* ya India, Mkopo wa Dola za Marekani milioni 500 kwa ajili ya utekekelezaji wa miradi ya maji katika Miji 21, Tanzania Bara na Zanzibar. Pia tumeshakamilisha majadiliano na Benki ya Dunia ambapo Dola za Marekani milioni 350 zinatarajiwa kupatikana na kati ya kiasi hicho Dola za Marekani 60 sawa na asilimia 17 kitatolewa mwezi Julai, 2018.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja juu ya pendekezo la Serikali la kuanzisha mfumo wa *stamp* za kodi za kielektroniki. Serikali ilishauriwa itengeneze yenyewe mfumo wa *ETS ili* kiasi cha fedha ambacho kitalipwa kampuni ya *CIPA* iwe ni sehemu ya mapato ya Serikali, badala ya mapato yatokanayo na *stamp* ya kuchukuliwa na Kampuni Binafsi.

Mheshimiwa Spika, tumelichambua sana hili, niseme tu kwamba teknolojia ya kutengeneza mfumo huu ni mpya

hapa nchini na hivyo hapakuwa na kampuni au taasisi ya Serikali iliyokuwa na uwezo wa kutengeneza mfumo huo. Kutokana na hilo, ililazimu Serikali itangaze Zabuni ya Kimataifa kwa uwazi na ndipo tulipompata Mzabuni mwenye uwezo na uzoefu wa kutengeneza mfumo huu kati ya Makampuni tisa yaliyojitokeza na hapakuwepo Kampuni ya ndani iliyojitokeza.

Mheshimiwa Spika, pia uwekezaji wa mradi huu ni zaidi ya mwaka mmoja na hivyo gharama za mradi zimezingatia muda huo ili kufidia gharama ya uwekezaji. Mapato yatokanayo na *stamp* za kodi kwa muda wa mwaka mmoja hayawezi kulingana na gharama za uwekezaji wa mradi huo katika mwaka wa kwanza.

Mheshimiwa Spika, vilevile mfumo huo utakapokamilika kujengwa, utaanza kuunganishwa kwenye viwanda vya uzalishaji kwa awamu kulingana na uhatarishi wa upotevu wa mapato katika bidhaa husika.

Mheshimiwa Spika, napenda niseme tu kwamba mfumo huu una faida nyingi sana ambazo zinazidi hizo gharama ambazo ilikuwa ni wasiwasi wa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, niseme kuhusu ushuru wa korosho zinazosafirishwa nje ya nchi na matumizi yake. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Waziri wa Kilimo walifafanua jambo hili kwa ufasaha jana na nisingependa kurudia. Ni vyema niseme na Watanzania wasikie na ikae kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge lako Tukufu. Mimi Phillip Mpango siwezi kamwe kuwahujumu wananchi, wakulima wa korosho wa Mikoa ya Mtwara na Lindi au mkoa mwingine wo wote ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwahikikishie Watanzania kuwa Mtwara na Lindi nitakwenda, iwe katika kutelekeza majukumu yangu ya kikazi au kuwatembelea ndugu na marafiki. Hakuna anayeweza kunizuia, ni haki yangu na uhuru

wangu kama Mtanzania ambayo haiwezi kupokonywa kwa vitisho. Hata ikibidi kufa katika kutumikia Taifa na iwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika nafasi mbalimbali nilizotumikia Serikali ya CCM na Taifa hili kwa ujumla, nimetumia uwezo wangu wote kuwatumikia Watanzania wa mikoa yote, nimefundisha wanafunzi wakiwa ni pamoja na wanaotoka Mikoa ya Kusini, nilipokuwa Mhadhiri Chuo Kikuu cha Dar es Dar es Salaam bila upendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, kati ya mambo niliyofanya nikiwa Mshauri wa Rais, Uchumi katika Serikali ya Awamu ya Nne na nilipokuwa Mkuu wa Tume ya Mipango, nilikuwa mstari wa mbele kuishawishi Serikali kuifanya Mtwara iwe kitovu cha ukuaji wa uchumi hapa nchini (Mtwara *Growth Pole)* na kuingiza miradi mikubwa ya maendeleo, kwa mfano upanuzi wa Bandari ya Mtwara, *LNG Plant* Lindi, Barabara za uchumi na kadhalika katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

Mheshiomiwa Spika, mimi na wenzangu tuliishauri Serikali kutenga nafasi za upendeleo kwa vijana kutoka Mikoa ya Kusini kusoma masomo ya sayansi ili baadaye waweze kufanya kazi katika viwanda vinavyohusiana na Sekta ya Gesi Asilia; niliapa kuilinda na kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayotaka pamoja na mambo mengine kuhakikisha maendeleo ya Uchumi wa Taifa yanakuzwa na kupangwa kwa uangalifu na kwa pamoja ambayo iko kwenye Ibara ya 9 (d). Iweje leo niwahujumu wananchi wa Mtwara na Lindi?

Mheshimiwa Spika, kama yupo mtu ana chuki binafsi na Phillip Mpango, pasipo chembe ya ukweli, mimi namwombea msamaha kwa Mungu. Nasema tena, sitayumba katika kusimamia matumizi bora ya fedha za umma kwa mujibu wa sheria. Nawakumbusha wabadhirifu wa fedha za umma, wajue wanakula sumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najua muda siyo rafiki, nilitarajia ningesema sana leo, lakini naomba niseme jambo moja kabla sijaenda kwenye kuhitimisha. Kulikuwa na hoja kuhusu mapendekezo ya Serikali ya kufuta sheria iliyoanzisha Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Spika, nilieleza katika hotuba niliyowasilisha tarehe 14 Juni, kwamba mapendekezo hayo ni mabadiliko ya kimuundo na siyo kufuta kazi muhimu za kupanga mipango ya maendeleo ya Taifa letu kwa kipindi cha muda wa kati na muda mrefu. Ukifuatilia historia ya muundo ya Taasisi ya Tume ya Mipango, iko wazi kuwa imekuwa inahama, kwa nyakati tofauti toka tulipopata Uhuru, Taasisi hiyo kuna kipindi ilikuwa peke yake kama Wizara kamili au Tume na wakati mwingine ikawa sehemu ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, tena jambo hili siyo kwa Tanzania pekee, hata katika nchi jirani za Uganda na Rwanda hivi sasa, fedha na mipango vinaunda Wizara moja *(Ministry of Finance and Economical Planning).* Lengo kuu ni kuwianisha Mipango ya Maendeleo ya Taifa na ugawaji wa rasilimali fedha, jambo ambalo ni gumu pale ambapo Taasisi hizi zinapokuwa zimetenganishwa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza, kazi ya kuandaa na kusimamia mipango ya maendeleo ya Taifa ndani ya Wizara ya Fedha na Mipango, itaongozwa na Kamishna atakayekuwa na fungu lake kuwezesha utekelezaji wa kazi za idara hiyo. Kazi hizo zimeendelea kufanyika vizuri baada ya kuhamisha wataalam wa iliyokuwa Tume ya Mipango ndani ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, naomba kuhitimisha. Kama nilivyoeleza katika hotuba yangu, hatua zilizopendekezwa kwenye Bajeti hii zinalenga kujenga msingi madhubuti wa uchumi wa viwanda na kupanua fursa za ajira na biashara. Dhamira yetu sote ni kufikia kiwango cha uchumi wa kipato cha kati itakapofika mwaka 2025. Ili kushiriki katika mafanikio

hayo, ni lazima kila mmoja wetu ashiriki katika shughuli halali za kuzalisha na afanye hivyo kwa juhudi na maarifa ili kuleta tija.

Mheshimiwa Spika, kufanikiwa kwa Bajeti hii kunahitaji nidhamu ya hali ya juu katika usimamizi wa mapato na matumizi. Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere alituusia, nitasema kwa Kiingereza; mwanzo wa kunukuu: "*our watch word must be frugality, this must run through the whole expenditure.*" Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, hii inatoka kitabu cha *Freedom and Socialism.* Ili kufikia azma hii, juhudi za pamoja kati ya Serikali na wadau wote zinahitajika ikiwa ni pamoja na kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika uchumi kwa kuwekeza zaidi katika maeneo ya kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najua Watanzania tuna kiu kubwa ya kuendelea, tena haraka, lakini tukumbuke kuwa kila safari inaanza na hatua moja ikifuatiwa na nyingine. Vile vile njia ya maendeleo ina vikwazo vingi na haiwezekani kutatua changamoto zote za nchi hii kwa mara moja.

Mheshimiwa Spika, hata nchi zilizoendelea kama Marekani na Uingereza na kadhalika bado wanazo changamoto, bado nao wanajenga barabara, reli, hospitali na kadhalika. Hivyo ni muhimu Watanzania tuendelee kufanya kazi kwa juhudi na maarifa na kudumisha amani na umoja wa Taifa letu. Changamoto zitaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, mjadala wetu wa siku saba umeyatendea haki mapendekezo ya Bajeti niliyowasilisha tarehe 14 Juni, 2017. Kukosoa kwa haki ili kujenga *(constructive criticism)* na kujikosoa ni sehemu muhimu sana katika harakati za maendeleo ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa jambo kubwa la Kitaifa kama hili la Bajeti ya Serikali, ningestaajabu sana kama kila Mbunge

angesimama na kusifia tu mapendekezo niliyowasilisha. Ndiyo maana mwanzo kabisa mwa Hotuba ya Bajeti Kuu nilibainisha kwa makusudi changamoto kubwa zinazotukabili kama Taifa na kwa ukweli, ili tujielekeze kwa pamoja katika kuzitatua.

Mheshimiwa Spika, imani yangu ni kuwa lazima tuwe wa kweli sisi wenyewe na kwa Taifa letu, lakini ni muhimu pia tuishi katika dunia, tusiishi katika dunia ya kufikirika. Kwa Kiingereza, *we have to be honest ourselves, honest to our country and be as pragmatic as possible. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatukuandaa bajeti hii kujifurahisha. Tumekuwa wakweli katika kutathmini utekelezaji wa Bajeti 2017/2018, tuliyoifanya. Katika mapendekezo tuliyoleta hapa Bungeni juu ya hatua ambazo tunaamini kwa dhati zitatupeleka mbele kama Taifa. Ukweli ni kwamba ni rahisi sana kusema, rahisi sana kwa rafiki zangu wa upande wa pili kukosoa, lakini nao wanajua kuwa ni vigumu kutenda, ndiyo maana hata walichokisema ni Bajeti Mbadala waliandikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalize kwa kumshukuru tena Mwenyezi Mungu kwa rehema zake. Namshukuru sana Naibu wa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, wewe mama ni mahiri kweli kweli, umekuwa ni msaada mkubwa sana. Namshukuru sana Katibu Mkuu na Wataalam wote wa Wizara ya Fedha kwa kuendelea kufanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge wote kuunga mkono Bajeti hii ya Serikali kwa mwaka 2018/2019 ikiwa ni hatua nyingine thabiti ya Kujenga Uchumi wa Viwanda Nchini Tanzania na kuboresha maisha ya wananchi wetu. Natanguliza ahsante kwa kura yenu ya 'Ndiyooo!'

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango. Ahsante sana Mheshimiwa, tunakushukuru sana kwa kuhitimisha hoja yako.

Waheshimiwa Wabunge, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, haikuwa rahisi kwake kugusa kila hoja ambayo ilizungumzwa huku ndani kwa dakika ambazo tulikuwa tumempa. Ametuahidi kwamba watapitia hotuba zetu na watatengeneza majibu ambayo yatapita hapa Mezani na tutapeana majibu hayo katika utaratibu wetu wa kawaida kwa wakati muafaka kupitia *pigeon holes* zetu.

Tunakushukuru tena Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango na Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Ashatu Kijaji kwa majibu yenu kwetu ambayo kwa kweli yanatia moyo kwa kiwango kikubwa. *(Makofi)*

Moja ya mambo ambayo ameyasema hapa ni kufuta kodi kwenye mashudu. Najua au nahisi kuwa ziko baadhi ya Halmashauri nazo zina vikodi kodi huko, sasa ni vizuri nazo huko mbele zikajiangalia ili ziendane na *sprit* hii ya Serikali. Ni mpango ambao unaenda kuboresha sana habari ya ufugaji wa mifugo na kukuza masuala ya ufugaji bora katika nchi yetu. *(Makofi)*

Nina matangazo mawili madogo. La kwanza kama nilivyosema kabla, Wajumbe wa Kamati ya Bajeti mtaenda katika ukumbi wenu wa kawaida ili muweze kupitia lile pendekezo la Muswada wa Sheria ya Fedha. Mheshimiwa Waziri na Naibu na Wataalamu wao wataelekea huko mara tukitoka hapa.

La pili, ni kwamba Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Peter Serukamba, anawaomba Wajumbe wote wa Kamati hiyo mkutane kwenye ukumbi ambao kwa kawaida huwa mnakutana, mara tu baada ya mambo haya ili muweze kukutana na ndugu zetu wa *TCRA*,

kuna mambo ya kuelimishana na ni muhimu sana kufanya hivyo leo. *(Makofi)*

Narudia tena Kamati ya Huduma, ambayo Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Peter Serukamba, anawaomba Wajumbe wote mkutane katika ukumbi wenu wa kawaida, mkutane na *TCRA*.

Mwisho, Waheshimiwa Wabunge, tukutane tena saa 11.00 kwa kazi kubwa maalum na sisi tutakuwa tumeshaandaa mambo yetu hapa. Naomba tuwahi, kwa sababu mara tu mkifika, zoezi lile muhimu litaanza ili tuweze kufanya maamuzi kuhusiana na shughuli nzima hii tuliyoianza mwezi Aprili yote, Mei yote na Juni karibu yote. Kwa maana hiyo,tutakuwa tumetekeleza wajibu wetu kama WaheshimiwaWabunge, tukifanya hivyo.

Baada ya hapo basi, niseme tu kwamba naahirisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 juu ya alama. Ahsante sana.

*(Saa 11.00 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Aah, leo *full House!* Waheshimiwa Wabunge, tukae. *(Kicheko)*

Ngoja tutoe nafasi ya Waheshimiwa Wabunge wanaoingia waweze kuingia, halafu tuelezane mambo yanayohusu taratibu.

Sasa namwomba *Sergeant-at-Arms,* igongwe kengele ili kuwahimiza Waheshimiwa Wabunge ambao wako sehemu nyingine za jengo hili au walioko njiani waweze kujiunga nasi ili tuweze kuanza zoezi lililo mbele yetu. Kwa hiyo, naomba kengele igongwe kufuatana na kanuni inavyotaka.

*(Hapa kengele iligongwa ili kuruhusu Waheshimiwa Wabunge kuingia ndani ya ukumbi)*

Kwa kweli mahudhurio ya leo ni mazuri. Naona hata Mheshimiwa Silinde naye amerudi, maana yake alikuwa haonekani. Sasa kesho tuna Muswada wa Fedha, usije ukasema tena maoni yako hayajaingizwa kwenye *Order Paper* na lawama nyingi. Kama wameshakuandikia, basi tuletee mapema ili... *(Kicheko/Makofi)*

Bunge hili ni zuri kweli, ndiyo maana mtu akitoka Bungeni ana-*miss.* Lina mambo yake na vionjo vyake. *(Kicheko)*

Basi Waheshimiwa Wabunge, natumaini tunaweza tukaanza sasa. Nawaomba sana katika zoezi linalokuja, basi wale wanaotembea tembea, au wale wanaokaa maeneo sio yao, hebu tupunguze hilo ili zoezi letu liweze kwenda vizuri. Naona wenzetu wengine bado wanazidi kuingia, karibuni sana. Naona bado kuna haja ya kuvuta muda kidogo. Nadhani tunaweza tukaendelea sasa.

Waheshimiwa Wabunge, nina maelezo mafupi kwenu na naomba tusikilizane kidogo ili twende pamoja. Kwa kuwa tumehitimisha mjadala wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa Fedha wa 2018/2019 na Mtoa hoja akaja kuhitimisha hoja yake hapa, tunatakiwa sasa katika hatua hii kufanya maamuzi kwa kuyapitisha au kutokuyapitisha makadirio hayo.

Kanuni ya 107(2) inaeleza kuhusu utaratibu wa kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Serikali na inasomeka kama ifuatavyo:

*“Uamuzi wa Bunge wa kupitisha au kutokupitisha Bajeti ya Serikali utafanywa kwa kupiga kura ya wazi, kwa kutaja jina la Mbunge mmoja mmoja.”*

Ibara ya 94(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kanuni ya 77(1) ya Kanuni za Bunge, pamoja na mambo mengine zinaelekeza kwamba Akidi ya Kikao cha

Bunge wakati wa kufanya maamuzi ni nusu ya Wabunge wote.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa idadi ya Wabunge wote ni 393, ukiondoa mwenzetu mmoja kama mnavyokumbuka, kwa hiyo, sasa hivi idadi ya Wabunge wote ni 392. Hivyo, kabla ya kuanza zoezi la kupiga kura, tunatakiwa kuwa na Wabunge wasiopungua 196 humu ndani.

Katibu wa Bunge atatumia utaratibu unaofaa kutuhakikishia kama tunazidi idadi ya 196. Katibu atafanya hivyo kwa utaratibu wa kuhesabu au atakavyoona inafaa, lakini mwisho atatujulisha.

Kanuni ya 79(1) inafafanua kuwa, mambo yote yanayohitaji kuamuliwa na Bunge, yataamuliwa kwa kufuata maoni ya Wabunge walio wengi, waliohudhuria na kupiga kura Bungeni. Hivyo katika zoezi letu la leo tutafuata utaratibu ufuatao:-

Kwanza, kengele itapigwa kama nilivyoelekeza ili Waheshimiwa Wabunge walio nje ya ukumbi waingie ndani. Pili, Katibu atawahesabu Wabunge wote ili kuona kama akidi inatimia, kwa maana ya kwamba tunafikia na kuzidi 196.

Tatu, zoezi la kupiga kura litaanza ambapo Katibu atasoma majina ya Wabunge mmoja baada ya mwingine na kila anayeitwa, atatoa uamuzi wake kwa kusema ‘Ndiyo’ au ‘Hapana.’

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapo, tutapatiwa matokeo ya kura kuhusiana na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa Fedha wa 2018/2019.

Waheshimiwa Wabunge, sasa namkaribisha Katibu wa Bunge ili atupatie idadi yetu tuweze kuendelea na zoezi hili baada ya hapo. Katibu.

**NDG. STEVEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, idadi kamili ya Wabunge waliopo ndani ya Ukumbi wa Bunge kwa sasa ni 303 na inawezekana ikaongezeka kwa kuwa baadhi ya Wabunge bado wanaendelea kuingia.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa idadi hiyo inatosha kuendelea na zoezi la kupiga kura, naomba uridhie tuendelee na hatua inayofuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa orodha iliyoandaliwa kwa madhumuni ya kupiga kura hii ya Bajeti, tutaanza kuita majina ya viongozi waliomo humu ndani, Mawaziri, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge na kufuatiwa na Wabunge wengine wote.

Mheshimiwa Spika, tunaomba kila Mbunge anayeitwa asiwe na maneno mengine zaidi ya kujibu 'Ndiyo' au 'Hapana' kwa sababu hizo ndizo tu zinazotakiwa kurekodiwa.

Mheshimiwa Spika, sasa tutaanza kuita majina kama ifuatavyo:-

**SPIKA:** Mpaka hapo kabla ya Katibu hajaanza, kuna neno? Hakuna.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tunaanza shughuli. Katibu sasa anza.

**NDG. NENELWA WANKANGA - KATIBU MEZANI:**

| | |
|---|---|
| Mhe. Dkt. Tulia Ackson | - Ndiyo |
| Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa | - Ndiyo |
| Mhe. Freeman Aikaeli Mbowe | - Hakuwepo |
| Mhe. Mussa Azzan Zungu | - Ndiyo |
| Mhe. Andrew John Chenge | - Ndiyo |
| Mhe. Najma Murtaza Giga | - Ndiyo |

| | |
|---|---|
| Mhe. Dkt. Adelardus Lubango Kilangi | - Ndiyo |
| Mhe. Capt. Mst. George Huruma Mkuchika | - Ndiyo |
| Mhe. Selemani Saidi Jafo | - Ndiyo |
| Mhe. January Yusuf Makamba | - Ndiyo |
| Mhe. Jenista Joakim Mhagama | - Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba | - Ndiyo |
| Mhe. William Vangimembe Lukuvi | - Ndiyo |
| Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa | - Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi | - Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Harrison George Mwakyembe | - Ndiyo |
| Mhe. Angellah Jasmine Kairuki | - Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Charles John Tizeba | - Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango | - Ndiyo |
| Mhe. Balozi Dkt. Augustine Philip Mahiga | - Hakuwepo |
| Mhe. Charles John Mwijage | - Ndiyo |
| Mhe. Prof. Joyce Lazaro Ndalichako | - Ndiyo |
| Mhe. Ummy Ally Mwalimu | - Ndiyo |
| Mhe. Prof. Paramagamba John Kabudi | - Hakuwepo |
| Mhe. Luhaga Joelson Mpina | - Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Medard Matogoro Kalemani | - Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla | - Ndiyo |
| Mhe. Eng. Isack Aloyce Kamwelwe | - Ndiyo |
| Mhe. Joseph Sinkamba Kandege | - Ndiyo |
| Mhe. Joseph George Kakunda | - Ndiyo |
| Mhe. Kangi Alphaxard Lugola | - Ndiyo |
| Mhe. Antony Peter Mavunde | - Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa | - Ndiyo |
| Mhe. William Tate Ole Nasha | - Ndiyo |
| Mhe. Abdallah Hamis Ulega | - Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji | - Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Susan Alphonce Kolimba | - Ndiyo |
| Mhe. Angeline Sylvester Mabula | - Ndiyo |
| Mhe. Elias John Kwandikwa | - Ndiyo |
| Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya | - Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile | - Ndiyo |
| Mhe. Eng. Hamad Yussuf Masauni | - Ndiyo |
| Mhe. Eng. Atashasta Justus Nditiye | - Ndiyo |
| Mhe. Subira Khamis Mgalu | - Ndiyo |
| Mhe. Japhet Ngailonga Hasunga | - Ndiyo |
| Mhe. Jumaa Hamidu Aweso | - Ndiyo |

| | |
|---|---|
| Mhe. Juliana Daniel Shonza | - Ndiyo |
| Mhe. Stella Ikupa Alex | - Ndiyo |
| Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo | - Ndiyo |
| Mhe. Doto Mashaka Biteko | - Ndiyo |
| Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa | - Ndiyo |
| Mhe. Jasson Samson Rweikiza | - Ndiyo |
| Mhe. Peter Joseph Serukamba | - Ndiyo |
| Mhe. Vedasto Edgar Ngombale | - Hapana |
| Mhe. Dkt. Raphael Masunga Chegeni | - Ndiyo |
| Mhe. Moshi Selemani Kakoso | - Ndiyo |
| Mhe. Dunstan Luka Kitandula | - Ndiyo |
| Mhe. Emanuel Adamson Mwakasaka | - Ndiyo |
| Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka | - Hakuwepo |
| Mhe. Suleiman Ahmed Saddiq | - Ndiyo |
| Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa | - Ndiyo |
| Mhe. Nape Moses Nnauye | - Ndiyo |
| Mhe. Abdallah Dadi Chikota | - Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma | - Ndiyo |
| Mhe. Kemilembe Julius Lwota | - Ndiyo |
| Mhe. Mwanne Ismail Mchemba | - Ndiyo |
| Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri | - Ndiyo |
| Mhe. William Mganga Ngeleja | - Ndiyo |
| Mhe. Juma Selemani Nkamia | - Ndiyo |
| Mhe. Salum Mwinyi Rehani | - Ndiyo |
| Mhe. Zaynabu Matitu Vulu | - Ndiyo |
| Mhe. Khalfan Hilaly Aeshi | - Ndiyo |
| Mhe. Innocent Lugha Bashungwa | - Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Jasmine Tisekwa Bunga | - Ndiyo |
| Mhe. Hawa Mchafu Chakoma | - Ndiyo |
| Mhe. Raphael Japhary Michael | - Hapana |
| Mhe. Ruth Hiyob Mollel | - Hapana |
| Mhe. Ally Saleh Ally | - Hapana |
| Mhe. Ester Amos Bulaya | - Hakuwepo |
| Mhe. Halima James Mdee | - Hakuwepo |
| Mhe. James Francis Mbatia | - Hapana |
| Mhe. John John Mnyika | - Hakuwepo |
| Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa | - Hakuwepo |
| Mhe. Juma Hamad Omar | - Hakuwepo |
| Mhe. Godbless Jonathan Lema | - Hakuwepo |
| Mhe. Wilfred Muganyizi Lwakatare | - Hapana |

Mhe. Esther Nicholas Matiko - Hakuwepo
Mhe. Antony Calist Komu - Hapana
Mhe. Susan Anselm Jerome Lyimo - Hapana
Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi - Hapana
Mhe. Hamidu Hassan Bobali - Hapana
Mhe. Tundu Antiphas Mughwai Lissu - Hakuwepo
Mhe. Joseph Michael Mkundi - Hapana
Mhe. Pauline Philipo Gekul - Hapana
Mhe. Yussuf Kaiza Makame - Hapana
Mhe. David Ernest Silinde - Hapana
Mhe. Qambalo Willy Qulwi - Hapana
Mhe. John Wegesa Heche - Hakuwepo
Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi - Hapana
Mhe. Mwita Mwikabe Waitara - Hapana
Mhe. Masoud Abdallah Salim - Hapana
Mhe. Cecilia Daniel Paresso - Hapana
Mhe. Cecil David Mwambe - Hapana
Mhe. Dkt. Suleiman Ally Yussuf - Hapana
Mhe. Zubeda Hassan Sakuru - Hakuwepo
Mhe. Devotha Mathew Minja - Hapana
Mhe. Peter Ambrose Paciens Lijualikali - Hapana
Mhe. Abdallah Ally Mtolea - Hapana
Mhe. Rashid Ali Abdallah - Hapana
Mhe. Maida Hamad Abdallah - Ndiyo
Mhe. Hamida Mohamed Abdallah - Ndiyo
Mhe. Munde Tambwe Abdallah - Hakuwepo
Mhe. Bahati Ali Abeid -Ndiyo
Mhe. Abdul-Aziz Mohamed Abood - Hakuwepo
Mhe. Khadija Hassan Aboud -Ndiyo
Mhe. Lameck Okambo Airo - Hakuwepo
Mhe. Ajali Rashid Akbar - Hakuwepo
Mhe. Abdallah Haji Ally - Hapana
Mhe. Jamal Kassim Ali - Hakuwepo
Mhe. Khadija Nassir Ali -Ndiyo
Mhe. Khamis Mtumwa Ali -Ndiyo
Mhe. Mbarouk Salim Ali - Hapana
Mhe. Hussein Nassor Amar -Ndiyo
Mhe. Wanu Hafidh Ameir -Ndiyo
Mhe. Zainab Mndolwa Amir -Ndiyo *(Makofi/ Vigelegele)*

**MBUNGE FULANI:** Uzalendo, uzalendo.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliongea bila utaratibu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, *order, order*!

**NDG. NENELWA WANKANGA- KATIBU MEZANI:**

Mhe. Ussi Salum Pondeza -Ndiyo
Mhe. Saul Henry Amon -Ndiyo
Mhe. Jaku Hashim Ayoub -Ndiyo
Mhe. Omary Ahmad Badwel -Ndiyo
Mhe. Nuru Awadh Bafadhil -Ndiyo *(Makofi/ Vigelegele)*

Mhe. Faida Mohamed Bakar -Ndiyo
Mhe. Zainab Mussa Bakar -Hakuwepo
Mhe. Hussein Mohamed Bashe -Ndiyo
Mhe. Mbaraka Salim Bawazir -Ndiyo
Mhe. Innocent Sebba Bilakwate -Ndiyo
Mhe. Lolesia Jeremia Bukwimba -Hakuwepo
Mhe. Abdallah Majura Bulembo -Ndiyo
Mhe. Halima Abdallah Bulembo -Ndiyo
Mhe. Selemani Said Bungara -Hapana
Mhe. Felister Aloyce Bura -Ndiyo
Mhe. Jerome Dismas Bwanausi -Ndiyo
Mhe. Marwa Ryoba Chacha -Hapana
Mhe. Josephine Tabitha Chagula -Ndiyo
Mhe. Lathifah Hassan Chande -Hapana
Mhe. Mary Pius Chatanda -Ndiyo
Mhe. Sikudhani Yassini Chikambo -Ndiyo
Mhe. Dkt. Rashid Mohamed Chuachua - Ndiyo
Mhe. Cosato David Chumi - Ndiyo
Mhe. Mbaraka Kitwana Dau - Ndiyo
Mhe. Dkt. David Mathayo David - Ndiyo
Mhe. Makame Mashaka Foum - Ndiyo
Mhe. Tauhida Cassian Galoss Nyimbo -Ndiyo
Mhe. Alex Raphael Gashaza - Ndiyo
Mhe. Josephine Johnson Genzabuke - Ndiyo

Mhe. Boniphace Mwita Getere - Ndiyo
Mhe. Anna Joram Gidarya - Hapana
Mhe. Seif Khamis Said Gulamali -Ndiyo
Mhe. Haji Ameir Haji -Hakuwepo
Mhe. Mwantumu Dau Haji -Ndiyo
Mhe. Othman Omar Haji - Hapana
Mhe. Khatibu Said Haji - Hapana
Mhe. Azza Hillal Hamad - Ndiyo
Mhe. Juma Kombo Hamad - Hapana
Mhe. Pascal Yohana Haonga -Hapana
Mhe. Joseph Leonard Haule - Hapana
Mhe. Juma Othman Hija - Ndiyo
Mhe. Mansoor Shanif Hiran - Ndiyo
Mhe. Augustine Vuma Holle - Ndiyo
Mhe. Joram Ismael Hongoli - Ndiyo
Mhe. Yusuph Salim Hussein - Hapana
Mhe. Khalifa Mohamed Issa - Hapana
Mhe. Zacharia Paulo Issaay - Ndiyo
Mhe. Asha Mshimba Jecha - Ndiyo
Mhe. Emmanuel Papian John - Hakuwepo
Mhe. Asha Abdallah Juma - Ndiyo
Mhe. Juma Ali Juma - Ndiyo
Mhe. Mwantakaje Haji Juma - Ndiyo
Mhe. Hamoud Abuu Jumaa - Hakuwepo
Mhe. Jafar Sanya Jussa - Ndiyo
Mhe. Ritta Esnepher Kabati - Ndiyo
Mhe. Risala Saidi Kabongo - Hapana
Mhe. Mgeni Jadi Kadika - Hapana
Mhe. John Peter Kadutu - Ndiyo
Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu - Ndiyo
Mhe. Alfredina Apolinary Kahigi - Ndiyo *(Makofi/ Vigelegele)*

Mhe. Haji Khatib Kai - Hapana
Mhe. Bonnah Moses Kaluwa - Ndiyo
Mhe. Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala -Ndiyo
Mhe. Vicky Paschal Kamata - Ndiyo
Mhe. Maria Ndila Kangoye - Ndiyo
Mhe. Costantine John Kanyasu - Ndiyo
Mhe. Sebastian Simon Kapufi - Ndiyo

Mhe. Rukia Ahmad Kassim - Ndiyo *(Makofi/ Vigelegele)*

Mhe. Katani Ahmad Katani - Hapana
Mhe. Zainab Athuman Katimba - Ndiyo
Mhe. Hassan Selemani Kaunje - Hakuwepo
Mhe. Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa - Ndiyo
Mhe. Kanali Mst. Masoud Ali Khamis - Ndiyo
Mhe. Yussuf Haji Khamis - Hapana
Mhe. Sadifa Juma Khamis - Ndiyo
Mhe. Ali Salim Khamis - Hapana
Mhe. Fakharia Shomari Khamis - Ndiyo
Mhe. Mohamed Juma Khatib - Hapana
Mhe. Munira Mustapha Khatibu - Ndiyo
Mhe. Aida Joseph Khenani - Hapana
Mhe. Omari Abdallah Kigoda - Ndiyo
Mhe. Mendrad Lutengano Kigola - Ndiyo
Mhe. Omari Mohamed Kigua - Ndiyo
Mhe. Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe- Ndiyo
Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete - Ndiyo
Mhe. Salma Rashid Kikwete - Hakuwepo
Mhe. Ali Hassan Omar King - Ndiyo
Mhe. Elibariki Emmanuel Kingu - Ndiyo
Mhe. Dkt. Stephen Lemomo Kiruswa - Ndiyo
Mhe. Mariam Nassoro Kisangi - Ndiyo
Mhe. Jumanne Kibera Kishimba - Ndiyo
Mhe. Jesca David Kishoa - Hapana
Mhe. Boniventura Destery Kiswaga - Ndiyo
Mhe. Charles Muhangwa Kitwanga - Ndiyo
Mhe. Allan Joseph Kiula - Ndiyo
Mhe. Suzan Limbweni Kiwanga - Hapana
Mhe. Grace Sindato Kiwelu - Hapana
Mhe. Silvestry Francis Koka - Ndiyo
Mhe. Leah Jeremiah Komanya - Ndiyo
Mhe. Yosepher Ferdinand Komba - Hapana
Mhe. Kiteto Zawadi Koshuma - Ndiyo
Mhe. Saed Ahmed Kubenea - Hapana
Mhe. Zuberi Mohamed Kuchauka - Hapana
Mhe. Rhoda Edward Kunchela - Hapana
Mhe. Julius Karanga Laizer - Hapana

Mhe. George Malima Lubeleje – Ndiyo
Mhe. Riziki Said Lulida – Hakuwepo
Mhe. Anna Richard Lupembe – Ndiyo
Mhe. Livingstone Joseph Lusinde – Ndiyo
Mhe. Eng. Gerson Hosea Lwenge - Ndiyo
Mhe. Hamad Salim Maalim – Hapana
Mhe. Amina Iddi Mabrouk – Ndiyo
Mhe. Stanslaus Shing'oma Mabula – Ndiyo
Mhe. Khamis Yahaya Machano – Hakuwepo
Mhe. Lucy Simon Magereli – Hapana
Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe - Ndiyo
Mhe. Catherine Valentine Magige – Ndiyo
Mhe. Sonia Jumaa Magogo - Hakuwepo
Mhe. Esther Alexander Mahawe – Ndiyo
Mhe. Almas Athuman Maige – Ndiyo
Mhe. Ezekiel Magolyo Maige - Ndiyo
Mhe. Kunti Yusuph Majala – Hapana
Mhe. Salome Wycliffe Makamba – Hapana
Mhe. Makame Kassim Makame – Ndiyo
Mhe. Eng. Ramo Matala Makani - Ndiyo
Mhe. Joel Mwaka Makanyaga – Ndiyo
Mhe. Amina Nassoro Makilagi – Ndiyo
Mhe. Hussein Ibrahim Makungu – Ndiyo
Mhe. Tunza Issa Malapo – Hapana
Mhe. Anne Kilango Malecela – Hakuwepo
Mhe. Angelina Adam Malembeka – Ndiyo
Mhe. Ignas Aloyce Malocha – Ndiyo
Mhe. Issa Ali Mangungu - Ndiyo
Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi - Ndiyo
Mhe. Sixtus Raphael Mapunda – Ndiyo
Mhe. Agness Mathew Marwa – Ndiyo
Mhe. Gimbi Dotto Masaba - Hapana
Mhe. Hassan Elias Masala – Ndiyo
Mhe. Stephen Julius Masele – Hayupo
Mhe. Augustino Manyanda Masele – Ndiyo
Mhe. Susanne Peter Maselle – Hapana
Mhe. Yahaya Omary Massare – Ndiyo
Mhe. Janeth Maurice Masaburi - Ndiyo
Mhe. Flatei Gregory Massay – Ndiyo
Mhe. Aisharose Ndogholi Matembe - Ndiyo

Mhe. Silafu Jumbe Maufi - Ndiyo
Mhe. Lucy Thomas Mayenga - Ndiyo
Mhe. Kiza Hussein Mayeye – Ndiyo *(Makofi/ Vigelegele)*

Mhe. Mussa Bakari Mbarouk – Hapana
Mhe. Prosper Joseph Mbena – Hakuwepo
Mhe. Janet Zebedayo Mbene – Ndiyo
Mhe. Richard Philip Mbogo – Ndiyo
Mhe. Taska Restituta Mbogo – Ndiyo
Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki – Hapana
Mhe. Bhagwanji Maganlal Meisuria – Ndiyo
Mhe. Neema William Mgaya – Ndiyo
Mhe. Mahmoud Hassan Mgimwa – Ndiyo
Mhe. Godfrey William Mgimwa – Ndiyo
Mhe. Suzana Chogisasi Mgonukulima – Hapana
Mhe. Omary Tebweta Mgumba – Ndiyo
Mhe. Joseph Kizito Mhagama – Ndiyo
Mhe. Mboni Mohamed Mhita – Ndiyo
Mhe. Esther Lukago Midimu – Ndiyo
Mhe. Rehema Juma Migilla – Ndiyo*(Makofi/ Vigelegele)*

Mhe. James Kinyasi Millya – Hapana
Mhe. Desderius John Mipata – Ndiyo
Mhe. Nimrod Elirehema Mkono – Hakuwepo
Mhe. Martha Moses Mlata – Ndiyo
Mhe. Goodluck Asaph Mlinga – Ndiyo
Mhe. Lucia Michael Mlowe – Hapana
Mhe. Ester Michael Mmasi – Hakuwepo
Mhe. Ally Keissy Mohamed – Ndiyo
Mhe. Twahir Awesu Mohammed – Hapana
Mhe. Ibrahim Hassanali Mohammedali – Ndiyo
Mhe. Amina Saleh Mollel – Ndiyo
Mhe. Dkt. Godwin Oloyce Mollel – Ndiyo
Mhe. Justin Joseph Monko – Ndiyo
Mhe. Daimu Iddi Mpakate – Ndiyo
Mhe. Dkt. Hadji Hussein Mponda – Ndiyo
Mhe. Maryam Salum Msabaha – Hapana
Mhe. Jacqueline Ngonyani Msongozi – Ndiyo

Mhe. Martin Mtonda Msuha – Ndiyo
Mhe. Shamsia Aziz Mtamba - Ndiyo *(Makofi/ Vigelegele)*

Mhe. Daniel Edward Mtuka – Ndiyo
Mhe. Maulid Said Mtulia – Ndiyo
Mhe. Muhammed Amour Muhammed – Hakuwepo
Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo – Ndiyo
Mhe. Joyce John Mukya – Hapana
Mhe. Phillipo Augustino Mulugo – Ndiyo
Mhe. Mary Deo Muro – Hapana
Mhe. Benardetha Kasabago Mushashu – Ndiyo
Mhe. Mussa Hassan Mussa – Ndiyo
Mhe. Joseph Kasheku Musukuma – Ndiyo
Mhe. Hawa Subira Mwaifunga – Hapana
Mhe. Frank George Mwakajoka – Hapana
Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda – Hapana
Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata – Ndiyo
Mhe. Fredy Atupele Mwakibete – Ndiyo
Mhe. Edward Franz Mwalongo – Ndiyo
Mhe. Victor Kilasile Mwambalaswa – Ndiyo
Mhe. Venance Methusalah Mwamoto – Ndiyo
Mhe. Zainabu Nuhu Mwamwindi – Ndiyo
Mhe. Hasna Sudi Katunda Mwilima – Ndiyo
Mhe. Abbas Ali Mwinyi – Ndiyo
Mhe. Maftaha Abdallah Nachuma –Ndiyo *(Makofi/ Vigelegele)*

Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu – Ndiyo
Mhe. Shamsi Vuai Nahodha – Ndiyo
Mhe. Joshua Samwel Nassari – Hapana
Mhe. Suleiman Masoud Nchambi – Ndiyo
Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki – Ndiyo
Mhe. Richard Mganga Ndassa – Ndiyo
Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro – Ndiyo
Mhe. Deogratias Francis Ngalawa – Ndiyo
Mhe. Eng. Edwin Amandus Ngonyani – Ndiyo
Mhe. Stephen Hillary Ngonyani – Hakuwepo
Mhe. Ahmed Juma Ngwali – Hapana
Mhe. Oran Manase Njeza – Ndiyo

Mhe. William Dua Nkurua – Ndiyo
Mhe. Daniel Nicodemus Nsanzugwanko – Ndiyo
Mhe. Albert Obama Ntabaliba – Ndiyo
Mhe. Musa Rashid Ntimizi – Ndiyo
Mhe. Nassor Suleiman Omar – Hapana
Mhe. Lucy Fidelis Owenya – Hapana
Mhe. Upendo Furaha Peneza – Hakuwepo
Mhe. Haroon Mulla Pirmohamed – Ndiyo
Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajab – Ndiyo
Mhe. Shally Josepha Raymond – Ndiyo
Mhe. Catherine Nyakao Ruge – Hakuwepo
Mhe. Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare – Ndiyo
Mhe. Conchesta Leonce Rwamlaza – Hapana
Mhe. Machano Othman Said – Ndiyo
Mhe. Magdalena Hamis Sakaya – Ndiyo

*(Makofi/Vigelegele)*

Mhe. Mattar Ali Salum – Ndiyo
Mhe. Ahmed Ally Salum – Ndiyo
Mhe. Salum Khamis Salum – Ndiyo
Mhe. Saada Mkuya Salum – Ndiyo
Mhe. Deo Kasenyenda Sanga – Ndiyo
Mhe. Edwin Mgante Sannda – Ndiyo
Mhe. Njalu Daudi Silanga – Ndiyo
Mhe. Joseph Roman Selasini – Hapana
Mhe. Oliver Daniel Semuguruka – Ndiyo
Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby – Ndiyo
Mhe. Rashid Abdallah Shangazi – Ndiyo
Mhe. Shaabani Omari Shekilindi – Ndiyo
Mhe. Prof. Norman Adamson Sigalla King – Ndiyo
Mhe. Mussa Ramadhan Sima – Ndiyo
Mhe. George Boniface Simbachawene – Ndiyo
Mhe. Margaret Simwanza Sitta – Ndiyo
Mhe. Joyce Bitta Sokombi – Hapana
Mhe. Jitu Vrajlal Soni – Ndiyo
Mhe. Rose Kamili Sukum – Hakuwepo
Mhe. Khalifa Salum Suleiman – Ndiyo
Mhe. Sabreena Hamza Sungura – Hapana
Mhe. Grace Victor Tendega – Hakuwepo
Mhe. Anatropia Lwehikila Theonest – Hapana

| | |
|---|---|
| Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka | – Ndiyo |
| Mhe. Fatma Hassan Toufiq | – Ndiyo |
| Mhe. Salim Hassan Turky | – Ndiyo |
| Mhe. Rose Cyprian Tweve | – Ndiyo |
| Mhe. Martha Jachi Umbulla | – Ndiyo |
| Mhe. Ally Seif Ungando | – Ndiyo |
| Mhe. Khamis Ali Vuai | – Ndiyo |
| Mhe. Anastazia James Wambura | – Ndiyo |
| Mhe. Selemani Jumanne Zedi | – Hakuwepo |
| Mhe. Kabwe Zuberi Ruyagwa Zitto | – Hakuwepo |

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, tumemaliza zoezi la kupiga kura.

**SPIKA:** Ahsante Katibu. Sasa uendelee na kufanya *tallying,* mkishapata hesabu kamili mtatujulisha.

Kwenye kura ya wazi huwa hatuna wakala kwa sababu ni ya wazi, kila mtu anaona, ingekuwa kura ya siri tungeweka wakala. Mtaona kwamba Spika hajapiga kura ni kwa sababu zikifungana basi inakuwa zamu yangu kupiga kura ya Ndiyo. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya zoezi la kupiga kura kukamilika, Katibu na Wasaidizi wake walienda kuhesabu kura na sasa wameshakamilisha zoezi hilo, naomba sasa nimwite Katibu ili aweze kutoa matokeo ya kazi yetu. Katibu.

**MATOKEO YA UPIGAJI KURA WA BAJETI YA SERIKALI**

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, idadi ya Wabunge waliopo na ambao walipiga kura walikuwa 348; Wabunge ambao hawakuwepo Bungeni ni Wabunge 43. Kura za Hapana zilikuwa 82, hakuna kura ambayo haikuamua na kura za Ndiyo ni 266. *(Makofi/ Vigelegele)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa matokeo hayo sasa natangaza kwamba Bunge limekubali na kuyapitisha

mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa jinsi hiyo, nitoe pongezi nyingi sana kwa Serikali kwa ujumla wake, tukianzia na Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli; Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Hassan Suluhu; Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa; Waheshimiwa Mawaziri wote, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na Wataalam wao wote waliohusika na hii bajeti *circle* yote tangu ilikoanzia huko mpaka tumefika leo hapa ni safari ndefu sana. *(Makofi)*

Nawapongeza Mawaziri wote ambao walilazimika kufika hapa na kuomba bajeti za Wizara zao moja baada ya nyingine, kazi kubwa sana mlifanya, mmeenda kwenye Kamati zetu, mmejieleza na kujieleza tena na tena na mlipokuja hapa moto uliwaka.

Kipekee tumpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Naibu wake ambao wao sasa wakabeba ule mzigo wote katika ukubwa wake kwa maana ya bajeti nzima na kuiwasilisha hapa na tukawa na mjadala mkali sana. Naamini mjadala huu ulikuwa ni wa afya tu, naamini kabisa Serikali wenzetu tutakapokuwa tunaondoka tukifunga Ijumaa mtaondoka mkiwa mmesheheni ushauri mwingi sana kutoka kwa Wabunge. Ushauri huo ndio maoni ya wananchi mtaenda kuangalia maana ushauri ni ushauri, mtatazama mtaona nini cha kufanya. *(Makofi)*

Pia Waheshimiwa inabidi tuwakumbushe, muwe mnawakumbuka waliowapa bajeti hii mpaka ikapita, Eeeh! Siyo unapewa bajeti na hawa, unatumikia hawa, sasa inakuwa kidogo...! Siku nyingine wanaotoa bajeti watakuja kununa sasa sijui itakuwaje.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)*

**SPIKA:** Ninyi semeni hivyo tu bahati nzuri hawa ni watu wa Mungu sana, lakini wangeamua mwaka fulani kura zote

zingekuwa za ndiyo hizi, maana hawezi mtu akakukatalia bajeti halafu Bunge linalokuja anakuuliza swali una mpango gani wa daraja langu? Bajeti wewe si ulikataa? *(Makofi/ Kicheko)*

Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Mpango hivyo hii Mawaziri msikate tamaa, unajua hivi vitu, alikuwa ananikumbusha rafiki yangu mmoja enzi hizo tuko kule Mlimani Chuo Kikuu, palikuwa pana wanafunzi wanalipwa kiasi hiki lakini wakawa wanataka kiasi kile kiongezeke mara mbili, sasa wakaitana Nkurumah *Hall* wamejaa kama hivi, akaitwa *Vice Chancellor,* ndiyo wanatoa maoni yao kwa mara ya kwanza, wanamwambia *Vice Chancellor* tunataka iongezeke kuanzia hapa mpaka hapa, *we want our money*, wanamwambia *we want our money today, here and now.*

Kwa hiyo, unaweza ukaona ukiwa unashughulika na uongozi, magumu siyo ya kwako peke yako mpaka huko kwingine kote, mambo ya hela huwa ni magumu sana. Sasa watu wanakwambia, *we want our money today, here and now* yaani unafanya fanyaje mpaka zishuke, unakuwa ni Yesu, ni Mana ya kwamba zinateremka tu kwamba mikate hii sasa imeshakuwa kadhaa? Ni ngumu sana. *(Makofi)*

Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Phillip Mpango kwa hiyo, nasi tunataka yaani kikapu kile cha samaki kitutoshe Watanzania kwa wakati mmoja lakini kwa kawaida rasilimali hazitoshi. Katika kutokutosha kwa rasilimali ndiyo kelele zote hizi na lawama eeh! Hata utaasikia ana kiburi huyu, ana nini ni kwa sababu ya hizo rasilimali hazitoshi, zingekuwa zinatosha ni kicheko tu, kila mtu anaondoka na mafungu yake hapa na mafurushi, basi inakuwa hivyo, *otherwise* kwa kweli tunawashukuru kwa uvumilivu mkubwa ambao mmekuwa nao.

Vile vile Waheshimiwa Wabunge nanyi niwashukuru sana na kuwapongeza kwa jinsi ambavyo mmewachachafya Mawaziri, kabisa kabisa! Mnawachachafya kweli hasa upande huu, maana upande huu mmekataa hata kutoa maoni tangu tuanze hawaleti

maoni, hata maoni ya kesho hawana! sababu hawajaandikiwa, looh! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa David Silinde alitoa mpya siku hiyo, basi tunatumaini Bunge lijalo watawaandikieni halafu tutapata maoni mbadala.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya pongezi hizo nyingi sana ambazo tunazitoa kwa Serikali, tunawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa bajeti hii, tunaamini kwamba bajeti hii itatusogeza sana kutoka pale tulipo, kwenda hatua kadhaa mbele kiasi ambacho mwakani wakati huu tutakapokutana *Inshaallah*, basi tutakuwa tunazungumza mambo mengine na tutakuwa tunapongezana zaidi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno hayo, sasa Katibu kinachofuata.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kuidhinisha jumla ya Shilingi Trilioni Thelathini na Mbili, Bilioni Mia Nne Sabini na Tano, Milioni Mia Tisa Arobaini na Tisa, Laki Nne Themanini na Mbili Elfu na Mia Nne Kumi na Nane (32,475,949,482,418) kwa Matumizi ya Serikali kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2019; Kutumia fedha zilizoidhinishwa kwa mwaka huo, kuruhusu kuhamisha baadhi ya fedha pamoja na mambo yanayohusiana na malengo hayo. *(A bill for an Act to Apply some of Thirty Two Trillion, Four Hundred Seventy Five Billion, Nine Hundred Forty Nine Million, Four Hundred Eighty Two Thousand Four Hundred Eighteen Shillings* (32,475,949,482,418) *out of the Consolidated Fund to the service of the year ending on the* 30th *June,* 2019, *to appropriate the supply granted for that year, to authorizes the reallocation of certain appropriations and to provide for matters connected with those purpose).*

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama ambavyo Katibu ametuongoza tuko kwenye Muswada wa Sheria wa Kuidhinisha Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2018 *(The Appropriation Bill,* 2018). Utaratibu wa Muswada huo ni kwamba utapitishwa mfululizo kwa hatua zake zote bila mjadala, kwamba hautapelekwa kwenye Kamati yoyote ya Bunge ya Kudumu wala Kamati ya Bunge Zima, masharti kusuhu Muswada huu kusomwa kwa mara ya kwanza hayatatumika, hautatangazwa kwenye Gazeti kabla haujawasilishwa Bungeni. Tunaendelea, Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2018 *(The Appropriation Bill, 2018)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Katibu tena.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kuidhinisha jumla ya Shilingi Trilioni Thelathini na Mbili, Bilioni Mia Nne Sabini na Tano, Milioni Mia Tisa Arobaini na Tisa, Laki Nne Themanini na Mbili Elfu na Mia Nne Kumi na Nane (32,475,949,482,418) kwa Matumizi ya Serikali kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2019; Kutumia fedha zilizoidhinishwa kwa mwaka huo, kuruhusu kuhamisha baadhi ya fedha pamoja na mambo yanayohusiana na malengo hayo. *(A bill for an Act to Apply some of Thirty Two Trillion, Four Hundred Seventy Five Billion, Nine Hundred Forty Nine Million, Four Hundred Eighty Two Thousand Four Hundred Eighteen Shillings* (32,475,949,482,418) *out of the Consolidated Fund to the service of the year ending on the* 30th *June,* 2019, *to appropriate the supply granted for that year, to authorizes*

*the reallocation of certain appropriations and to provide for matters connected with those purpose).*

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa hatua hiyo na kwa utaratibu wa Muswada huu, huwa hatuwahoji. Kwa hiyo, niwatangazie tu moja kwa moja kwamba Muswada huu kwa maana ya hapa Bungeni tumeshaupitisha. Kwa kuupitisha kwetu maana yake sasa tutaupeleka kwa Mheshimiwa Rais ili tuweze kupata baraka za sahihi yake na ukishasainiwa basi tunaitakia Serikali utekelezaji mwema wa sheria hiyo mara itakapokuwa imeshawekwa sahihi na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mmefanya kazi kubwa kwa siku ya leo ni kazi ambayo itaingia katika historia ya Bunge la Kumi na Moja kama moja ya majukumu makubwa ambayo tumeyatekeleza, niwapongeze sana, kwenye meza yangu ya shughuli hapa, shughuli zote za leo zimekamilika, niwakumbushe tu kwamba kesho tutakuwa tunashughulika na ile *Finance Bill*.

Waheshimiwa Wabunge, kwa vile shughuli zangu zimekamilika hapa, naomba sasa niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 12.30 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 27 Juni, 2018, Saa Tatu Asubuhi)*